ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaybah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais

70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 13 Julai, 2010

(Mkutano ulianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kumwita Katibu kwa ajili ya utaratibu wa shughuli za leo, naomba nitoe taarifa kwamba jana wakati tunatoka Dodoma wenzetu basi ambalo lilikuwa limewachukua Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lilipata ajali ya kumgonga mtu, tulipata taarifa kwa bahati mbaya huyo mtu amefariki pale pale.

Kwa hivyo, mazingira hayo yalisababisha basi lile libakie pale na askari waje wafanyekazi yao na wale wajumbe wapelekewe basi jengine, hali ambayo iliwafanya washindwe kuwahi boti ya saa 10:00 ambayo ilipangwa iwachukue kwa ajili ya kuja hapa.

Kutokana na hali hiyo niombe radhi kwa niaba yao kwa kuchelewa kufika mapema kwa sababu hiyo, ambapo lilikuwa ni jambo ambalo hatuwezi tukalizuia kwani ni suala la ajali. Kwa hiyo, huyo aliyefariki Mwenyezi Mungu amlaze mahala anapostahiki naye.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ya mwaka 2010/2011.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumuzi ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman (Waziri Kivuli wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Maoni ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Ahsante sana.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 – Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto

Mhe. Spika, kwanza naomba radhi sana sauti yangu leo imekuwa na matatizo, kutokana na kushangiria kupita kiasi kule Makamo Makuu Dodoma. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili niweze kutoa maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (*Subuhanahu Wataalla*), mwenye wingi wa rehema, kutujaalia kukutana hapa leo katika Baraza hili Tukufu kujadili masuala muhimu tukiwa wazima, pamoja na kutujaalia salama, amani na utulivu katika nchi yetu.

Vile vile napenda kuchukua fursa hii kutoa salamu za pole kwa msiba kwa Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba pamoja na waheshimiwa wengine ambao wamepata misiba na Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi. Amin.

Mhe. Spika, kupitia Baraza lako Tukufu napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume kwa uongozi wake bora, wenye busara, hekima, uadilifu na uliothamini utu, ambao umetuletea maendeleo na mafanikio makubwa kwa wananchi wa Zanzibar kwa kipindi chake chote cha uongozi. Jitihada zake zinaonekana wazi na zimeleta maendeleo makubwa ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kuendeleza amani na utulivu nchini.

Mhe. Spika, nkupitia Baraza lako tukufu kwa heshima kubwa napenda naomba kuchukuwa nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Dkt. Ali Mohammed Sheni Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuchaguliwa kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar. Vile vile kwa dhati nampongeza sana Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kupata nafasi ya mara ya pili kugombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pongezi nyingi pia kwa Mhe. Dkt. Mohammed Gharib Bilal kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Jamhuri ya Muungano akiandamana na Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, kwa nafasi ya pekee nampongeza sana Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa na chama chake kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha na Naibu Waziri Kiongozi Mhe. Ali Juma Shamhuna kwa kuongoza vyema shughuli za serikali. Miongozo yao imesaidia kufanikisha shughuli za wizara yangu. *(Makofi)*

Aidha napenda kuchukua nafasi hii adhimu kukupongeza wewe Mhe. Spika kwa kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa hekima, busara na uadilifu katika kipindi chote cha miaka mitano. Uongozi wako umewezesha kutekeleza shughuli za serikali kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi wote wawili, Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi na Mhe. Ali Mzee Ali kwa kusaidia na wewe katika kuliendesha Baraza hili kwa ustadi, umakini pamoja na kufuata taratibu za Baraza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza lako Tukufu kwa ushirikiano, miongozo, maelekezo pamoja na ushauri wao kwa masuala ya wizara yangu, ambayo yametuwezesha kufanikisha shughuli zetu kwa mafanikio makubwa.

Kwa hivyo, nawapongeza sana Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii), Mhe. Ame Mati Wadi (Makamo Mwenyekiti). Aidha pongezi za dhati kwa Mhe. Aziza Nabahan Suleiman (Waziri Kivuli wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, kwa kuhamasisha pamoja na michango yake katika wizara hii. *(Makofi)*

Vile vile napenda kuishukuru Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya Baraza lako Tukufu, kwa miongozo na maelekezo yao yaliyotuwezesha kutunza hesabu na kuweka kumbukumbu za vifaa vya serikali kwa mujibu wa taratibu zilizopo. Nachukuwa nafasi hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu, kwa miongozo na michango yao iliyotuwezesha kutekeleza majukumu ya wizara yangu kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hotuba hii imezingatia mipango na mikakati mikuu ya serikali ambayo ni Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA), Malengo ya Milenia, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Sera za Kisekta pamoja na Mpango Mkakati

wa Wizara. Maeneo hayo yanalenga kuandaa mazingira mazuri yatakayosaidia ukuwaji endelevu wa uchumi na kuleta maendeleo ya taifa letu.

MALENGO MAKUU YA WIZARA

Mhe. Spika, wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 imejipangia kutekeleza malengo makuu, ambayo yamo katika Mpango Mkakati wa Wizara kama ifuatavyo:-

1. Kuimarisha uwezo wa wizara kiufundi na kiutendaji.

2. Kuhakikisha Mipango ya Kitaifa, kisekta, sheria, sera, kanuni na miongozo inayolenga katika kukuza ajira na kuimarisha utatu inaandaliwa na kutekelezwa.

3. Kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika sera, mipango, programu na bajeti.

4. Kuwajengea uwezo wa kiuchumi, kijamii na kisiasa, wanawake, vijana na jamii kwa ujumla.

5. Kuhakikisha masuala ya UKIMWI, Dawa za Kulevya, Mazingira na Utawala Bora yanazingatiwa katika shughuli za wizara.

6. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika nyanja za jinsia, Haki za Binadamu na masuala ya kazi.

7. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa, Sera, Sheria na programu zinazowalenga wanawake, watoto, vijana, waajiri na waajiriwa.

8. Kuijengea uwezo jamii kushiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2009/2010

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, Idara ya Mipango na Sera ndio kiungo kikuu cha uendeshaji wa kazi za wizara. Idara hii ina jukumu la kupanga, kuratibu na kusimamia shughuli zote za wizara zinazolenga kuwaletea maendeleo vijana, wanawake, watoto na jamii kwa ujumla. Idara pia ina jukumu la kusimamia mafunzo na

maslahi ya wafanyakazi kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wa mipango na programu za wizara.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, idara hii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi watendaji 35 wa wizara, ili kuwaongezea uwezo na ujuzi wa kazi zao.

2. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya wizara.

3. Kukiimarisha Kitengo cha Habari na kuendelea kukusanya habari na kutoa taarifa za maendeleo ya wizara.

4. Kutekeleza programu ya kupambana na UKIMWI katika maeneo ya kazi.

5. Kuendelea kukiimarisha Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini cha Wizara.

6. Kuandaa miradi na programu mbali mbali kwa ajili ya kutekeleza sera na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, idara imefanikiwa kuwapatia Mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi watendaji 31. Kati ya hao watendaji 10 ni wanaume na watendaji 21 ni wanawake. Kiambatisho nambari 1 kinaeleza zaidi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, idara imetayarisha vipindi vinne (4) ambavyo vimerushwa kupitia TVZ kwa lengo la kutoa habari, kushajiisha na kuielimisha jamii juu ya shughuli zinazofanywa na wizara.

MIRADI INAYOSIMAMIWA NA IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, idara hii katika kipindi cha mwaka 2009/2010 imesimamia utekelezaji wa miradi miwili (2) ifuatayo:-

1. Mradi wa Jinsia Zanzibar

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), wenye madhumuni ya kuisaidia Serikali

ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau mbalimbali kuweza kuzingatia masuala ya jinsia katika mipango na bajeti za maendeleo. Aidha, Mradi huu una madhumuni ya kujenga uwezo wa Taasisi mbalimbali na wananchi katika kupambana na udhalilishaji wa kijinsia.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Mradi huu umeweza kutekeleza yafuatayo:-

Mhe. Spika, wizara ilimuajiri mtaalamu wa masuala ya jinsia ambae alishiriki kikamilifu katika mchakato wa mapitio ya utayarishaji wa Mpango wa Pili wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA) ili kuhakikisha kuwa Mpango huo unazingatia ipasavyo masuala ya jinsia, yakiwemo mahitaji, haki na fursa za kimaendeleo zinawafikia wanawake na wanaume. Changamoto iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha kwamba kila sekta inatekeleza Mpango huo kwa kuzingatia masuala ya jinsia yaliyoainishwa katika MKUZA.

Mhe. Spika, Mradi umesimamia utayarishaji wa taarifa ya miaka 15 ya utekelezaji wa Azimio la Beijing la mwaka 1995. Taarifa hiyo iliwasilishwa katika mkutano wa Kimataifa wa Kamisheni ya Ustawi wa Wanawake ya Umoja wa Mataifa (*CSW*) uliofanyika New York mwezi Machi, 2010. Mkutano huu pamoja na mambo mengine, ulijadili taarifa za nchi kwa kipindi cha miaka 15 ya utekelezaji wa Azimio hilo na kupitisha maazimio maalumu kwa ajili ya kuendeleza utekelezaji wa Azimio la Beijing.

Mhe. Spika, Mradi wa Jinsia kwa kushirikiana na Idara ya Wanawake na Watoto ulisimamia Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, tarehe 8 Machi, ambapo kwa mwaka huu ujumbe ulikuwa “Miaka Kumi na Tano ya Beijing Wanawake Wanaweza Wapewe Nafasi”. Maadhimisho haya yalifanikishwa kwa kuendesha kongamano na maigizo ambayo yaliwashirikisha wananchi wapatao mia tano (500) wakiwemo maafisa wa Serikali, masheha, na wajasiriamali wanawake.

Wito ulitolewa kwa wanawake kujipanga vizuri kugombea nafasi za uwakilishi na ubunge katika majimbo yao ili kuweza kufikia asilimia hamsini katika uchaguzi wa mwaka huu (2010). Aidha, programu za vyombo vya habari vikiwemo vipindi vya redio, televisheni na makala mbali mbali yanayohusu ujumbe wa mwaka yalitayarishwa.

Mhe. Spika, mradi ulifanya maadhimisho ya siku 16 za wanaharakati dhidi ya ukatili wa kijinsia Unguja na Pemba. Maadhimisho hayo yaliwashirikisha wananchi mia tatu (300) kati ya hao wanawake mia mbili (200) na wanaume mia moja (100) kwa Unguja. Aidha kwa Pemba wananchi mia mbili (200) walishiriki, kati ya hao wanawake mia moja na thelathini (130) na wanaume

sabini (70). Mikutano miwili imefanyika, mmoja Mkoa wa Kaskazini na wa pili Mkoa wa Kusini Unguja ambayo imewashirikisha watu mia moja na hamsini (150) kila Mkoa katika kuadhimisha siku hiyo.

Kwa upande wa Pemba, mikutano miwili (2) ilifanyika Mkoa wa Kusini na Mkoa wa Kaskazini Pemba ambayo iliwashirikisha watu mia moja (100) kila Mkoa. Mikutano hiyo ilijadili kwa kina sheria na masuala yanayohusiana na udhalilishaji wa kijinsia. Baada ya mikutano hiyo, wajumbe walikubaliana kuunda na kuziimarisha Kamati za Utendaji za Kudhibiti Unyanyasaji wa Kijinsia katika Shehia zao ili kupunguza kesi za aina hii.

Mhe. Spika, katika kuendeleza juhudi za kupinga udhalilishaji wa kijinsia, Mradi kwa kushirikiana na Idara ya Wanawake na Watoto ulifanya makongamano mawili (2) ambayo yaliwashirikisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, watendaji wa vyombo vya sheria pamoja na viongozi wa dini. Makongamano hayo yalijadili taarifa ya uchambuzi wa sheria na taratibu dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia, ambapo baadhi ya sheria zilibainika kuwa na mapungufu yanayopaswa kufanyiwa kazi na Taasisi husika.

Mhe. Spika, katika kuunga mkono juhudi za kupinga udhalilishaji wa kijinsia, Mradi umefanya tathmini iliyohusisha baadhi ya Kamati zilizoanzishwa katika ngazi mbali mbali. Lengo la tathmini hiyo ni kutambua uwezo walionao, changamoto zinazowakabili na mahitaji katika kufanikisha majukumu yao. Taarifa ya tathmini hiyo itatusaidia kuweka mkakati wa kuzijengea uwezo na kutoa muongozo kwa wadau wengine watakaokuwa tayari kuzisaidia Kamati hizo.

Aidha Mradi umeendesha mafunzo ya wiki moja kwa wajumbe thelathini na tano (35) wa Kamati za kupinga udhalilishaji wa wanawake na watoto za Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na Shehia tano (5) za Mkoa huo. Mafunzo hayo yalizingatia mapungufu yaliyobainishwa katika tathmini.

Mhe. Spika, mradi umeendesha mafunzo ya ushauri nasaha kwa watendaji thelathini na moja (31) kati ya hao wanawake ishirini na nne (24) na wanaume saba (7) wa vitengo vya ushauri nasaha ambapo kwa wizara yetu washiriki kumi na tatu (13), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii sita (6), Polisi watano (5), Mahakama watatu(3) na asasi zisizo za kiserikali wanne (4).

Lengo ni kukuza utendaji wao katika kutoa ushauri nasaha kwa waathirika wa kesi za udhalilishaji. Aidha katika kuhakikisha masuala ya unyanyasaji wa kijinsia yanapungua, tayari baadhi ya Shehia za Wilaya za Kaskazini “A” na “B” zimeanzisha Kamati zitakazosimamia na kufuatilia matukio yote ya kesi za

udhalilishaji wa kijinsia. Jumla ya Kamati kumi na nane 18 za Shehia zimeundwa. Kiambatisho nambari 2 kinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, ili kukuza uzingatiaji wa masula ya jinsia katika sekta mbali mbali, Mradi wa Jinsia ulisimamia ukaguzi wa masuala ya jinsia uliohusisha Wizara yangu, Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mradi huu pia ulisimamia tathmini ya upangaji na utumiaji wa rasilimali kwa mtazamo wa kijinsia ambao ulihusisha Mfuko wa Elimu ya Juu ulioko Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Kitengo cha utoaji wa huduma za afya ya uzazi kilichopo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Taarifa za tathmini hizi zitasaidia katika kuimarisha upatikanaji wa elimu ya juu kwa wanawake na kuimarisha huduma za afya ya uzazi kwa kinamama.

2. Programu ya Kuijengea Uwezo Wizara (*JP5*).

Mhe. Spika, programu hii inalenga kutekeleza Mkakati wa Kupunguza Umasikini Zanzibar, kwa njia ya kuongeza ajira, kujenga uwezo kwa Taasisi za Serikali na Binafsi katika kutekeleza sheria za kazi, kutoa mafunzo kwa wajasiriamali, kuweka mfumo imara wa Hifadhi ya Jamii kwa wote nchini na kujenga uwezo kwa Taasisi husika katika utekelezaji wa sera ya ajira na mpango wa kukuza ajira kwa vijana.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

Mhe. Spika, Kituo cha Kutoa Taarifa kwa Waomba Kazi na Wajasiriamali, ambacho kimejengwa na wizara kupitia Progaramu hii kimekamilika na ununuzi wa vifaa umefanywa. Kituo hicho kitawawezesha vijana na wajasiriamali kufahamu fursa za ajira zilizopo ndani na nje ya nchi ili waweze kuomba nafasi hizo na kupata ajira. Aidha kitawasaidia wajasiriamali kutambua fursa za masoko. Hii itawawezesha kutangaza na kuuza bidhaa zao kiurahisi kwa njia ya mtandao.

Mhe. Spika, Kanuni za sheria mbili za kazi (sheria ya Ajira na Sheria ya Uhusiano Kazini) zimetayarishwa jambo ambalo litarahisisha utekelezaji wa sheria husika.

Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) kupitia Mradi wa *JP5* imetoa vifaa vya skuli kwa watoto mia mbili (200) kati ya hao wanawake ni themanini na saba (87) na wanaume mia moja na kumi na tatu (113) kwa Shehia za Nungwi na Mkokotoni kwa Unguja, na watoto mia mbili (200) kati ya hao wanawake ni mia moja na ishirini na sita (126) na wanaume ni sabini na nne (74) kwa Shehia za Micheweni, Wete, Chake Chake na Mkoani kwa Pemba waliookolewa katika mazingira magumu ya Ajira za

Watoto na kurejeshwa skuli. Watoto hao walipatiwa sare za skuli, mikoba, madaftari na vifaa vyengine vya skuli.

Kwa Shehia ya Nungwi, vijiji vilivyonufaika ni Banda Maji, Mji kati, Mgagadu, Kiungani, Muwanda, Kendwa, Mchangani, Kikwajuni na Kinyasini ambapo kwa Shehia ya Mkokotoni ni vijiji vya Kiongole, Mwanzo mgumu, Kicheche, Kibaoni, Mzingani, Ikulu, Mzambarauni, Kibonde tondoo, Uwanja wa mpira na Mawimbini. Vijiji vya Pemba vilivyofaidika ni Ng'ombeni na Uweleni kwa Wilaya ya Mkoani, Selemu na Jadida kwa Wilaya ya Wete, Konde na Kifundi kwa Wilaya ya Micheweni na Kwale, Mjananza na Michungwani kwa Wilaya ya Chake Chake. Kiambatisho nambari 3 kinatoa maelezo zaidi.

Katika kuhakikisha kuwa watoto hao wanaendelea na skuli na hawarejei katika mazingira hatarishi walikokuwepo, Wizara kupitia mradi huu umewapatia mafunzo wanawake kwa upande wa Pemba wa maeneo yaliyotajwa kuhusu utengenezaji wa sabuni na chaki ili waweze kujiajiri wenyewe. Vile vile kwa kuanzia wamepewa vifaa mbali mbali zikiwemo mashine za kutengenezea chaki, unga wa chaki pamoja na vifaa vya kutengenezea sabuni.

Mhe. Spika, Rasimu ya awali ya Sera ya Mafunzo ya Kazi imekamilika. Sera hiyo itasaidia kuweka mfumo mzuri wa mafunzo ya kazi kwa vijana nchini. Sera hii inalenga kuweka utaratibu maalum wa kuwapatia mafunzo ya kazi vijana wanaojifunza kazi za amali katika sekta isiyo rasmi. Sera hii itawawezesha vijana wanaohitimu mafunzo kutambulika na kuweza kuajirika katika sekta rasmi kulingana na taaluma na ujuzi waliojifunza. Sambamba na hilo, Programu imekamilisha Mpango wa Taifa wa Kupambana na Ajira za Watoto ambapo jumla ya nakala mia mbili (200) za mpango huo zimechapishwa.

Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) imekamilisha Utafiti wa Mfumo wa Hifadhi ya Jamii kwa wote na hivi sasa imo katika mchakato wa kutayarisha Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar. Kukamilika kwa sera hii kutawezesha kuwa na mfumo mzuri wa hifadhi ya jamii nchini.

Mhe. Spika, wizara imesimamia matayarisho ya eneo la ujenzi wa Vituo vya Mafunzo ya Ujasiriamali kwa vijana. Matayarisho hayo yameanza kwa upande wa Muungoni Unguja.

PROGRAMU YA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI

Mhe. Spika, katika kipindi hiki, wizara imeweza kutekeleza programu ya UKIMWI kama ifuatavyo:-

- Kuhamasisha kujikinga na UKIMWI kwa wafanyakazi wa wizara yangu kupitia vikao.

- Kuhamasisha watoto kutoka sehemu mbali mbali za Pemba wakiwemo kutoka Mabaraza ya Watoto, watoto wanaoishi katika mazingira magumu na wanaoishi na virusi vya UKIMWI, ili kupata ufahamu kuhusu namna ya kujikinga na maradhi ya UKIMWI.

- Kuhamasisha wafanyakazi wa wizara na familia zao kupima afya zao na kujikinga na maambukizo ya UKIMWI, ambapo jumla ya wafanyakazi 30 walipimwa afya zao.

MALENGO YA IDARA YA MIPANGO NA SERA KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi watendaji wa wizara, ili kuwaongezea uwezo na ujuzi wa kazi zao.

2. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya wizara.

3. Kutekeleza programu ya kupambana na UKIMWI katika maeneo ya kazi.

4. Kuandaa miradi na programu mbali mbali kwa ajili ya kutekeleza sera na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar.

5. Kukiimarisha Kitengo cha Habari na kuendelea kukusanya habari na kutoa taarifa za maendeleo ya wizara.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango na Sera iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi milioni mia nne na kumi na tano elfu, laki moja na arobaini na mbili elfu (415,142,000/-) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi milioni ishirini (20,000,000/-) kwa kazi za maendeleo.

KAMISHENI YA KAZI

Mhe. Spika, Kamisheni ya Kazi ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi katika sekta ya umma na sekta binafsi nchini, sambamba na kusimamia

masuala ya usalama na afya kazini, kushughulikia suala la ajira pamoja na utoaji wa elimu kwa waajiri, waajiriwa na jamii kwa ujumla.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Kamisheni ya Kazi ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kutekeleza Sera ya Ajira, Mpango wa Kukuza Ajira, Mpango wa Kudhibiti Ajira ya Watoto na kanuni za kazi.

2. Kukiimarisha Kitengo cha Ajira ili kiweze kuweka takwimu za ajira kwa lengo la kupunguza ajira kwa wageni.

3. Kuimarisha Kitengo cha usuluhishi wa migogoro ya kazi, usalama na afya kazini na Afisi ya Mrajis wa vyama vya wafanyakazi na waajiri.

4. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za kazi za Tanzania Bara pamoja na kukuza ushiriki katika mikutano ya Kimataifa, Kikanda na Afrika Mashariki.

5. Kusimamia sheria za kazi pamoja na kumalizia uundaji wa kanuni za kazi kwa sheria mbili zilizobaki.

6. Kufanya tathmini ili kupata taarifa yakinifu zitakazosaidia Bodi ya Ushauri ya Mishahara katika mapendekezo ya kima cha chini cha mishahara.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Kamisheni ya Kazi kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* ilifanya utafiti wa kuangalia hali halisi ya Taasisi mbalimbali za kazi. Rasimu ya awali ya ripoti ya utafiti huo imekamilika na imewasilishwa kwa wadau wa masuala ya kazi ili kutoa maoni yao. Aidha Kamati ya Kitaifa ya Utatu ya kusimamia Mradi wa Kukuza Utekelezaji wa Sheria za Kazi imeundwa ili iweze kufanya kazi za usimamizi wa mradi huo.

Mhe. Spika, Kamisheni kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* chini ya mradi wa utekelezaji wa sheria za kazi imetoa mafunzo ya sheria za kazi kwa viongozi wa vyama vya wafanyakazi na Jumuiya ya Waajiri juu ya sheria za kazi nchini, lengo ikiwa ni kuongeza ufanisi na kuweka mazingira bora katika sehemu za kazi. Vile vile mafunzo juu ya majadiliano na mapatano sehemu za kazi yalitolewa kwa baadhi ya watendaji wa Serikali, Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Kazi, Jumuiya ya Waajiri na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi ili kusaidia kuziwezesha pande husika kuingia katika makubaliano na kuwa na mikataba ya hiari ambayo itainua maslahi ya

wafanyakazi na kujenga ari ya ufanisi kazini pamoja na kupunguza migongano sehemu za kazi.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Kazi imewapatia mafunzo ya utatuzi wa migogoro ya kazi wafanyakazi wa Kitengo cha Usuluhishi wa Migogoro, maafisa na wakaguzi kazi, maafisa wa Jumuiya ya Waajiri pamoja na maafisa kutoka Vyama vya Wafanyakazi. Mafunzo hayo yalijumuisha maafisa ishirini (20) ambapo kumi (10) ni wanawake na kumi (10) ni wanaume. Wizara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki imewapatia mafunzo maafisa watatu (3) wa Kitengo cha Usalama na Afya Kazini, mafunzo ambayo yaliendeshwa na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Finland. Wizara ilipokea baadhi ya vitabu muhimu vya masuala ya usalama na afya kazini ambavyo vinatumika kwa sasa. Chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kitengo hiki kimewekwa katika mpango wa miaka minne wa kuimarishwa zaidi. Vile vile Afisi ya Mrajisi wa Vyama vya Wafanyakazi inaendelea kuimarishwa kwa kupatiwa mafunzo chini ya Mradi wa Kuimarisha Utekelezaji wa Sheria za kazi.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Kamisheni ya Kazi imeendeleza mashirikiano na Taasisi za kazi za Tanzania Bara zikiwemo Idara ya Kazi, Idara ya Ajira, Jumuiya ya Waajiri *(ATE)*, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi *(TUCTA)*, Mamlaka ya Afya na Usalama Kazini na Kitengo cha Taarifa za Wafanyakazi *(Labour Market Information Centre).* Kamisheni imeshiriki katika majadiliano ya soko la pamoja la Afrika Mashariki kwa masuala ya kazi ambapo utekelezaji wake unaanza mwezi Julai mwaka huu. Kamisheni inaendelea kushiriki katika mikutano ya Kimataifa ambayo inaitishwa na Shirika la Kazi Duniani *(ILO).* Aidha Kamisheni ya kazi inashirikiana na Taasisi za Tanzania Bara katika kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo, ikiwemo miradi ya Kuimarisha Utekelezaji wa Sheria za Kazi, Hifadhi ya Jamii pamoja na Mradi wa Kupambana na Ajira za Watoto.

Mhe. Spika**,** Kamisheni ya Kazi imeendelea na usimamizi wa sheria za kazi ambapo ilifanya ukaguzi kazi kwa Taasisi za kazi mia moja na ishirini na tatu (123) na ukaguzi wa Usalama na Afya Kazini kwa Taasisi mia moja na thelanini (130) ***(Kiambatisho nambari 4).*** Aidha kwa Unguja, migogoro ya kazi mia moja na thelathini na saba (137) imepokelewa na mia moja na nne (104) imepatiwa ufumbuzi, migogoro thelathini na mbili (32) inaendelea kushughulikiwa na mgogoro mmoja (1) umepelekwa Mahakamani na kwa Pemba migogoroo kumi (10) imepokelewa ambapo tisa (9) imepatiwa ufumbuzi na mmoja unaendelea kutafutiwa ufumbuzi. ***(Kiambatisho nambari 5a na 5b).*** Vile vile Kamisheni ya Kazi kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* imeandaa rasimu za Sheria mbili (2) za kazi ambapo kwa sasa rasimu hizo zinarekebishwa kutokana na maelekezo ya Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Kazi.

Mhe. Spika, Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* Kamisheni inaendelea kufanya utafiti ili kupata taarifa yakinifu katika mapendekezo ya kuweka kima cha chini cha mshahara. Wataalamu kutoka Makao Makuu ya Shirika la Kazi Duniani *(ILO - Geneva)* wamefika Zanzibar kuonana na wadau mbalimbali wa sekta za umma na binafsi ili kupata maoni yao, ushauri na mapendekezo ili utafiti uanze.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Kazi inaendelea kutoa elimu kupitia njia ya redio na semina sehemu za kazi. Jumla ya vipindi ishirini na moja (21) vimerushwa hewani kati ya Julai 2009 hadi sasa kupitia Sauti ya Tanzania Zanzibar. Aidha elimu ya kupambana na ajira za watoto imetolewa kwa Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Ajira hizo, pamoja na viongozi wa Shehia za Nungwi, Mkokotoni, Kizimkazi na Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2009 hadi kufikia mwezi wa Machi mwaka huu jumla ya Shilingi milioni thelathini na nane, laki tatu na themanini na sita elfu, mia moja na hamsini (38,386,150/=) zimekusanywa, kati ya Shilingi milioni sitini (60,000,000/=) zilizokadiriwa kukusanywa. Hii ni sawa na asilimia 63.9%.(***kiambatisho nambari 6)***

MALENGO YA KAMISHENI YA KAZI KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Kamisheni ya Kazi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuendelea na utekelezaji wa Sera ya Ajira kwa kufanyia marekebisho baadhi ya sheria za kazi, pamoja na kuanzisha na kuzijengea uwezo Kamati za kisekta za kukuza ajira katika mikoa na Wilaya.

2. Kuanza mchakato wa kutayarisha Sera ya Hifadhi ya Jamii kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi na wadau wengine.

3. Kuimarisha masuala ya utatu na kuongeza uwezo wa wafanyakazi na waajiri kuhusu majadiliano ya pamoja sehemu za kazi.

4. Kuziimarisha na kuziendeleza Taasisi za kazi.

5. Kuimarisha masuala ya usalama na afya sehemu za kazi.

6. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa kutokomeza Ajira za Watoto.

7. Kuimarisha ukaguzi na kusimamia sheria za kazi pamoja na uundwaji wa kanuni za sheria za kazi.

8. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za kazi za Tanzania Bara pamoja na kukuza ushiriki katika mikutano ya Kimataifa, Kikanda na Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, Ili Kamisheni ya Kazi iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi milioni mia moja na sitini na tano, laki nne na themanini na nane elfu (165,488,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi milioni kumi (10,000,000/=) kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA MAENDELEO YA VIJANA

Mhe. Spika, Idara hii inasimamia sera na mipango ya kuwawezesha vijana kujiimarisha kiuchumi na kijamii. Aidha inaandaa mipango ya maendeleo ya vijana kwa kushirikiana na Taasisi mbali mbali za vijana na zinazohusiana na vijana.

Mhe. Spika, mwaka 2009/2010 Idara ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuendelea na hatua ya kuunda Baraza la Vijana la Zanzibar.

2. Kuchapisha nakala zaidi za Sera ya Maendeleo ya Vijana na kuendelea kuhamasisha utekelezaji wake.

3. Kuratibu na kusimamia Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa.

4. Kuendeleza na kuimarisha vikundi vya vijana vya uzalishaji mali kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali, uongozi na utunzaji wa hesabu za fedha.

5 Kusimamia Mpango wa Kukuza Ajira kwa vijana (Awamu ya mwanzo ya majaribio) unaolenga kuanzisha miradi ya kiuchumi kwa Vijana wasiokua na ajira Unguja na Pemba.

6 Kuanzisha kituo cha majaribio cha miradi ya kiuchumi ya vijana Unguja.

7 Kukusanya takwimu za vijana na shughuli za kiuchumi na kijami kwa kila Wilaya.

8 Kuandaa na kutekeleza mpango wa malezi kwa vijana kwa kutoa mafunzo ya ushauri nasaha, stadi za maisha, afya ya uzazi, vita dhidi ya ukimwi na dawa za kulevya.

Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Vijana katika kipindi cha mwaka 2009/2010 imeendelea na mchakato wa uundaji wa Baraza la Vijana la Zanzibar ambapo Katiba ya Baraza hilo iliyoandaliwa kwa lugha ya Kiingereza imetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, ili kuwawezesha wadau wake kufahamu Katiba ya Baraza hilo na kutoa fursa kwa vijana wengi wenye viwango vya elimu tofauti kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kuanzisha Baraza lao. Hatua za kukamilisha uundaji wa Baraza hilo zinaendelea.

Mhe. Spika, Kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudimia Watoto Duniani *(UNICEF),* nakala elfu mbili (2,000) za Sera ya Maendeleo ya Vijana zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau.

Mhe. Spika, Tarehe 12 Agosti ya kila mwaka, Idara huadhimisha siku ya Kimataifa ya Vijana Duniani kwa kuwakusanya vijana wa mikoa yote ya Zanzibar kukaa pamoja kutafakari utekelezaji wa sera yao, kujadili mambo yanayowahusu, kubadilishana uzoefu wa namna ya kutatua matatizo yao kama vile utunzaji wa mazingira, kuhamasishwa kuwa sekta binafsi ni mkombozi wa tatizo la ajira pamoja na vijana kuhamasishana kupambana na UKIMWI na dawa za kulevya. Kwa mwaka 2009, Idara iliadhimisha siku hiyo kwa kufanya mkutano wa siku tatu wa Kamati ya Utekelezaji wa sera ili kuona namna ya sera ilivyotekelezwa na sekta tofauti za Serikali na zisizo za kiserikali. Aidha Idara ilifanya mkutano wa siku mbili uliozijumuisha jumuiya za vijana za Unguja na Pemba kwa lengo la kukusanya maoni kuhusu utekelezaji wa sera kupitia jumuiya za vijana.

Mhe. Spika, Katika kuendeleza mashirikiano kati ya vijana wa Zanzibar na vijana wengine duniani kwa mwaka 2009/2010 Makambi Kazi kumi (10) yaliandaliwa katika Wilaya za Kusini , Magharibi na Kati Unguja ambapo yaliwashirikisha vijana themanini (80) kutoka nchi za Afrika, Asia, Ulaya na Amerika ya Kaskazini, kati yao wanaume ni hamsini (50) na wanawake thelathini (30). Aidha vijana kumi (10) wa Zanzibar walipatiwa fursa ya kushiriki kambi kazi nchini Kenya, Canada, Ujerumani, Ireland na Hispania. (***Kiambatisho nambari 7)***

Mhe. Spika, Katika kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru, kwa mwaka 2009, jumla ya miradi tisini na nane (98) yenye thamani ya Shilingi bilioni mbili, milioni mia nane na themanini na nne, laki nane na na arobaini na moja elfu na hamsini na mbili (2,884,841,052) ilitembelewa wakati wa mbio hizo. Miradi hiyo ilichangiwa na wadau mbali mbali pamoja na nguvu za wananchi (***Kiambatisho nambari 8).*** Idara ilikuwa mwenyeji wa Tathmini ya Mbio za

Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2009 ambapo washiriki mia moja na hamsini (150) kutoka mikoa yote ya Tanzania walihudhuria.

Mhe. Spika, Idara imeratibu uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2010 ambapo mbio za mwaka huu zimezinduliwa katika Mkoa wa Manyara na Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Ali Moh'd Shein. Ambae ndiye atakuwa Rais wa Zanzibar tukijaaliwa. Ujumbe wa mwaka huu ni "Mapambano dhidi ya malaria, uhamasishaji wa wananchi kushiriki uchaguzi mkuu kwa amani, utulivu na mshikamano". Aidha ujumbe wa kudumu wa mapambano dhidi ya UKIMWI, rushwa na dawa za kulevya unahusika. Mbio za mwaka huu zitafikia kilele chake tarehe 14, Oktoba mkoani Kigoma.

Mhe. Spika, Idara imefanya tathmini za shughuli za vikundi vya vijana na wajasiriamali ili kujua shughuli zao za maendeleo, kutoa mafunzo ya mbinu ya uzalishaji na uwekaji kumbukumbu sahihi ili waweze kufanya shughuli zao kwa uhakika na kitalaamu zaidi. Jumla ya Vikundi kumi na nne (14) vya mikoa ya Unguja vilifanyiwa tathmini vyenye wajasiriamali mia moja na kumi na tisa (119), wakiwemo wanawake arobaini na saba (47) na wanaume sabini na mbili (72). Aidha kwa upande wa Pemba, jumla ya vikundi kumi na sita (16) vyenye wajasiriamali mia moja na sabini (170) vilifanyiwa tathmini za shughuli zao kati ya hao wanawake walikuwa tisini (90) na wanaume themanini (80) ***(Kiambatisho nambari 9a na 9b).***

Mhe. Spika, Katika kuendeleza mafunzo ya maadili mema kwa Taifa sambamba na kuwafahamisha vijana kujitambua na kujua umuhimu wao kwa jamii, Idara kwa kushirikiana na Tume ya UKIMWI Zanzibar na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa msaada wa Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu Duniani *(UNFPA)* imo katika mchakato wa kuandaa mpango wa mafunzo ya stadi za maisha *(National Framework of Life Skills).* Katika mchakato huo maoni mbali mbali ya vijana, jumuiya za vijana na vikundi vya vijana vijiweni na Jumuiya za Dini yamezingatiwa na kuingizwa ili kuimarisha mpango huo. Vile vile Idara itaandaa kitini cha kufundishia stadi za maisha kwa Zanzibar baada ya kukamilika mpango huo. Aidha Idara imeshirikiana na Vijana wa Skauti kwa kutoa mafunzo ya stadi za maisha na vita dhidi ya Dawa za Kulevya, juu ya kujikinga na maradhi ya UKIMWI na mimba katika umri mdogo. Jumla ya Vijana 37 wa skauti wa kijiji cha Vikunguni na Wawi Pemba wamepatiwa mafunzo hayo kupitia mradi wa *"Absent behavior change for youth" (ABY) wa USAIDS.*

MALENGO YA IDARA YA MAENDELEO YA VIJANA KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, Katika mwaka 2010/2011, Idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuendelea na hatua za uundaji wa Baraza la Vijana Zanzibar

2. Kuratibu na kusimamia Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana

3. Kuendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano kwa Taasisi za vijana ndani na nje ya nchi pamoja na kuendeleza kambi kazi za vijana Zanzibar.

4. Kuendeleza na kuimarisha vikundi vya vijana vya uzalishaji mali kwa kutoa mafunzo ya uanzishaji na uendelezaji wa *SACCOS* na ujasiriamali, uongozi na utunzaji wa hesabu.

5. Kuendeleza mafunzo ya Mpango wa Kukuza Ajira kwa vijana katika sekta za kilimo, biashara na utalii

6. Kuandaa na kutekeleza mpango wa malezi kwa vijana kwa kutoa mafunzo ya ushauri nasaha, stadi za maisha, afya ya uzazi, vita dhidi ya UKIMWI na dawa za kulevya.
7. Kuadhimisha siku ya Kimataifa ya Vijana Duniani.

Mhe. Spika, Ili Idara ya Maendeleo ya Vijana iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi milioni sabini na tatu, laki tatu na thelathini elfu (73,330,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi milioni thelathini (30,000,000/=) Kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa, Kikanda na sheria, sera na programu zinazohusu ukuzaji wa uhai, hifadhi na maendeleo ya wanawake na watoto Zanzibar.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 Idara hii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na kulinda haki za wanawake na watoto pamoja na kushajihisha jamii kuziheshimu.

2. Kuinua hali za wanawake kiuchumi kwa kuwapatia ushauri na mafunzo.

3. Kuendelea na utayarishaji wa sheria ya mtoto.

4. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa na Kimataifa katika kuhakikisha kuwa haki za wanawake na watoto zinalindwa.

5. Kutoa mafunzo kuhusu Sera ya Hifadhi na Maendeleo ya Wanawake na Sera ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Watoto kwa waratibu wa maendeleo ya wanawake na watoto wa Shehia.

Mhe. Spika, Idara imeshughulikia na kuyapatia ufumbuzi malalamiko ya wanawake mia moja na kumi na nne (114) kwa Unguja ***(Kiambatisho nambari 10a*** na malalamiko thelathini (30) kwa Pemba ***(Kiambatisho nambari 10b)*** na malalamiko ya watoto mia mbili (200) kwa Unguja ***(Kiambatisho nambari 11a)*** na malalamiko mia moja na sitini na mbili (162) kwa Pemba ***(Kiambatisho nambari 11b).*** Malalamiko hayo yalihusu; huduma za watoto, kutelekezwa, mgawanyo wa mali**,** mimba nje ya ndoa, migogoro ndani ya ndoa, mimba za umri mdogo, mvutano wa malezi, ukatili kwa watoto, mauaji ya watoto, kutoroshwa na udhalilishaji wa wanawake.

Mhe. Spika, Idara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeendesha midahalo kwa wanafunzi wa skuli ishirini na nne (24) za Wilaya zote za Unguja kuhusu unyanyasaji wa kijinsia (***Kiambatisho nambari 12).*** Lengo la midahalo hiyo ni kuwaelimisha wanafunzi hao juu ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia pamoja na mbinu za kujilinda na vitendo hivyo. Katika midahalo hiyo wanafunzi walipendekeza njia za kupambana na vitendo ya udhalilishaji, miongoni mwa njia hizo ni:-

1. Kuundwa kwa Kamati ya kuchunguza vitendo vya udhalilishaji wanafunzi hasa vile vinavyowahusisha walimu.

2. Sheria kali zichukuliwe kwa walimu watakaobainika kuwadhalilisha wanafunzi ili iwe fundisho kwa wengine.

3. Kuimarishwa vitengo vya ushauri nasaha vya maskuli ili kuweza kuwahudumia wanafunzi ipasavyo.

4. Kuipitia upya miundo na mifumo ya Kamati za maskuli ili ziweze kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, Idara ya Wanawake na Watoto ilitoa mafunzo ya siku tano kwa watendaji wa vyombo vya habari ambapo jumla ya waandishi thelathini (30) kutoka vyombo vya habari vya Zanzibar wamepatiwa mafunzo juu ya namna ya kuripoti habari za udhalilishaji wa kijinsia kulingana na mikataba ya haki za binaadamu na sheria za nchi.

Mhe. Spika, Idara ya Wanawake na Watoto kwa mashirikiano na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani *(UNICEF)* inaendelea kutayarisha sheria ya mtoto, na tayari rasimu ya kwanza imeshajadiliwa na wadau wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wanasheria, askari magereza, polisi, mahakimu, watendaji wanaoshughulikia masuala ya haki na ustawi wa watoto, afya, elimu pamoja na wajumbe kutoka Taasisi zisizo za kiserikali. Ili kuhakikisha sheria inazingatia maadili ya dini, kikao cha viongozi wa dini kimefanyika na kupata michango yao. Rasimu hiyo itawasilishwa kwa watoto ili kupata mawazo yao.

Mhe. Spika, Tarehe 16 Juni ya kila mwaka, ni siku ya maadhimisho ya Mtoto wa Kiafrika. Maadhimisho ya mwaka huu yamefanyika katika ngazi ya Taifa kwa kutoa taarifa maalum juu ya siku hii ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kwa Ripoti ya Kitaifa juu ya hali ya watoto nchini. Ripoti hiyo huwasilishwa katika Baraza lako Tukufu na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza kutoa maoni, maelekezo na miongozo kwa ajili ya kuifanyia kazi ili kuhakikisha udhalilishaji wa watoto wa aina zote unamalizika.

MALENGO YA IDARA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na kulinda haki za wanawake na watoto.

2. Kuinua hali za wanawake kiuchumi kwa kuwapatia ushauri na mafunzo.

3. Kumalizia utayarishaji wa sheria ya mtoto.

4. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa na Kimataifa katika kuhakikisha kuwa haki za wanawake na watoto zinalindwa.

5. Kusambaza na kutoa taaluma juu ya Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake *(CEDAW)* ili ueleweke zaidi na jamii.

6. Kushajihisha jamii juu ya haki na maendeleo ya wanawake na watoto.

Mhe. Spika, Ili Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi milioni themanini na saba na laki tano (87,500,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MAENDELEO YA JAMII

Mhe. Spika, Idara hii ni kiungo muhimu kati ya jamii na Serikali, ina jukumu kubwa la kuunganisha pamoja nguvu za Serikali, wananchi na wadau wengine wote katika kuleta maendeleo endelevu ya jamii. Idara pia ina jukumu la kuelimisha jamii juu ya masuala yanayohusiana na ustawi na maendeleo ya jamii.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ililenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kutekeleza na kusimamia Sera ya Maendeleo ya Jamii na Mpango Kazi wa Sera hiyo.

2. Kuzijengea uwezo Kamati za Maendeleo kwa kuwapatia mafunzo yanayohusu usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

3. Kufuatilia na kutathmini miradi ya maendeleo iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

4. Kuimarisha uwezo wa Idara.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Idara imechukua hatua mbali mbali za kuhakikisha maendeleo ya jamii yanaimarika, miongoni mwa hatua hizo ni kukamilisha Sera ya Maendeleo ya Jamii. Mchakato wa uandaaji wa Sera ya Maendeleleo ya Jamii ulipitia hatua mbali mbali hadi kukamilika kwake mwezi Septemba, 2009. Azma ya Idara ni kuhakikisha kwamba Sera inafahamika na wadau wake wote na hivyo kuhakikisha inatumika kikamilifu ili kuleta msukumo wa maendeleo ya jamii nchini.

Mhe. Spika, Katika kipindi hiki, Idara imekamilisha mapitio ya Muongozo wa kufundishia Kamati za maendeleo ya jamii. Muongozo uliokuwepo ulikuwa haukidhi haja ya hali halisi na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Hivyo Idara kwa kushirikiana na wadau wengine iliufanyia marekebisho muongozo huo na

kuingiza baadhi ya mada zinazoendana na wakati uliopo kulingana na mahitaji ya Kamati za Maendeleo ili kuleta maendeleo endelevu. Miongoni mwa mada zilizoongezeka katika muongozo huo mpya ni: Sera na Mipango ya Maendeleo, Uratibu na mashirikiano, Mpango Mkakati na Masuala Mtambuka kama; UKIMWI, dawa za kulevya, afya ya uzazi na mazingira. Muongozo utaiwezesha Idara kuzijengea uwezo Kamati za Maendeleo ya Jamii kwa kuzingatia mahitaji na hali halisi na hivyo kuziwezesha kufanya kazi zake kwa umakini na ufanisi. Aidha Idara imeufanyia majaribio muongozo huo mpya ili kuuboresha zaidi. Kukamilika kwa Muongozo huo kutaiwezesha Idara kuzijengea uwezo Kamati za Maendeleo ya jamii kwa kuzingatia mahitaji na hali halisi na hivyo kuziwezesha kufanya kazi zake kwa umakini na ufanisi.

Mhe. Spika, Idara kwa kushirikiana na Shirika la Kusaidia Watoto *(Save the Children)* ilifanya uhamasishaji wa kuanzisha vikundi vya wazazi vitakavyosimamia ulinzi na malezi ya watoto katika Shehia. Uhamasishaji huo umefanywa kupitia kwa baadhi ya waratibu wa shughuli za wanawake na watoto wa Wilaya zote kumi (10) za Unguja na Pemba. Jumla ya vikundi mia moja (100) vya usimamizi wa ulinzi na malezi ya watoto vimeundwa kupitia waratibu wa Shehia mia moja (100) ambapo kila Wilaya imetoa Waratibu wa Shehia kumi (10). Vikundi hivyo kwa kuanzia vimeundwa katika Shehia zenye mabaraza ya watoto pekee. Lengo ni kuhakikisha kila Shehia inakuwa na kikundi kinachosimamia ulinzi na malezi ya watoto. Changamoto iliyopo ni kuhakikisha vikundi hivyo vinajengewa uwezo ili kumudu majukumu yao kikamilifu. Vikundi vilivyoanzishwa vina majukumu matatu (3) makuu nayo ni:-

1. Kukutana kila mwezi kujadili juu ya masuala ya watoto.
2. Kutoa taarifa kwa waratibu wa Shehia juu ya hali ya ulinzi wa watoto katika maeneo yao.
3. Kuelimisha wazazi juu ya masuala ya ulinzi na malezi bora ya watoto katika Shehia zao.

Mhe. Spika, Tarehe 15 Mei ya kila mwaka, Idara hii huadhimisha Siku ya Familia Duniani. Maadhimisho hayo yana lengo la kutathmini na kuandaa mikakati ya kuzisaidia familia kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kauli mbiu ya Kitaifa ya mwaka huu katika maadhimisho hayo ilikuwa ni *"Elimu: Msingi wa Maisha Bora ya Familia".* Maadhimisho ya mwaka huu yalifanyika kwa kuwakutanisha wadau wa familia wakiwemo viongozi wa dini, waandishi wa habari, watendaji wa Serikali na Taasisi zisizo za kiserikali ambao wanahusika na masuala ya familia. Kufuatia kikao hicho mapendekezo mbali mbali yalitolewa ili kukabiliana na changamoto zinazozikabili familia katika kujenga maadili mema ambayo ndio chimbuko la maendeleo.

Baadhi ya mapendekezo hayo ni:

1. Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto imetakiwa kuratibu na kusimamia masuala ya familia kikamilifu pamoja na kushirikiana na wadau wa masuala ya familia kuangalia kiini cha matatizo ya familia pamoja na changamoto zinazozikabili familia na kuandaa mikakati ya utekelezaji.

2. Utaratibu wa kuhakikisha kwamba wazazi wanapatiwa Stadi za maisha uandaliwe ili kuwawezesha kupata mbinu na taaluma sahihi ya jinsi ya kukabiliana na changamoto zinazozikabili familia na hivyo kujenga familia bora na imara.

3. Jamii imetakiwa kurudi katika miongozo ya dini kama ni suluhisho la changamoto nyingi zinazozikabili familia hivi sasa.

4. Wizara ya Elimu imetakiwa kuliangalia upya suala la maadili ya walimu ambao ni walezi wakubwa wa watoto. Aidha washiriki wametoa msisitizo kwa Wizara ya Elimu kutekeleza jukumu lao la kutoa taaluma ya masuala ya familia kwa wanafunzi.

5. Masuala ya familia ni muhimu kuzingatiwa katika sera, sheria, mipango, mikakati na ilani za vyama mbali mbali vya kisiasa.

6. Wakati umefika wa kuisimamia dhana ya uanzishaji wa kitengo cha kuwapatia taaluma na ushauri kwa wale wanaotaka kufunga ndoa.

MALENGO YA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, Idara hii katika mwaka 2010/2011, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuzijengea uwezo Kamati za Maendeleo ya Jamii ili ziweze kumudu vyema majukumu yake ya kuleta ustawi na maendeleo ya jamii.

2. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii ikiwa ni muongozo wa kuleta maendeleo ya jamii nchini.

3. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi mbali mbali za Kitaifa na Kimataifa katika kuleta maendeleo ya jamii.

4. Kuelimisha jamii kuhusiana na masuala mbali mbali ya maendeleo ya jamii.

Mhe. Spika, Ili Idara ya Maendeleo ya Jamii iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi milioni hamsini na tatu na laki tisa (53,900,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MFUKO WA KUJITEGEMEA

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kutoa mikopo nafuu ili kuwawezesha wananchi kiuchumi na kupunguza umasikini. Lengo ni kutilia mkazo suala zima la kupunguza umasikini kwa wananchi katika hali ya kuwajali na kuwapatia fursa ili waweze kunyanyua hali zao za maisha.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2009/2010, Idara hii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia sera, kanuni na miongozo ya utoaji na urejeshaji mikopo kwa kuzingatia ukuaji wa ajira kijinsia.

2. Kusimamia uratibu wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(JK/AK)* na kuongeza ajira kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu.

3. Kutoa mikopo yenye thamani ya TShs 120m.

4. Kutoa mafunzo ya utoaji mikopo, uendeshaji biashara, uwekaji wa kumbukumbu na kujikinga na maambukizo ya UKIMWI kwa wateja.

5. Kuwapatia wajasiriamali fursa za kushiriki katika maonyesho mbali mbali pamoja na kuadhimisha siku za Kimataifa kwa lengo la kujifunza na kuwapatia masoko ya ndani na nje.

6. Kuendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya Idara na Taasisi za ndani na nje.

7. Kuhamasisha jamii katika ubunifu na utumiaji wa rasilimali zilizopo katika maeneo yao.

8. Kuimarisha utendaji wa kazi za Idara.

Mhe. Spika, Kwa mwaka huu wa fedha, hadi mwezi Aprili Mfuko wa Kujitegemea umetoa mikopo mia moja na ishirini na moja (121) kati ya hiyo Unguja ni sabini na saba (77) na Pemba ni arobaini na nne (44) kwa wateja mia moja na arobaini na moja (141) ambapo tisini na moja (91) kutoka Unguja na hamsini (50) kutoka Pemba ikiwa wanawake ni themanini na nne (84), kwa Unguja ni sitini na tatu (63) na Pemba ni ishirini na moja (21) na wanaume

hamsini na saba (57) kati ya hao Unguja ni ishirini na nane (28) na Pemba ni ishirni na tisa (29). Mikopo hiyo ina thamani ya Shilingi milioni themanini na tatu na laki nne (83,400,000/=) ambapo Unguja zimetolewa Shilingi milioni hamsini na sita na laki nane (56.8m) na Pemba ni milioni ishirini na sita na laki sita (26.6m) sawa na asilimia sabini (70%). ***(Kiambatisho Nambari 13)***. Hadi kufikia mwezi Aprili, Idara imekusanya marejesho ya fedha za mikopo ya Shilingi milioni sitini na saba, laki mbili na arobaini na sita elfu na hamsini (67,246,050/=), kati ya fedha hizo Unguja ni milioni arobaini na tano, laki mbili na arobaini na mbili elfu na mia tatu (45,242,300/=) na Pemba ni Shilingi milioni ishirini na mbili, elfu tatu, mia saba na hamsini (22,003,750/=). (***Kiambatisho nambari 14).***

Mhe. Spika, Idara imehamasisha na kutoa ushauri wa kitaalamu na mafunzo ya utumiaji wa mikopo, uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu (mapato na matumizi) ya miradi na uzalishaji bora katika bidhaa, mbinu za ubunifu pamoja na kujikinga na maambukizi ya UKIMWI kwa wajasiriamali mia tatu na arobaini na tano (345) kati ya hao wanawake ni mia mbili na sabini na sita (276) na wanaume ni sitini na tisa (69).

Mhe. Spika, Idara kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(JK/AK),* hadi kufikia mwezi wa April, 2010 imetoa jumla ya Shilingi bilioni moja, milioni mia tatu na kumi na nne, laki sita na arobaini elfu **(1,314,640,000/=)** kwa *SACCOS* pamoja na watu binafsi kwa Unguja na Pemba. Kati ya fedha hizo Unguja zimetolewa Shilingi milioni mia tisa na kumi na mbili, laki tatu na sabini elfu **(912,370,000/=)** na Pemba zimetolewa Shilingi milioni mia nne na mbili elfu, laki mbili na sabini elfu **(402,270,000/=) (*Kiambatisho nambari 15a,15b, 15c na 15d).***

Mhe. Spika, Katika kutekeleza suala la uhamasishaji wa jamii kuwa wabunifu wa miradi kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yao na kuziongezea thamani bidhaa zao, wajasiriamali wamezalisha bidhaa za aina mbali mbali ambazo zitawaletea tija zaidi**.** Bidhaa hizo kama ndimu ambapo wajasiriamali wametengeneza siki, achari, mafuta na sabuni. Aidha wametumia difu kutengeneza vipochi, matungi ya taa na viatu. Mafuta ya nazi safi *(virgin oil)* yenye rutba na kutibu maradhi mbali mbali yametengenezwa kwa kutumia teknolojia nyepesi. Rasilimali nyingine ni dagaa ambalo limetengenezwa la kukausha, la kutia viungo na kutengeneza chakula cha kuku.

Mhe. Spika, Kwa mwaka huu, jumla ya wajasiriamali arobaini (40), wanawake thelathini na mbili (32) na wanaume wanane (8) wamepatiwa fursa ya kushiriki katika Maonyesho ya 11 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Jua Kali/Nguvu Kazi yaliyofanyika Tanzania Bara (Arusha na Dar es Salaam). Fursa hii hutolewa ili wapate kuuza bidhaa zao pamoja na kubadilishana ujuzi wa kuweza kuzalisha bidhaa zenye ubora.

Mhe. Spika, Idara kwa kushirikiana na Taasisi zisizokuwa za Kiserikali ziitwazo *"Kizoro Art Presentation"* na *"Mbamba Marketing Centre"* imewajengea uwezo wajasiriamali kwa kufichua vipaji vyao, kuboresha vifungashio vya bidhaa na mikakati ya kuandaa maonyesho madogo na makubwa nchini.

MALENGO YA IDARA YA MFUKO WA KUJITEGEMEA KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, Katika kipindi cha 2010/2011, Idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia utekelezaji wa sera, kanuni na miongozo ya utoaji na urejeshaji mikopo kwa kuzingatia ukuaji wa ajira kijinsia ili kuimarisha mifuko kuwa endelevu.

2. Kuendelea kuratibu Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(JK/AK)* kupitia mikopo yenye masharti nafuu na kuongeza ajira.

3. Kutoa mikopo yenye thamani ya shillingi milioni mia moja na ishirini (120) kwa wananchi wasiokuwa na ajira wenye uwezo wa kufanya kazi kupitia Mfuko wa Kujitegemea.

4. Kuendelea kutoa mafunzo ya upatikanaji na matumizi bora ya mikopo, ujasiriamali, ufundi stadi, uzalishaji mali na kujikinga na maambukizo ya UKIMWI kwa wateja.

5. Kuimarisha utendaji kazi wa Idara.

6. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa katika kuwanyanyua wajasiriamali nchini.

Mhe. Spika, Ili Idara ya Mfuko wa Kujitegemea iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, katika mwaka wa fedha 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya Shilingi milioni mia moja na kumi (110,000,000/=) kwa matumizi ya kawaida.

AFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Afisi kuu Pemba inasimamia shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba ambayo inajumuisha Idara zote za Wizara. Hivyo Afisi hiyo inatekeleza malengo ya Wizara iliyojipangia kwa upande wa Pemba. Utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2009/2010 na malengo ya Afisi hiyo

kwa mwaka 2010/2011 tayari yameshaelezwa katika utekelezaji wa kila Idara ambao unahusisha na Afisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, Ujenzi wa Afisi Kuu ya Wizara Pemba, unasimamiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi. Kwa kipindi kirefu, zoezi hili lilikwama kutokana na tatizo la upatikanaji wa kiwanja. Baada ya jitihada kubwa, Wizara yangu imefanikiwa kupata kiwanja katika eneo la Tibirinzi na hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kwamba kazi ya usarifu na usimamizi wa ujenzi imeshakabidhiwa kwa mtaalamu na atakapokamilisha kazi ya usarifu, shughuli za ujenzi zitaanza.

Mhe. Spika, Ili kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Afisi Kuu Pemba kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya Shilingi milioni mia moja na themanini, laki sita na arobaini elfu (180,640,000/=) kwa kazi za kawaida.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha 2009/2010, Wizara yangu ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi milioni sitini (60,000,000/=). Hadi kufikia mwezi Mei, 2010 tumeweza kukusanya mapato ya Shilingi milioni thelathini na nane, laki tatu na themanini na sita elfu, mia moja na hamsini (38,386,150/=) ambayo ni sawa na asilimia 63.9%.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu ilitengewa jumla ya Shilingi milioni mia moja na thelathini (130,000,000/=) kwa kazi za maendeleo. Fedha zilizotolewa kwa kazi hizo mpaka kufikia Mei, 2010 ni Shilingi milioni hamsini na moja (51,000,000/=) ambazo ni sawa na asilimia 39%. Aidha kwa mwaka wa fedha 2009/2010, makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida yalikuwa ni Shilingi milioni mia sita na arobaini na tano, laki tano na hamsini na sita elfu (645,556,000/=) na hadi kufikia Mei 2010, fedha zilizotolewa ni Shilingi milioni mia nne na thelathini, laki tisa na thelathini na tatu elfu na mbili (430,933,002/=) ambayo ni sawa na asilimia 67%. *(Kiambatisho Nambari 15a na 15b).*

HITIMISHO:

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuzishukuru Nchi, Mashirika ya Kimataifa na Kitaifa pamoja na taasisi mbali mbali zisizo za Kiserikali ambazo zilishirikiana na wizara yangu katika kutekeleza majukumu ya wizara katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Zanzibar. Nchi hizo ni kama ifuatavyo; Serikali ya India, Japan, Misri, Marekani, Uingereza, Jamhuri ya Watu wa China na Jamhuri ya Watu wa Iran. Taasisi za Kimataifa ni; *ILO*, *UNDP*, UNFPA, UNICEF, SAVE THE CHILDREN, UNESCO, ADB, DFID, SWISS

CONTACT, Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, na Jumuiya ya Madola.
Taasisi za Kitaifa ni *ZAYADESA, BOT, PBZ, ZANEMA, ZATUC, ZSSF, ZACA, ZAIADA, ZAWDO, ZAFELA, ZAWCO, ZAMWASO, ZANGOC, ZLSC, COWPZ, PIRO, UVIKIUTA, WEDTF, TAWLA, TAMWA, CHANGAMOTO, PRIDE, TMC, TGNP, UWT, CRDB, AKIBA BANK na POSTAL BANK.*

Mhe. Spika, Naomba kuchukuwa nafasi hii kuvishukuru vyombo vya habari ikiwemo televisheni, redio na magazeti ambavyo vimetoa mchango mkubwa katika kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya masuala mbalimbali yanayotekelezwa na wizara yangu.

Mhe. Spika, naomba kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru sana kwa dhati kabisa wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto wakiongozwa na jemedari Katibu Mkuu Rahma Mshangama, Kamishna Iddi Mapuri, Wakurugenzi Rahma Ali, Khamis, Radhiya Rashid, Moh'd maarufu Mkuu wa mwenge, Afisa Mdhamini Bi Mauwa na Maafisa wa ngazi zote na Mkurugenzi Asha Khalfani kwa kufanya kazi kwa juhudi kulikotuwezesha kutekeleza malengo yetu kwa ufanisi. Aidha, nawaomba wazidishe juhudi zaidi katika kutekeleza malengo yetu ya mwaka huu na kuwaletea maendeleo wanawake, watoto na vijana.

Mhe. Spika, Kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wapokee, wajadili, watupe ushauri na maelekezo, hatimae kupitisha makadirio na kuidhinisha jumla ya Shilingi bilioni moja na milioni themanini na sita (1,086,000,000/=) ikiwa ni fedha za kazi za kawaida na Shilingi milioni sitini (60,000,000/=) zikiwa ni fedha za kazi za Maendeleo kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha 2010/2011. Pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya Shilingi milioni hamsini na nne, laki mbili na themanini na nne elfu (54,284,000/=) kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa kupitia Baraza hili naomba kabla ya kumaliza kuwashukuru tena sana Wajumbe wa Baraza hili tukufu pamoja na watendaji wote wa Baraza. Nawaombea kwa Mungu Waheshimiwa wote watakaogombea tena nafasi ya Wawakilishi na wale watakaogombea nafasi ya Ubunge wafanikiwe, waendelee kuwa chachu ya maendeleo ya taifa hili.

Hali kadhalika nawaombea sana wele wengine ambao wameamua kuacha wenyewe kugombea au wengine ambao demokrasia imewaweka kando kwamba huo sio mwisho. Naompongeza sana maalim Mula kwa kuachia ngazi yeye mwenyewe, nawaombea kila la kheri kwa dhati na nasema nathamini sana mashirikiano mazuri tuliyokuwa nayo baina yetu katika kipindi nilichohudumu humu Barazani nasema ahsante sana.

Mhe. Spika, Naomba kutoa hoja. Ahsanteni.

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Mwenyekiti Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):

UTANGULIZI

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kutoa hotuba ya Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto kwa Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, sifa njema zote zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo hii kwenye Baraza lako Tukufu kwa madhumuni ya kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, nitakuwa mtovu wa shukurani ikiwa sitakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya Mwanzo kabisa, baada ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, naomba nichukuwe fursa hii maalum kuwapongeza wajumbe wenzangu wote kwa kushirikiana vyema katika kazi zetu mbali mbali ambazo tulipata mashirikiano mazuri katika Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na watoto Unguja na Pemba bila ya matatizo.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa mara nyengine tena kutetea kiti hicho.

Mhe. Spika, kuchaguliwa kwake kunadhihirisha wazi kuwa bado Wananchi wa Tanzania wana imani nae kutokana na kipaji na upeo wake mkubwa alionao katika kuwatumikia Watanzania.

Mhe. Spika, aidha, natoa pongezi za dhati kwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzíbar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu. Uteuzi huo unaonesha ni jinsi gani anavyokubalika kuwatumikia Wazanzibari, na ukomavu wa kisiasa ndani ya Chama cha Mapinduzi.

Aidha, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inampongeza sana Dr. Bilal kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu 2010. Hii inaudhihirishia umma wa Watanzania kuwa, wanakaribia kupata kiongozi mahiri ambae atashirikiana bega kwa bega na Rais wake katika jitihada za kupambana na umasikini na kuleta maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, tunawapongeza wale wote waliogombea nafasi ya Urais wa Zanzíbar kwa tiketi ya C.C.M kwa ujasiri wao mkubwa wa kuyakubali matokeo na kuahidi kuwaunga mkono wale wote walioteuliwa kugombea nafasi za uongozi ndani ya chama chao. Hichi ni kielelezo tosha cha kukua kwa demokrasia ndani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, wakati wa kuichambua na kuipitia Bajeti ya Wizara hii, nathubutu kusema kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu walifanya uchambuzi wa kina kwa Idara moja moja zilizo chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na hatimaye kuikubali. Naomba niwatambulishe kwa majina Wajumbe hao ili kuweka vyema kumbukumbu katika hansard yetu:

Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Mwenyekiti
Mhe. Ame Mati Wadi	-	M/Mwenyekiti
Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-	Mjumbe
Mhe. Ali Hají Ali	-	Mjumbe
Mhe. Ali Mzee Ali	-	Mjumbe
Mhe. Haji Faki Shaalí	-	Mjumbe
Mhe. Hasnuu Moh'd Hají	-	Mjumbe
Mhe. Moh'd Ali Salim	-	Mjumbe
Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak	-	Mjumbe
Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
Ndg. Salmin Amour Abdalla	-	Katibu
Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu

Mhe. Spika, Idara ya Mipango na Sera katika mwaka wa fedha 2009/2010, imefanikiwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watendaji 31 ndani na nje ya nchi. Kati yao wanawake 21 na wanaume 10.

Mhe. Spika hii ni faraja Kubwa kwetu kwani wizara inazidi kutuonesha kwamba ina nia safi ya kutekeleza mikataba na maazimio mbalimbali ya Kimataifa inayolinda haki za wanawake. Hii ni kutokana na kuwa imesomesha idadi kubwa ya wanawake ikilinganishwa na wanaume. Kwa kweli hii ni hatua muhimu ambayo itasaidia kuhakikisha kuwa wanawake wanapata nafasi sawa

na wanaume bila ya ubaguzi katika kuwakilisha serikali yao katika ngazi za Kitaifa na Kimaifa.

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) na wadau mbalimbali, wizara inaendelea na mradi wa jinsia Zanzíbar. Pamoja na mambo mengine, mradi huu una lengo la kuzijengea uwezo taasisi mbalimbali kupambana na udhalilishaji wa kijinsia.

Mradi huu kwa mashirikiano makubwa na Idara ya Wanawake na Watoto ulisimamia maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani na kuendesha kongamano na maigizo ambayo yaliwashirikisha wananchi mbalimbali. Hatua hii inalenga kuwajuulisha Wanawake wa Zanzíbar juu ya hali ya maendeleo ambayo Wanawake wa sehemu nyengine Duniani wamefikia na kuwahamasisha kuwa imara katika kutekeleza majukumu yao na kutatua matatizo yao kwa kutumia mbinu mbalimbali.

Kongamano lililowashirikisha mafiasa wa serikali, masheha na wajasiri amali wanawake lilifanywa kwa ajili ya kutafakari michango ya wanawake katika maendeleo ya jamii.

Mhe. Spika, kwa kushirikiana bega kwa bega kati ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na watoto, Wizara ya Fedha na Uchumi, na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii chini ya mradi wa jinsia Zanzíbar, tathmini ya upangaji na utumiaji wa rasilimali kwa mtazamo wa kijinsia ilifanywa. Tathmini hiyo ambayo itaonesha idadi ya wanawake wanaohitajika katika kada mbalimbali na kulinganishwa na idadi halisi ya Wanawake waliomo kwenye kada hizo, itasaidia kuimarisha huduma za afya ya uzazi na elimu ya juu kwa upande wa wanawake.

Mhe. Spika, waathirika wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia walipatiwa ushauri nasaha kupitia vituo 13 vya ushauri nasaha vya Wizara ya Kazi, vituo 6 vya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, vituo 3 vya mahakama, vituo 5 vya Polisi na vituo 4 vya asasi zisizo za kiserikali.

Hata hivyo, kamati inaiomba wizara ichukuwe hatua kali kwa yeyote atakaekwamisha ushahidi katika kesi hizo, ili iwe funzo kwa watu wengine wenye nia kama hiyo, kwani kumejitokeza wimbi kubwa la kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto ambazo huishia njiani kwa kisingizio cha kukosekana ushahidi wa kutosha.

Zaidi ya hayo, naiomba Serikali ya Mapinduzi Zanzíbar kuharakisha mipango ya ununuzi wa mashine ya kuchunguzia viasili (DNA) ili kupata ithibati kwa wale wanaokiuka maadili kwa kuwapa ujauzito watoto wetu na hatimaye sheria ichukuwe mkondo wake.

Mhe. Spika, wizara imeendelea na programu ya kuijijengea uwezo kwa kuongeza ajira kwa vijana, kuweka mfumo imara wa hifadhi ya jamii, kutoa mafunzo kwa wajasiriamali mbalimbali na kujenga uwezo kwa taasisi za serikali na zile za watu binafsi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 47 wa Hotuba ya Mhe. Waziri tumeelezwa kuwa rasimu ya kwanza ya Sheria ya Mtoto imetayarishwa na kujadiliwa na Wadau mbalimbali ili watowe maoni na michango yao kwa lengo la kuimarisha zaidi.

Kwa kuwa Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto inatarajia kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kumalizia utayarishaji wa Sheria ya mtoto, kama inavyothibitika katika ukurasa wa 49 wa Hotuba ya Mhe. Waziri, Kamati yetu inaiomba Wizara kuwa makini zaidi na utayarishaji wa rasimu hiyo ya Sheria kwani baadhi ya mambo yaliyopendekezwa ndani ya rasimu hiyo ya sheria ya mtoto yanakwenda kinyume na maadili yetu.

Kamati yetu inashauri hili kwa kuwa sheria yeyote inayotungwa nchini inatakiwa pamoja na mambo mengine kuangalia pia mila, utamaduni, silka na maadili ya jamii.

Mhe. Spika, Uwiano na Muendelezo (C*omposition and Development)* ni moja wapo ya kipengele muhimu katika mchakato wa uandishi wa sheria ambacho mwandishi hutakiwa kuzingatia. Hichi ni kipengele cha tano katika hatua za uandishi wa sheria.
Kwa kutambua kuwa Rasimu ya awali ni kianzio tu cha jambo linalotakiwa kufanywa na hutoa nafasi kwa washirika wa Maendeleo na Wadau wengine kuipitia rasimu hiyo na kutoa maelekezo yao kwa nia ya kuimarisha zaidi. Kutokana na maelezo yangu haya, Kamati yetu inawaomba wahusika wa rasimu hiyo kuyafikiria na kuyachukulia hatua mapendekezo yote yaliyotolewa na Wadau ili Sheria ya Mtoto iweze kutekelezwa kama ilivyokusudiwa. Hii ni kutokana na kuwa, mwandishi wa sheria anatakiwa kuwa tayari wakati wowote kutolewa makosa ili kazi yake iwe bora zaidi.

Mhe. Spika, Mtaalamu aliyeajiriwa na wizara alishiriki vilivyo kwenye harakati za utayarishaji wa mpango wa Pili wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini Zanzíbar (MKUZA) ili kusisitiza uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika mpango huu. Kwa kupitia mradi wa jinsia, wizara ilisimamia maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani.

Mhe. Spika, wizara kwa kupitia Kamisheni ya Kazi imeandaa jumla ya vipindi 21 ambavyo vimerushwa hewani kupitia Sauti ya Tanzani Zanzíbar kwa ajili ya kuelimisha jamii jinsi ya kupambana na ajira za watoto. Vipindi hivyo

vimetayarishwa ili kuwanusuru watoto wetu na ajira mbaya ambazo zinaweza kuwasababishia ulemavu na kuwakosesha fursa ya kuendelea vyema na masomo.

Mhe. Spika, kwa kupitia programu ya kuijengea uwezo wizara, ujenzi wa kituo cha kutoa taarifa kwa waomba kazi umekamilika na vifaa vinavyohitajika vimenunuliwa. Kituo hicho kitawawezesha vijana nchini kufahamu nafasi za kazi za ndani na nje ya nchi ili waweze kuzitumia kwa mujibu wa fani zao.

Zaidi ya hayo, kanuni za sheria ya ajira na sheria ya uhusiano kazini zimekamilika na hivyo ni rahisi kwa sasa kutekeleza sheria hizo.

Mhe. Spika, watoto 400 kutoka katika shehia mbalimbali za Unguja na Pemba waliokolewa kutoka katika mazingira magumu ya ajira kwa watoto na kurejeshwa skuli. Kamisheni ya kazi, kwa kushirikiana na shirika la Kazi duniani imetoa vifaa vya skuli kwa watoto hao.

Hii ni hatua muhimu kwa maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla kwani kuelimika kwa watoto wetu ni Mwanzo mzuri wa kujenga mustakabali mwema wa maisha yao.

Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na shirika la Kazi duniani (ILO) imekamilisha utafiti wa mfumo wa hifadhi ya Jamii kwa wote. Harakati za kuandaa sera ya hifadhi ya jamii Zanzíbar zinaendelea, mbapo pamoja na mambo mengine itasaidia kuweka mfumo mzuri wa hifadhi ya jamii kwa wananchi waliostaafu hapa Zanzíbar kwa nia ya kuwawezesha waishi vyema kwa kujikimu ipasavyo wao na familia zao.

Utafiti wa hali za taasisi mbalimbali za kazi umefanywa na rasimu ya awali ya ripoti ya utafiti huo imekamilika. Aidha, Kamati ya usimamizi wa mradi wa kutekeleza sheria za kazi imeundwa rasmi ili kusimamia mradi huo.

Mhe. Spika, Idara ya mfuko wa kujitegemea imefanikiwa kutoa mikopo 121 kwa wateja 141, ikiwa ni wanawake 84 na wanaume 57, yenye thamani ya shilingi za Kitanzania 83,400,000/= Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametueleza kwamba Idara ya Maendeleo ya Vijana inatarajia kuendeleza na kuimarisha vikundi vya uzalishaji mali vya vijana kwa kuwapatia mafunzo ya uanzishaji na uendelezaji wa SACCOS. Mhe. Spika, Kamati yetu inaunga mkono wazo hilo hasa tukizingatia kuwa uanzishaji wa vikundi hivyo hutoa ajira kwa wananchi, jambo ambalo litasaidia kuwatoa kwenye janga la umasikini.

Aidha, uanzishwaji wa vikundi hivyo utasaidia kupunguza idadi ya vijana wazururaji na hata wale wanaojihusisha vikundi viovu na utumiaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, pamoja na uungaji mkono huu, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaishauri Wizara kuwa karibú na Idara ya Maendeleo ya Vijana Ambayo ndiyo hasa yenye mamlaka ya kisheria ya kushughulikia vikundi vya ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS) kwa upande wa Zanzíbar kwa mujibu wa sheria Namba 4/1986.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, Kamati yetu inatoa tahadhari kwa wananchi kwamba waitumie mikopo inayolewa kwa ajili ya uzalishaji zaidi ili kufikiwa lengo lililokusudiwa.

Mhe. Spika, jumla ya wajasiriamali 40 wamepatiwa fursa ya kushiriki katika maonyesho mbalimbali yakiwemo yale ya 11 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya jua kali/Nguvu kazi pamoja na kuadhimisha siku za kimataifa kwa lengo la kujifunza zaidi na kuwapatia masoko ya ndani na nje ya nchi.

Aidha, vijana kumi walipata fursa ya kushiriki katika kambi kazi katika nchi mbalimbali duniani, kwa kupitia Idara ya Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Sambamba na hayo, mfuko wa kujitegemea umeweza kutoa mafunzo kwa vijana 345 juu ya utumiaji sahihi wa mikopo, uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu ya miradi, uzalishaji bora wa bidhaa na kujikinga na maambukizi ya UKUMWI.

Mhe. Spika, Wizara ya Kazi itaendelea kuhamasisha jamii katika ubunifu na utumiaji wa rasilimali zilizopo katika maeneo yao. Bidhaa mbalimbali zimetengenezwa kwa rasilimali za hapa hapa nyumbani. Kwa mfano: difu la mnazi kutengenezwa vipochi, viatu na matungi ya taa, ndimu kutengenezwa siki, achari, sabuni na mafuta. Rasilimali ya dagaa hukaushwa na kutengenezwa chakula cha kuku.

Mhe. Spika, Kamisheni ya kazi imeimarisha kitengo cha ajira ili kuhakikisha kwamba ajira zinaelekezwa kwa wenyeji ambao ndio walengwa wakuu wa sekta ya uwekezaji hapa nchini.

Mafunzo ya utatuzi wa migogoro ya kazi yaliyowajumuisha mafiasa 20 yalifanyika kupitia Idara hii. Pia wizara ilipokea baadhi ya vitabu muhimu vya masuala ya usalama na afya kazini. Mafunzo haya yatapelekea kujenga

nidhamu nzuri ya kazi na kusuluhisha matatizo madogo madogo yanayotokea kazini na hatimaye kuleta maendeleo endelevu.

Mhe. Spika, wizara pia kupitia Kamisheni ya kazi imeendeleza ushirikiano baina yake na taasisi mbalimbali duniani. Kwa kushirikiana na shirika la kazi duniani (ILO), Kamisheni inaendelea na utafiti ili kutoa taarifa rasmi kuhusiana na mapendekezo ya kima cha chini cha mshahara hapa Zanzíbar.

Mhe. Spika, baada ya maoni hayo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, niwaombe sasa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na kuipitisha bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kutoka katika mfuko mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yenye jumla ya shilingi 1,146,000,000/= . Shilingi 1,086,000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 60,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kabla sijawasilisha naomba niseme maneno machache tu, kwa kuwa mimi na wananchi wangu ambao wanajiajiri katika sehemu mbali mbali za nchi yetu na nje ya nchi.

Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa miaka miwili na nusu nimefanya kazi katika Wizara ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Lakini katika harakati zetu zote tulizokwenda kila mwaka hatua zinazidi kuendelea mbele.

Ombili langu kwa serikali naomba bado Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Wanawake serikali iwafikirie nyongeza ya bajeti yao. Tukitaka tusitake hii Wizara inagusa nyanja mbali mbali, hasa tukizingatia akina mama, vijana wetu, na hata wanaume watu wazima wanahitaji kupata mikopo mbali mbali midogo midogo ya kuwasaidia juu ya maisha yao. Kwa hivyo naiyomba sana serikali hili liliangalie ili wapewe uwezo zaidi wa kufanya kazi zao kwa ufasaha zaidi.

Mhe. Spika, jengine nitamuomba sana Mhe. Waziri akija hapa hii ninaisema mimi mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la kwahani kwa sababu vijana hawa nitakaowasemea wamo katika Jimbo langu la Kwahani. Katika nchi yetu ya Zanzibar Unguja na Pemba kuna mtiririko mkubwa sana wa vijana wetu wanaokwenda Arabuni kutafuta kazi, hasa vijana wetu wa kike.

Katika taarifa yetu hii ya Waziri nimesema kwamba sasa hivi kuna mfumo mzuri umepangwa juu ya kupata kazi nje na ndani ya nchi. Nataka Mhe. Waziri angalau aje atupe maelekezo, hawa vijana wetu ambao wanachukuliwa hapa kiudalali wanadanganywa hapa kwamba wende Arabuni kuna kazi wakifika kule wanasumbuliwa. Taarifa tunazozipokea kwamba kuna vijana wetu wameondoka hapa kwa hadaa baada ya kufika kule wanateswa na wana madhila makubwa sana, wanatafuta njia za kurudi kwao hawazipati. Naiyomba

serikali kwa moyo safi kabisa ifanye kila uwezo iwasiliane na Balozi wetu waliyekuwepo katika nchi za Kiarabu kama Abudhabi, Maskat na kwengineko, watafute vijana wetu hawa wafanyiwe utaratibu wa kurudishwa kwao. Mimi nina watu wanafika kumi wanadai tuwasaidie kwa hali na mali ili warudi kwao kwani hakuna kazi kuna madhila. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri vijana wetu wameondoka hapa kwa kudanganywa lakini walipofika kule wameingia katika shimo ambalo hawalijui.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, na kwa niaba ya wananchi wangu wote wa Jimbo la Kwahani naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na naomba kuwasilisha.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman (Waziri Kivuli wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu kwa kutufikisha hapa leo kwenye majadiliano ya mwisho ya bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa awamu ya uchaguzi wa 2005-2010.

Mhe. Spika, namaliza kipindi hiki kabla ya uchaguzi mkuu wa 2010 kwa kukushukuru wewe binafsi Mhe. Waziri wa wizara hii na watendaji wote pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili kwa mashirikiano makubwa tuliyokuwa nayo wakati wa kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi.

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kuwa wengi wa wajumbe wako ukiwemo wewe mwenyewe watapata ridhaa za vyama vyao kuendelea kuwatumikia wananchi ndani ya mabadiliko makubwa ya kiutawala na kisiasa katika nchi pamoja na mabadiliko makubwa ya kibiashara, kiuchumi katika kanda ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, ni imani yangu pia kuwa wale ambao hawatarudi tena katika Baraza lako tukufu baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2010 basi itakuwa ni nafasi adhimu ya kuombana radhi kwa mabaya machache yaliyosababisha tukihiriane. Pia ni fursa nyengine ya kujipongeza kwa mema mengi tuliyoyafanya kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Zanzibar na taifa letu.

Mhe. Spika, hapana shaka wananchi watatukumbuka kwa mambo mengi ikiwemo kuanzisha na kupitisha kwa sauti moja ya Baraza na bila ya kujali itikadi zetu hoja ya kuwa na uhuru wa kutafuta na kutumia rasilimali ya mafuta. Pamoja na hoja ya kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa madhumuni ya hatma njema ya kiuchumi na kisiasa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hivi karibuni katika Jimbo la Koani Wilaya ya Kati palitokea ajali mbaya ya gari iliyopoteza maisha ya watu wakiwemo wanawake na watoto. Nachukua nafasi hii kwa niaba ya wanawake wenzangu popote walipo nchini kutoa mkono wa pole kwa wafiwa na kuwaomba wawe na subra kwa misiba hiyo mizito. Nawaombea malazi mazuri kaburini na maisha mema ya akhera marehemu wote waliotangulia. Pia nitoe mkono wangu wa pole kwa waheshimiwa wenzangu ambao wamefikwa na msiba humu katika hili Baraza kama Mhe. Muhiddin Moh'd Muhiddin na Mhe. Dadi Faki Dadi kwa kufiwa na wapenzi wao Mwenyezi Mungu atawapa subra.

Mhe. Spika, pia nawashukuru wanawake wote wa Tanzania na zaidi Zanzibar na hasa wale wa Chama cha Wananchi CUF chini ya Mwenyekiti Professa Ibrahim Lipumba na Katibu Mkuu Maalim Seif Sharif Hamad walioamua kunileta katika Baraza hili kuwawakilisha wanawake wa Wilaya ya Mjini kwa kipindi cha mwaka 2005-2010. Nawashukuru kwa mashirikiano yao makubwa wakati huu wa utekelezaji wa majukumu haya mazito.

Mhe. Spika, sitowamaliza mmoja mmoja lakini nazidi kukushukuru wewe binafsi tena kwa kuliongoza Baraza hili kwa hekima, busara na uadilifu mkubwa uliopelekea kupitisha mambo mazito na muhimu kwa maslahi ya nchi yetu. Nachukua nafasi hii pia kumshukuru kiongozi wangu wa upinzani Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa kutuongoza na kutusaidia tutekeleze majukumu aliyotupangia, tumuombe Mwenyezi Mungu atuzidishie imani na umoja ili tushirikiane kujenga mustakabal mpya wa nchi yetu.

Mhe Spika, mwisho ingawa si kwa umuhimu, nawashuku na kuwapongeza kwa dhati ya moyo wangu, viongozi wetu wa vyama vya siasa, Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharrif Hamad na Makamo Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, ambaye pia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Amani Abeid Amaan Karume kwa ujasiri wao wa kisiasa na wingi wa uzalendo wa nchi yetu kwa kufanya mazungumzo ya pamoja yaliyozaa maafikiano.

Mhe Spika, maafikiano ya kisiasa yanahitajika ili kujenga na kuimarisha utawala bora katika Serikali na umoja wa kweli kati ya visiwa vya Unguja na Pemba. Ukosefu wa umoja na kudorora kwa utawala bora na kuvunjika kwa misingi ya Haki za Binadamu ni jumla ya hasara za kisiasa zinazokwaza maendeleo ya nchi yoyote duniani. Nina imani kuwa kwa kila Mzanzibari anaeipendelea mema nchi yetu atawaunga mkono viongozi wetu wakuu katika jitihada hizi muhimu za kuleta umoja wa kweli na endelevu.

Ajira na Soko la Pamoja la Afrika Mashariki

Mhe Spika, kimsingi wizara hii inafanya uratibu wa ajira nchini na walengwa wakuu ni vijana na wanawake na huku ikisimamia pia uratibu wa ukuzaji na

uendelezaji wa mtoto. Hili ni jukumu muhimu kwa kuwa ajira si tu ni matokeo katika mchakato wa maendeleo bali ni moja ya malengo muhimu ya kiuchumi na maendeleo. Mhe Spika, bajeti hii inakuja wakatiTanzania inaingia katika Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki huku nguvukazi ikichukuliwa kuwa kama moja ya huduma muhimu ambayo malipo yake yataongozwa na nguvu za soko.

Mhe Spika, kwa umuhimu wa matarajio ya soko jipya la ajira katika Jumuiya, sote tulitarajia kuwa Mhe Waziri angechukuwa fursa ya kutueleza chochote kuhusu matumaini ya manufaa ya soko kwa kuzingatia ishara na vigezo vya maendeleo ya nguvu kazi katika nchi yetu hasa ikilinganishwa na wenzetu katika jumuiya.

Mhe Spika, umadhubuti wa viashiria vya maendeleo ya nguvu kazi ni faraja ya neema za soko huria na udhaifu wa viashiria ni changamoto ya kukabiliana na ushindani mpya wa soko hilo. Suala tunalomuuliza Mhe Waziri, ni je, Zanzibar kama uchumi unaojitegemea lakini usio na mamlaka ya sera inatarajia nini katika Soko la Pamoja ambalo linajumuisha pia ajira?

Mhe Spika, wakati tukimsubiri Mhe Waziri alitolee ufafanuzi suala hili, kuna kilio kikubwa cha Wazanzibari kuhusiana na soko jipya la kikanda ambalo linagusa moja kwa moja masuala ya ajira. Mhe Spika, tunaelewa kuwa kuna mageuzi makubwa yanatokea Tanzania lakini kadiri mchakato unapozidi kasi hofu ya Wazanzibari ipo pale pale kuwa mafanikio ya umoja pia ni ishara ya kumalizwa Zanzibar kiuchumi na hatimae kisiasa.

Mhe Spika, umoja wa kikanda umetutoa katika fursa ya kuwa washiriki wa kudumu inayotoa nguvu za mazungumzo na uwezo wa maamuzi katika mambo yanayohusu maendeleo yetu. Uwezo wa kusimamia maendeleo ya Zanzibar uko katika Katiba ya Zanzibar, na wakati wajibu wa utekelezaji uko katika Serikali, wajibu wa usimamizi uko katika Baraza la Wawakilishi. Kama angalau Serikali ya SMZ ingefahamu kinachoendelea katika mabadiliko haya makubwa naamini na hata sisi wasimamizi wa Serikali tungefahamu kinachoendelea.

Mhe Spika, tunaelewa kuwa masula ya Mambo ya Nje ni ya Muungano lakini mkikubali kuwa na jumuiya maana yake sasa nchi zilizomo ndani ya Jumuiya hiyo si za nje tena kwa nchi nyengine, na kwa maana hiyo, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Tanzania yenyewe si nchi za nje tena kwa Zanzibar. Kwa maana hiyo kushirikishwa katika jumuiya kwa niaba yetu ni dharau kwa wananchi na kebehi ya uhuru wao.

Mhe Spika, mabadiliko ya Sera za Nje Tanzania yaliziondowa nchi zetu kwenye diplomasia ya siasa iliyohitajika kwa ajili ya ukombozi wa Afrika na

kuziingiza kwenye diplomasia ya uchumi inayohitaji mashirikiano kati ya chumi zetu na nyengine duniani. Hivyo, woga wa kisiasa kwa Zanzibar kupewa aina yoyote ya uwanachama wa kushiriki na kuchangia maamuzi katika umoja wa kikanda inatoka wapi.

Mhe Spika, kwa mantiki hiyo, kwa sasa suala la jumuiya ni suala la Mashirikiano kuliko la nje na kwa kweli inasikitisha kuwa hata sisi katika Baraza hili tunaoisimamia Serikali hatuna hata fursa ya kushauriwa na wala hata ya kuarifiwa rasmi juu ya mabadiliko makubwa yanayoendelea katika nchi na kanda. Mhe Spika, iwapo Serikali inaridhika kwa kusemewa kila kitu katika vikao vya jumuiya basi sisi wawakilishi wa wananchi haturidhiki kwani tunavyo amini hii ni Jumuiya ya Watu wa Afrika Mashariki na siyo ya Serikali za Afrika Mashariki.

Mhe Spika, nchi zikiamua kuwa na Soko la Pamoja maana yake sasa kila nchi ina kasimu uwezo na maamuzi yake ya kisera, mikakati na mipango ya maendeleo kuwa ya pamoja. Ajira kama sehemu muhimu ya maendeleo huzingatia uwezo na ujuzi wa nguvukazi pamoja na teknologia ya taarifa za kupatikana ajira. Mhe Spika soko la ajira linajumuisha Taasisi na Vyombo vya Jumuiya yenyewe na vile vile kwenye Sekta Binafsi ambayo sasa iko huru kueneza shughuli zake popote katika jumuiya.

Mhe Spika, Zanzibar tuna bahati mbaya katika umoja kwani Muungano wetu wa Tanzania unatosha kutoa funzo kwa yanayokuja. Wazanzibari bado tunauguza ‘vidonda ndugu’ kutokana na athari ya kupoteza ajira katika Taasisi za Muungano pamoja na Jumuiya na Taasisi za Kimataifa ambazo zote makao makuu yao yako upande mmoja wa Muungano; licha ya kwamba hata zile ambazo zinafungua matawi yake Zanzibar basi zinaingia kwa mwendo na mjo wa konokono. Nikisema hivyo kwa mjo wa konokono maana yake zinakuja kidogo kidogo lakini pia hazipo. Kwa mfano, *BoT* na benki nyengine wao wanakuja hapa na wafanyakazi wao sawa sawa na konokono aliyebeba mzigo wake mgongoni.

Mhe Spika, kwa muktadha na mnasaba huu, ni dhahiri kuwa katika muundo mpya wa kiuchumi na baadae kisiasa, Zanzibar kama nchi yenye kuhudumia uchumi wake haina kamwe nafasi ya kupumua; na hivyo itamalizika na hatimae itapotea. Mhe Spika, athari mbaya ya umoja uliokosa misingi ya ushirikishaji ni kwamba leo tunalazimika kwenda kupiga magoti kwa wabia wenzetu wa Muungano kuomba huruma zao zisaidie uchumi wetu.

Mhe Spika, iwapo imepita miaka 45 ya Uhuru tumeshindwa kulirekebisha hili, basi leo na kuendelea, tutalazimika kwenda kwao, tena kila mara kuwaomba na wao waende Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda ili wakubaliane kutuhurumia

tusaidie watu wetu. Mhe Spika, Zanzibar inaelekezwa wapi! Bado tuna mushkeli kuwa maana ya uhuru ni pamoja na kuwa na maamuzi.

Mhe Spika, kinadharia baada ya Soko la Pamoja kuundwa ajira hutawaliwa na nguvu za soko kwa sekta za umma na ile ya kibinafsi na kwa hivyo mwananchi ana haki ya kuajiriwa popote katika Jumuiya isipokuwa kwa ajira chache za kiusalama wa nchi husika. Aidha, masaa ya kazi, maslahi ya kazi kama likizo ya mwaka na ile ya uja uzito huamuliwa na jumuiya na huwa sawa kwa nchi zote ili kuifanya nguvu ya soko ifanye kazi kwa kutoa fursa sawa katika jumuiya. Mhe Spika, nalizungumzia Soko la Pamoja kwa kuwa sasa hili ndilo eneo muhimu la kazi kwa Afrika Mashariki.

Mhe Spika, katika mpango mkakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2006/10 unaonesha kuwa Jumuiya ina Taasisi 5 na kati ya hizo, taasisi mbili zinahusu uendelelezaji wa Mto Victoria. Zilizobakia ni pamoja na Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki, Wakala wa Usimamiaji wa Usalama wa Anga na Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki. Katika haya sikioni kinacho nasibika moja kwa moja na mikakati ya uchumi wa Zanzibar ingawa nchi 3 waanzilishi wanayo miradi 2 katika ziwa linalowaunganisha.

Nilifikiria kama Zanzibar ingekuwa na nafasi ya kushiriki ingesema angalau taasisi moja pia iwe ya uvuvi wa mwambao na wa bahari kuu ambao ungewanufaisha pia watu wa mwambao wa bahari ya Hindi badala ya Ziwa peke yake hasa ukizingatia hii ndio sehemu kubwa ya ajira ya vijana. Mhe Spika, nayasema tena haya, kwa kuwa humu ndimo mwenye raslimali yetu na ndimo mwenye fursa za kupata ajira kwa watu wetu. Wanaotuwakilisha hawakutusaidia isipokuwa kwa miradi ambayo kwa kawaida si taasisi za kudumu zinazohakikisha ajira endelevu.

Mhe Spika, pamoja na taasisi 5 nilizozitaja, vile vile Jumuiya inayo vyombo 7 vya kudumu katika muundo wake ambavyo ni Mkutano wa Marais wahusika (*The Summit*), Baraza la Mawaziri (*Council of Ministers*), Kamati za Uratibu (*Co-ordination Committees*), Kamati za Kisekta (*Sectoral Committees*), Mahkama ya Afrika Mashariki (*EACJ*), Bunge la Afrika Mashariki (*EALA*) na Secretariate ya Jumuiya. Mhe Spika katika vyombo hivi muna ajira na naamini Wazanzibari hawana ajira katika taasisi na vyombo hivi ambavyo pamoja na kuhitaji uwezo lakini ili kuzipata, pia kunahitajika busara za viongozi wa nchi husika. Je, ni kweli kuwa huruma na busara za wenzetu zinasaidia uchumi wetu?

Mhe Spika, katika Afrika ya Mashariki iliyovunjika, Zanzibar ilipewa heshima ya kuwa na Taasisi ya Utafiti wa Viumbe vya Baharini katika kutambuwa umuhimu wa bahari na visiwa vyetu. Inasikitisha kuwa kila demokrasia na ushirikiano vinapozidi katika Bara letu athari yake mbaya ni kuipoteza

Zanzibar fursa za kujiamulia mambo yake ya kiuchumi. Mhe Spika, kwa mabadiliko haya ya kikanda, ilivyokuwa Zanzibar haina nafasi ya kuzungumza na kushiriki maamuzi, watakaonufaika ni wachache wanaoalikwa vikao na watakaoumia ni Wazanzibari wengi. Iwapo uratibu wa kazi hautazingatia haya itakuwa ni hasara kubwa kwa Wazanzibari.

Hali ya Ajira Zanzibar

Mhe Spika, kwa mujibu wa takwimu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA), sehemu kubwa ya ajira ya wananchi wa Zanzibar iko katika kilimo. Karibu asilimia 40 ya Wazanzibari wanategemea ajira zao katika kilimo, kati yao asilimia 60 ni wanawake. Vile vile, Serikali inatoa ajira kwa asilimia 15 ya nguvu kazi kati yao asilimia 4 tu ni wanawake. Zaidi, huku kauli mbiu ya nchi ikisisitiza kuwa sekta binafsi ndio muhimili wa uchumi, ajira katika sekta hii ni asilimia 12 na wanawake wanapata chini ya asilimia 2 ya ajira katika sekta binafsi.

Mhe Spika, hali hii ya ajira katika nchi inaonesha kuwa bado Sekta Binafsi inayotegemewa kuinuwa uchumi ni dhaifu hapa Zanzibar licha ya kwamba ushiriki wa wanawake katika ajira hii ndogo hauna maana kubwa kiuchumi. Hali hii inajitokeza wakati tuko peke yetu kama Zanzibar na mpango mkakati wa soko la pamoja ni kuifanya ajira kuwa huru hasa katika sekta binafsi. Hii ni kusema hata hii ajira ndogo tuliyonayo leo, basi fursa ziko wazi kwa kila mwananchi wa Afrika Mashariki mwenye uwezo kunufaika nayo.

Mhe Spika, kwa maelezo hayo inaonesha kuwa iwapo sekta binafsi haitoongeza mchango katika umiliki wa harakati za kiuchumi katika uzalishaji na huduma wakati huu wa majio ya soko la pamoja, basi ni dhahiri kuwa hatutanufaika vyema kiuchumi, kijamii na hivyo kiajira wakati soko hilo litakapo pambamoto. Serikali inayo wajibu mkubwa wa kurekebisha sheria na taratibu zinazokatisha tamaa sekta binafsi katika utekelezaji wa malengo yake. Bila shaka, sekta ya kifedha ambayo haijasaidia ipasavyo sekta binafsi hasa biashara na kilimo, inahitaji kuongeza mchango wake kuinua uchumi wa kisekta.

Mhe Spika, naishauri Serikali iihamasishe na iisaidie sekta binafsi ili iongeze kasi katika utoaji wa huduma za usafiri wa baharini na angani kwa kuongeza wingi na ukubwa wa vyombo ili tuwe kiongozi katika soko hili la huduma katika soko la pamoja. Aidha, kwa upande wa ajira ya kilimo ambapo washiriki wengi ni wanawake, tunazidi kuishauri Serikali kusimamia kwa vitendo kauli mbiu ya ‘Kilimo Kwanza’ kwa kuongeza matumizi katika technologia ya kisasa pamoja na ya pembejeo za kilimo ili kuongeza uzalishaji na maslahi ya nguvu kazi.

Maslahi ya Kazi

Mhe Spika, maslahi ya kazi ambayo ni pamoja na mshahara wa mwezi unaokabiliana na upandaji bei kwa bidhaa na huduma, viinua mgongo na mafao pamoja na malipo ya uzeeni yako kiwango cha chini hapa Zanzibar na kila siku wajumbe wako tunalizungumzia. Hali hii inaathiri ufanisi wa kazi. Mara nyingi kwa hapa kwetu maslahi ya kazi yanaathiriwa na ukubwa wa ajira ya Serikali pamoja na baadhi ya mashirika ya Serikali.

Mhe Spika, kwa mfano, Serikali inatumia fedha nyingi katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ na kwa hivyo maendeleo ya Serikali za Mitaa yamedhoofika kutokana na kasma kubwa ya matumizi inayokwenda kwenye Vikosi vya Serikali. Mhe Spika, kwa umuhimu wa Serikali za Mitaa katika utoaji wa huduma kwa jamii, Serikali hizo zinahitaji kuwa na wizara yake pekee ili kuziongezea hadhi na kujiamini mbele ya jamii. Hili litasaidia katika kupanga ajira yake bila ya kuingiliwa na Serikali Kuu kama ilivyo sasa**.**

Mhe Spika, malipo ya masaa ya ziada ya kazi yamepotea katika mipango ya uchumi Zanzibar na vile vile malipo ya likizo ni kitu kilichosahaulika. Ndani ya soko la pamoja mambo haya husawazishwa kwa kuwa na sera ya aina moja kwa nchi wanachama. Ipo haja kwa Zanzibar kuyarejesha kabla kanuni za umoja hazijatushindikiza. Ni vyema Serikali ianze kurekebisha sheria mbali mbali zenye kuwakosesha wafanyakazi maslahi kwa mujibu wa kanuni za kimataifa.

Mhe Spika, ubora wa viwango vya bidhaa na huduma katika soko la pamoja ni muhimu kwa ushindani wa soko. Hivyo, nguvukazi iliyo elimika, yenye ujuzi na uzoefu wa kazi ndio inayohitajiwa na kila muajiri katika sekta za umma na binafsi. Naipongeza SMZ kwa jitihada zake za kuendeleza elimu ya juu katika vyuo vikuu lakini mkazo zaidi unahitajika katika masomo ya science ili kutayarisha nguvukazi inayoweza kujifunza, kuendelezwa na kutumia teknologia ya kisasa katika kazi.

Mhe Spika, suala la ujuzi na utundu wa ufundi mchundo kwa vijana wanaoshindwa kuendelea na masomo linahitaji kutiliwa mkazo ili wanufaike na soko la ajira lenye unafuu wa ujira (*cheap labour*). Hapana budi basi, hata mitaala yetu ya elimu ya msingi na kati ilenge katika elimu ya nadharia na vitendo ili vijana wetu wapate kazi zenye maslahi bora hasa kwa kuwa maslahi ya kazi yanatokana na ufanisi wa kazi kuliko bajeti ya Serikali.

Ajira maalum za Vijana

Mhe Spika, tunazidi kusisitiza kuwa kwa vile suala la uvuvi limepewa kipaumbele na jumuiya katika kupunguza umasikini, tulitarajia uvuvi

ungeshirikisha pia bahari badala ya Ziwa Victoria pekee. Hii ingesaidia kunyanyua ajira ya vijana katika ukanda wa pwani, kunyanyua kiwango cha ukuaji uchumi pamoja na kupunguza utapia mlo kwa watoto. Tunaishauri Serikali kuufanya uvuvi kuwa kimbilio la vijana sambamba na kilimo cha mazao.

Mhe Spika, tunasisitiza kuwa wakati wote wa kuzungumzia ajira, msisitizo uwekwe juu ya kuongeza ajira ya vijana na wanawake na kustaafisha waliofikia umri. Mhe Spika, sote tunaamini kuwa ukiwakosesha vijana na wanawake fursa ya soko la ajira unawaalika katika hatari za masoko haramu ya madawa ya kulevya, uharamia na umalaya. Matokeo ya masoko haya ni kushamiri kwa maambukizo ya ukimwi ambao pia tumeamua kuupiga vita kwa hali yoyote.

Mhe Spika, kwa upande wa Mashirika, Shirika la Meli na Uwakala la Zanzibar limekithiri katika ajira isiyo na tija. Shirika hili linahitaji uhuru zaidi wa kupanga mikakati yake. Katika ajira za vyombo vya baharini mpango mashuhuri duniani wa ‘kupanda na kushuka’ meli utalinasua shirika katika mtego wa matumizi makubwa yasiyokuwa na tija.

Mhe Spika, vile vile utaratibu huu utatoa ajira pana kwa vijana na katika hali hiyo Shirika litakuwa na uwekezaji mkubwa na litakuwa na udhibiti wa soko la huduma ya usafiri wa baharini Afrika Mashariki na nje. Nashauri hivi kwa sababu Soko la Pamoja linasisitiza mtandao wa usafirishaji katika kanda.

Mhe Spika, eneo jengine muhimu kwa kuongeza ajira ya vijana wetu ni katika ufundi wa matengenezo wa vyombo vya baharini. Hadi sasa kwa Afrika Mashariki ni Mombasa pekee ndiko kwenye vyelezo viwili vya kupandisha vyombo vya baharini. Iwapo Serikali itaimarisha Chelezo cha Mamlaka ya Bandari cha Malindi, vijana wengi wanaozurura ovyo watapata ajira. Eneo linalohitajika kwa kufanya chelezo si kubwa na hata mtaji wake si mkubwa. Rai hii inazidi kutilia nguvu maoni yangu kwa Serikali ya kuwa kiongozi katika huduma za usafiri wa baharini ndani na nje ya ya soko la pamoja.

Udhaifu wa Nguvukazi katika Soko la Ajira

Mhe Spika, tulijiamulia wenyewe kuwa Kiswahili ndio lugha ya taifa. Hatukukosea hata kidogo kwani kama alivyotarajia Marehemu Mwalimu Nyerere Kiswahili kimetuunganisha watanzania. Kwa hivyo, tunahitaji kukikuza, kukitumia na kukienzi kwa faida ya taifa letu na watoto wetu. Hata hivyo Mhe Spika, mahitaji ya soko jipya la ajira yanatulazimisha tujipange upya kwa kuzingatia pia matumizi ya lugha zinazotumiwa na wenzetu katika soko hasa Kiingereza na Kifaransa.

Mhe Spika, mara zote matangazo ya ajira katika vyombo vya habari yanasisitiza matumizi ya lugha nyengine hasa Kiingereza sambamba na Kiswahili. Ni ukweli usiofichika kuwa hapa ndipo panapowapa shida vijana wetu hasa katika hatua ya maongezi. Kwa vile sisi Mhe Spika muda ndio umetuacha mkono, basi natoa wito kwa vijana wetu kuwa sasa muda umewadia wazitumie kwa uwazi, na bila haya wala woga lugha za Kiingereza na Kifaransa ili kujiongezea nafasi ya kushinda mahojiano ya kutafuta kazi katika soko la ajira.

Mhe Spika, kwa mnasaba huo huo, pia naiomba Serikali kuanzia sasa ishajiishe bila woga wa kisiasa matumizi ya lugha ya Kiingereza katika midahalo na makongamano ya kitaalamu ili kuwaongezea kujiamini katika matumizi ya lugha watendakazi wetu. Tumechoka kuwaona wataalamu wetu wazuri wenye vyeo vikubwa kazini lakini wanapokabiliana na wenzao katika mataifa mengine hugeuka mababu.

Mhe Spika, tunapaswa kuiga mifano bora ya Rwanda na Burundi ambazo ni nchi zinazotumia zaidi lugha zao za nyumbani pamoja na Kifaransa lakini wanapokuwa kwenye mijadala ya kimataifa hukizungumza Kiingereza kwa ufasaha sana. Mhe Spika, nataasaf kusema kuwa haya yanatuhusu hata sisi Wawakilishi wa wananchi ambao tuna nafasi kubwa ya kujifunza na kujiendeleza katika mambo mbali mbali tukiwa hapa Barazani.

Mhe Spika, Wajumbe wako tunaendelea kupata malalamiko kuwa baadhi ya waajiri katika sekta binafsi Zanzibar hasa katika hoteli za kitalii wanaendelea kutoitendea haki nguvu kazi. Kutowapatia wafanyakazi mikataba wakati wa kuajiri, malipo madogo ya mishahara bila marupurupu kwa masaa ya ziada; kutofuata utaratibu wa kutekeleza adhabu na kutozingatia mambo ya kiusalama ni baadhi tu ya changamoto inayokabili soko la ajira nchini. Mara kadhaa mapungufu haya huzua migogoro sehemu za kazi na kesi za aina hii huwa hazina kikomo ingawa uwezekano wa mfanyakazi kushinda kesi hizo ni adimu.

Mhe Spika, haturidhishwi na utaratibu wa sasa wa utumishi (*scheme of service*) wa umma. Hakuna utaratibu bora wa kupitana kwa malipo ya kazi, hakuna utaratibu bora wa kupandishana vyeo na pia hakuna mipango madhubuti ya kuwajengea uwezo watendaji ili kukidhi mahitaji ya kazi yenyewe. Bado kuna wafanyakazi wenye kubobea kwa fani fulani lakini kwa kuwa kazi aliyosomea inashikiliwa na fulani basi ataendelea kuishikilia hata kama hana uwezo. Hili hushusha morali ya mwajiriwa na hatimae hata kuamua kukimbia ajira hasa pale ajira inapokuwa na maslahi madogo.

Mhe Spika, katika safari yetu ya soko la pamoja, ingawa nguvu kazi ina uhuru wa kwenda itakapo kulingana na maslahi ya kazi, hata hivyo itakuwa ni jukumu la Serikali kujitahidi kupunguza tatizo la kukimbiwa na nguvu kazi.

Baadhi ya sehemu za kazi zinahitaji sio tu elimu na ujuzi lakini pia uzalendo ambao husaidia kulinda heshima, mila na utamaduni wa watu. Mambo haya tutayalinda kwa kuwajali wazalendo katika kazi.

Masuala ya Watoto

Mhe Spika, mambo muhimu yanayo wahusu watoto ni pamoja na malezi bora, ukuzaji maadili, afya bora pamoja na kupata elimu mapema. Serikali imejitahidi katika kuwapatia elimu watoto wetu ingawa ongezeka la idadi ya wanafunzi halihakikishi ubora wa elimu. Elimu ya chekechea na msingi inahitaji ubora zaidi ili angalau tujigeze na skuli za binafsi. Ama kwa upande wa malezi na maadili kukosekana kwa mashirikiano miongoni mwa wazee kama zamani kuanzia ngazi ya kikoo hadi kijiji na kijamii yanaendelea kuongeza kasi ya kuporomoka kwa maadili.

Mhe Spika, utoaji wa huduma za afya ya watoto bado hauridhishi mjini na vijijini. Ukienda katika zahanati za vijijini hali halisi ni kuwa hakuna waganga mabingwa waliobobea kwa maradhi maalum ya watoto. Kwa kuwa vijijini kuna umasikini mkubwa wa kipato, dhiki ya matibabu inaongeza mzunguko wa umasikini huo. Aidha, ukubwa wa malipo ya huduma za uchunguzi wa afya na uzazi; ongezeke la vifo vya uzazi; ukosefu wa chakula bora wakati wa uja uzito, maambukizo ya ukimwi na utapia mlo kwa watoto ni changamoto inayozidi kuhatarisha maendeleo ya watoto.

Mhe Spika, wakati nikitoa pongezi kwa wizara kwa kulifanyia kazi suala la ajira ya wototo, sasa naishauri wizara kulivalia njuga suaula la watoto wa mitaani ambao sasa wanaanza kuwa ombaomba mijini na mashamba. Watoto hawa ni wale wanaotoroka skuli mapema, ingawa kuna baadhi ya wazee wanaowatuma watoto kuomba na wengine hata kuwarandisha migongoni ili kupata huruma za uombaji. Mhe Spika, iko haja ya kuwa na sheria ambazo zitawabana wazee wanaowadhalilisha watoto na kuwavunjia misingi bora ya maisha.

Mhe Spika, serikali ilifanya utaratibu mzuri wa kuwapeleka watoto katika sehemu za kurekebishwa tabia baada ya kufanya makosa makubwa. Katika sehumu hizo wanaowachunga watoto ni wazee ambao wameaminiwa na serikali na jamii. Tumepata taarifa katika Baraza hili kuwa wazee hao ‘mafataki’ sasa wanakidhi haja zao za kimapenzi kwa watoto hao. Hili si jambo la kuzungumzwa kila mara katika Baraza hili na kwa hivyo, tunaitaka serikali ishirikiane na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza hili kupata maelezo ya maovu waliyoyaona wakati wa kutembelea Chuo cha Mafunzo ili ichukuwe hatua kali pamoja na Baraza hili liarifiwe. Kuanzia sasa serikali ichukuwe hatuwa za kuwatenga watoto na ‘vitangi’ na badala yake kazi ya kurekebisha tabia wapewe kinamama majasiri.

Hitimisho

Mhe Spika, mabaliko ya kiuchumi ya kikanda katika Afrika Mashariki yachukuliwe kuwa ni changamoto ya dharura ya kuanzisha mfumo mpya wa kushughulikia na kuratibu ajira nchini. Mkazo mpya katika ajira inayoongozwa na soko huria la pamoja, hauna budi kuzingatia haja ya kuongeza uwezo wa nguvukazi katika elimu, taaluma na ujuzi wa kazi ili vijana wetu waweze kumudu ushindani wa kisoko katika ajira.

Mhe Spika, wakati tukifikiria kuwa wabia katika soko la ajira la Afrika Mashariki tusisahau wajibu wa kumuendeleza mwanamke kielimu ili anufaike na soko hilo la ajira. Serikali inalazimika kuendelea kupiga vita aina zozote za udhalilishaji na ubaguzi wa kijinsia, wa kimajimbo au wa kimaumbile katika mchakato wa kupata ajira nchini na katika kanda. Kwa vile sote tunaamini kuwa watoto ndio taifa la kesho, tuna wajibu na jukumu la kuwatayarisha ili waje wakabili mabadiliko na changamoto zinazoendelea za maisha. Kwa maana hiyo, tunao wajibu pia wa kuwarithisha taifa lenye uhuru wa matumizi ya raslimali na uchumi endelevu. Vile vile Taifa lenye amani, mshikamano na umoja wa kweli.

Mwisho kabisa, naitakia heri Zanzibar katika kura ya kihistoria ya maoni juu ya mustakbali wa utawala wa nchi yetu na kwa ujumla naitakia Tanzania Uchaguzi Mkuu wenye uwazi, haki na uhuru ili tukamilishe adhma njema ya kuwa na taifa linaloongozwa kwa misingi ya haki za kibinaadamu na demokrasia na utawala bora. Nawaomba wajumbe wote tuiunge mkono hoja na tuwaombee wenzetu wapewe matumizi waliyoyaomba na kama kuna nyongeza wafikiriwe. Naunga mkono hoja kwa niaba ya wanawake wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. Lakini kidogo nina maombi yangu ya binafsi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha ajitahidi kumsaidia Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Kwa sababu kuna kitu mbele yetu kinatukabili tena kizito na kigumu na anahitaji kupata pesa ili aweze kufanya hizo kazi na tufikie kwenye lengo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kiasi anachoomba Mhe. Waziri huwa kama anakiomba kwa ajili ya matumizi yake, lakini ukija kwenye kupewa Mhe. Waziri anapewa kasoro.

Bajeti ya mwaka jana aliomba shilingi 645 milioni, lakini alipewa shilingi 430 milioni mpaka mwezi Machi, lakini safari hii pia kaomba shilingi bilioni moja na kitu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, asipunguziwe sana kama atapunguziwa, lakini apewe kiwango ambacho kitaweza kumsaidia kufanya majukumu yake mliyomkabidhi kama serikali. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri anaunga mkono maneno hayo.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya mwanzo kuwa mchangiaji wa jumla juu ya Hotuba yake ya Makadiro ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2010/2011 ya Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwanza na mimi niungane na wajumbe pamoja na wewe kwa kutoa pole kwa wenzetu wawili Wajumbe wa Baraza hili ambao walippata msiba wa jamaa zao. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kufiliwa na watu wao wa karibu, kama Mhe. Muhyddin kafiliwa na mwanawe na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini mama yake mzazi. kwa hivyo, na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Koani tunawatakia pole na kuwa na subira. Kifo ni kazi ya Mwenyezi Mungu haina makosa, Mwenyezi Mungu awafariji.

Lakini pia nipokee pole iliyotolewa na Mhe. Aziza Nabahan Suleiman(Waziri Kivuli) juu ya matokeo ya msiba yaliyotokea Jimbo la Koani kwa ajali ambayo ilihusisha vifo vya watu wanne wakiwemo mama na mtoto. Namshukuru sana na hayo tutayafikisha kwa sababu mimi ndio Mwakilishi wa Jimbo la Koani. Kwa hivyo, hapa hapa nimeyapokea na pole hizo nitazifikisha kwa wahusika.

Juu ya hili Mhe. Spika, msiba ule umetokana na magari mabovu ya Kampuni ya *MECCO* ambayo yameletwa nchini kwa utengenezaji wa barabara. Sasa juu ya hili Mhe. Spika, naomba niseme kwanza, kwa sababu mimi ndiye Mwenyekiti wa Uingizaji wa vyombo vya moto hapa nchini. Nitahakikisha hivi sasa na serikali ivumilie sitaruhusu kamati yangu kuingiza vifaa vibovu vya kutengenezea njia na baadae kusababisha ajali, badala ya kutengeneza njia lakini vikaja kutuuwa. Kwa hivyo, Mheshimiwa nitapofanya hivyo, serikali inivumilie kwa sababu nimeshauliwa watu wangu.

Mhe. Spika, jengine ulitoa taarifa asubuhi ya pole juu ya kadhia iliyotokea jana. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM juu ya safari ya Dodoma, bahati mbaya au nzuri na mimi nilikuwa muhanga. Mimi nakushukuru nimepokea pole zao na wewe nakutakia heri. Sisi bahati nzuri wazima isipokuwa tunawapa pole wale wenzetu ambao mtu wao amepoteza roho kwa kumgonga na ile gari, lakini pia tulichukua nafasi ya kwenda kuwafariji nao waliridhika.

Mhe. Spika, mimi nimshukuru waziri juu ya taarifa yake hii. Haya aliyoandika ndio aliyoyafanya, lakini pia yana mapungufu kutokana na uhaba wa fedha. Sasa niruhusu basi kuchangia hotuba hii Mheshimiwa pamoja na taarifa ile ya hotuba ya uhai na uhiradhi wa mtoto ambayo kwa kanuni tulikuwa hatustahiki kuichangia ila tuliuliza maswali. Sasa katika mchango wangu basi nitaingiza yote mawili katika mchango wa jumla.

Mhe. Spika, la kwanza kuhusu huduma za kijamii. Kwa sababu wizara hii shughuli zake ni za MTAMBUKA, zinahusisha wizara mbali mbali. Sasa la kwanza katika suala zima la uhifadhi la uhai wa mtoto kuna jambo zito tangu mwaka jana tunalizungumza kuhusu huduma za mama katika uzazi salama. Hili katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tulilizungumza kwa nguvu zote mwaka jana na mwaka huu. Lakini bado msimamo wa serikali umekuwa mgumu na jambo hili Jumuiya za Kimataifa zinatilia mkazo. Kinamama wasaidiwe na matibabu yao hasa katika wakati wa uzazi kama hapana budi yawe bure. Wananchi hawana tabu ya kuchangia mambo mengine, lakini kwenye hizi shughuli za upasuaji wakati wa uzazi jambo hili bado ni mzigo.

Nimuombe Mhe. Waziri aandae warka rasmi sasa hivi kwa Mhe. Rais. Kwa sababu kwa mujibu wa katiba yetu rais ni sehemu ya Baraza, amwambie hasa, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi juu ya hili Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ameshindwa hataki tunakuomba na wewe rais wa nchi wananchi wetu jambo hili wanaona mzigo upunguze. Nina hakika mimi serikali inamudu gharama hizo wala haitoasirika kwa kusamehe shilingi 40,000/- kwa huduma ya upasuaji kwa wajawazito. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili namuomba Mhe. Waziri aandae kwa sababu hivi sasa tumeshafika pahala tena, yeye tu na rais ndio wanaweza kutusaidia juu ya jambo hili, bado ni mzigo kwa wananchi wetu.

Pili Mhe. Spika, linahusiana na hapo hapo kuhusu huduma za akinamama. Na hili natilia mkazo tunataka sasa hivi watoto wetu wanyonye maziwa ya mama zao. Bahati nzuri utaratibu umewekwa na bado upo, nilipouliza swali nimeambiwa upo kwa kama wale wafanyakazi wa serikali wanao muda wa kwenda kuwanyonyesha watoto walikowaweka halafu warejee. Lakini fursa hiyo imesema katika utaratibu huo hata kama pana usafiri taasisi inayohusika imsaidie mama mwenye kunyonyesha arudi amnyonyeshe mtoto kwa wakati ili watoto wetu waweze kunyonya maziwa ya mama zao.

Mhe. Spika, jambo hili katika utekelezaji linakuwa gumu, kwanza baadhi ya taasisi hizo huwa hazitoi nafasi, lakini pia na hao wanaopewa nafasi huzitumia vibaya badala yake huenda Juakali na kwengineko.

La mwisho changamoto iliyopo baadhi ya akinamama huwa hawapendi hasa kuwanyonyesha watoto kwa sababu tu atamuudhi baba maziwa yataanguka. Sasa hili Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri alifanyie kazi, ziwa ni kiungo alichowekewa mtoto, baba mtoto ana kiungo chake cha kutumia. Kwa hivyo, lazima ziwa la mama litumike kwa mtoto kwa kunyonyeshwa ili apate lishe ya kutosha. *(Kicheko)*

Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri tutoe elimu kwa akinamama wahakikishe watoto wetu wanapata ziwa la mama wakati wote mpaka anapotimiza kipindi chake cha kuachishwa au labda kama kuna matatizo mengine ndio yatumike maziwa ya kopo na mengineyo.

Mhe. Spika, eneo jengine kuhusu maji na usafiri. Katika takwimu zilizopita za miaka ya 1980 Kisiwa changu cha Uzi katika *data* zile kilionekana ni kimoja katika vijiji masikini. Lakini bado kuna matatizo ya maji, kina mama wakati wa kupumzika inabidi wasipumzike wahangaikie maji. Sasa ningemuomba Mh. Waziri juu ya hili nasema kwa lugha nyepesi ahakikishe kama yeye ni waziri ajue kinamama wa Uzi na Ng'ambwa wana matatizo ya kupata maji safi na salama. Ingawa miundombinu hiyo serikali imejitahidi, lakini maji yenyewe hayapatikani.

Sasa Mhe. Waziri washirikiane kama nilivyozungumza kuwa wizara hii ni MTAMBUKA amwambie Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kinamama na watoto hawawezi kupata maji safi na salama, kwa hivyo ajitahidi kufanya utaalamu. Kwa sababu sasa hivi nafikiri kuna suala la kitaalamu basi na yeye atusaidie na mimi mwenyewe kila siku naamkia huko, lakini nafikiri kazi ikifanywa mikono mingi nzuri kwa kazi hata Wahindi wamezungumza, arabu ya kula tu. Kwa hivyo, mimi na yeye tukifanya kazi nafikiri tutafanikiwa.

Mhe. Spika, eneo jengine ni barabara. Bado wakati mwengine wagonjwa wa Kisiwa cha Uzi wanapata tabu inabidi lazima wavuke. Lakini pia Mwenyezi Mungu katujaalia pale maji baadhi ya wakati yanatoka tumetengeneza barabara yetu, bado dhaifu, tumejitahidi wenyewe kupanga mawe lakini haitoshi lazima tutataka nguvu za serikali. Wakati mwengine tunakuwa na wajawazito, wakati mwengine haijambo kama mtu kajikata panga unaweza kumfunga *bandage*, lakini mja mzito wakati huo wakunga wa kienyeji wameshashindwa anataka kuletwa Hospitali ya Mnazi Mmoja *Ambulance* haifiki tunampa tabu, basi angalau ile barabara tukiweza kusaidiwa itapitika. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atusaidie na hasa tunawalilia hawa kinamama na watoto ili kupata huduma.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 58 na 64 kifungu cha 75 na 85 kinachohusiana na Mfuko wa Kujitegemea. Mhe. Spika, nashukuru sana kuletewa Mfuko huu na namna ulivyotumika, lakini bado haujaweza kuondoa kiu ya wananchi kwa kupata yale mafao halisi ili waweze kutumia kuondosha umasikini. Fedha hizi zimekuja kwa kuzisikia au kuziona tunasema nyingi sana, lakini baada ya kufika kwenye utekelezaji ni ndogo sana. kwa mkupuo tu katika Mkoa wetuhizi zimekuja kwa *pilot* tu, zimetosheleza kwa majaribio lakini ule mchezo hasa bao.

Nimuulize Mheshimiwa sasa huu mchezo na tuliambiwa pesa hizi baadae zitaletewa ni lini? Fedha hizi kwa miradi iliyopewa vijiji hivi ni kwa majaribio

na takriban kila jimbo labda wamepata mradi mmoj mmoja tu, sasa mchezo kamili utakuwa lini ili hizo fedha ziweze kuendelea. Katika hiyo *pilot survey* je, maendeleo yake yako vipi? Mheshimiwa atueleze ili na wale wenye kutoa feedha wapate moyo wa kuongeza fedha hizo. Au kuna maharibiko, kwa sbabu tunaona kimwa na wananchi wanaanza kupiga kele, fedha za Karume wee, fedha za Kikwete hatuzioni, kwa nini zimekuwa sasa hivi baada ya kumalizika hakuna utaratibu wa wananchi kuweza kujua siku gani wataweza kupata.

Mhe. Spika, niende ukurasa wa 16 Afisi Kuu Pemba. Mhe. Spika, nashukuru sana wizara hii hasa kutokana na afisi ya Pemba juu ya shughuli wanazozifanya. Miradi ya vikundi vya kinamama inakwenda vizuri sana na bado iko hai, lakini vile vile kuna matatizo. Matatizo yaliyokuwepo na wakati nilipokuwa kwenye Kamati ya Ustawi wa Jamii ilikuwa usafiri. Nashukuru kwa pale ofisini wamepata gari moja, lakini wataalamu au maafgisa kufuatilia miradi kule na kama unavyojua elimu zao ndogo usafiriwa kutoa elimu maafisa wetu hawana.

Kama tunavyokujua Kisiwa cha Pemba baskeli haiwezi kwenda inakuwa ni vigumu, hata hizo skuta kama tunasema tunawapa labda watakwendea Chake Chake na Mkoani kwenye barabara lakini kumfatia mtu Mgelema, Pujini au Kichuani ni vigumu.

Mimi nimekwenda na Mhe. Najma Halfani tumeanguka zaidi ya mara tatu kule haifiki hata kidogo, labda watafutiwe kirongwe. Kwa hivyo, Mheshimiwa basi watafutiwe angalau gari zitazoweza kufuatilia miradi ya wananchi kule waliko ili iendelezwe. Kwa sababu lazima kuwe na ufuatiliaji na wengine wanakuwa hawana taaluma, taaluma ya kupewa mara moja tu haitoshelezi lazima akaongezwe taaluma ili ule mradi wake uwe *sustainable*. Kwa hivyo, Mhe. Spika, na hili Mhe. Waziri alione. Gari kwa ufuatiliaji wa miradi ya akinamama na vijana kule hakuna, hivyo serikali iwapatie.

Mhe. Spika, jengine haraka haraka kwenye Mfuko wa Ibara ya Vijana. Ibara ya vijana tumeona shughuli za mwenge zimekwenda vizuri na kadhalika. Lakini bado eneo la Mfuko wenyewe hasa haupo kwa vijana na vijana tunazungumza ndio wenye kilio cha ajira. Mtu mzima si sana kusikia mambo ya ajira kwa sababu pengine keshafanya kazi kashachoka, lakini vijana bado wanahitaji mengi. Mfuko huu miaka ya nyuma tulikata baadhiya idara wakati tuko kwenye kamati kuongezea.

Sasa kwa ufupi Mhe. Spika, ningeiomba serikali kwa uchache wake kila Mkoa ukapata angalau shilingi 50 milioni kwa miradi, yaani fungu zima la vijana liwe angalau shilingi 500 milioni ili kuendeleza vijana, la si hivyo hawa wenzetu tutawapa kazi bure. Vijana hawasikii, taaluma wanasoma. Nashukuru vijana

sasa hivi wanajiendeleza vizuri sana kiskuli. Wamekubali elimu na wakati wa jioni tunaona wanakwenda wakisoma masomo ya ziada.

Mhe. Spika, haya ni maendeleo yanatia moyo, lakini akimaliza anataka kuitumia elimu ile, hawa wenzetu tumewaweka wawatayarishe ili waanze maisha mengine mapya baadae watakwenda kama kwenye biashara au vipi, lakini angalau kuwa na Mfuko wa kuanzia. Sasa fedha hizi zinakuwa chache au hazimo kabisa. Mhe. Spika, hili nalo tuna mapungufu.

Mhe. Spika, baada ya hilo basi niwapongeze vijana wetu ambao wamefanya vizuri kwenye michezo, lakini ili kufanikisha haya, waongezewe vifaa waweze kupatiwa hasa na sehemu za viwanja vya michezo vimekuwa vigumu kama ilivyoelezwa na Mwenyekiti wa Kamati hapa. Vijana sasa hivi nafasi za michezo hazimo na vijana wetu wanakuwa wengi na michezo ni sehemu ya maisha kwa vijana kwa kukua ili kuwapa akili.

Mhe. Spika, baada ya hayo basi nirejee kuwashukuru watendaji wote kwa kazi zao nzuri na mimi nakubaliana hizi fedha alizoziomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Koani tunaiomba serikali iwape. Ahsante sana.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya wizara hii. Kwanza naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa namna ambavyo amewasilisha bajeti yake na pia naomba niwapongeze sana watendaji wake.

Mimi Mhe. Spika, ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC* ya Baraza lako na kwa kweli mara nyingi tunapoitembelea wizara yake wanajaribu sana kudhibiti matumizi ya serikali. Kwa hivyo, naomba wapokee pongezi zangu sana katika hilo.

Jambo jengine Mhe. Spika, ni kwamba Mhe. Waziri katika kitabu chake kifungu cha mwisho, naomba kunukuu.

Kifungu cha 93 kinasema:

> "Kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wapokee, wajadili, watupe ushauri na maelekezo, hatimae kupitisha makadirio na kuidhinisha jumla ya shilingi 1,086,000,000/= ikiwa ni fedha za kazi za kawaida na shilingi 60,000,000 zikiwa ni fedha za kazi za maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2010/2011".

Sasa Mhe. Spika, mimi sina tatizo kubwa tatizo langu ni kidogo sana kwa Mhe. Waziri kupewa hizi pesa, sasa sijui utaratibu gani ambao unatumika kuomba fedha ndogo namna hii. Hii wizara ni wizara muhimu sana, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa shilingi 1,060,000,000/- kwa

kweli nahisi ni fedha ndogo sana. sasa ikiwa kweli wanataka kutekeleza majukumu ni vizuri akajitahidi kujenga hoja ili kuona anapata fedha ya kutekeleza majukumu yake. Vyenginevyo itakuwa kila mwaka anakuja hapa anatwambia nimefanya hiki na hiki hakikuwa, kwa sababu hawezi kufikia lengo kwa pesa ambayo anapewa *one billion*. Nimeangalia Kikosi cha Valantia ni *two billion*.

Sasa ikiwa wizara nzima inapewa bilioni moja, Kikosi cha Valantia kinapewa bilioni mbili, kwa kweli inaonekana ama hatujawa *serious* serikali kwa jumla au waziri mwenyewe hajajenga hoja ya kutosha kuona kwamba ana majukumu mengi katika wizara ya kuyafanyia kazi. Sasa hili naomba labda aje anisaidie kidogo.

Lakini baya zaidi katika hili, nilikuwa naangalia hili buku la makadirio ya mapato na matumizi. Kuna ukurasa ambao fedha za kazi za kawaida sina matatizo nazo, ndio zile ambazo Mhe. Waziri ameziomba. Ukurasa wa 51 Fungu Vote 28, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ameomba shilingi 1,086,000,000/-. Sina tatizo hata kidogo.

Lakini pia kuna ukurasa wa kazi za maendeleo, ukurasa wa 515, Fungu Vote 28 tena Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Hapa kuna fedha ambazo zimewekwa, zimekadiriwa kwa ajili ya shughuliza maendeleo katika wizara hii shilingi 3,730,080,000/-. Lakini waziri yeye katuomba tumpatie shilingi 60 milioni tu, sasa hapa nina tatizo kidogo. Je, ni kweli anahitaji shilingi 60 milioni tu, asije akasema tumpe shilingi 60 milioni halafu wakati wa kupitisha vifungu hapa akatuomba shilingi 3,730,080,000/. Nafikiri hapa kuna tatizo ambalo ni lazima liwekwe sawa.

Kwa sababu Baraza linapopitisha huwa linapitisha fedha zile za *contribution* ya serikali lakini pia zile za wafadhili. Sasa ni vizuri hii *paragraph* ya 93 nahisi ina matatizo ambayo inaomba fedha za kawaida na za maendeleo.

Mimi kwa maoni yangu ni kwamba ikiwa ni fedha za kazi za kawaida sio shilingi 60 milioni pale, hapa pangepaswa kuwa na shilingi 3,730,080,000/- nafikiria hivyo. Lakini ikiwa mwenyewe anahitaji hizi shilingi 60 milioni tu, mimi sina tatizo hata kidogo Mhe. Spika, lakini hapa pia ningeomba ufafanuzi wa tatizo hili.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ningeishauri wizara ni kuangalia vipaji vya watoto wa kike katika skuli. Kuna wakati baada ya mitihani vijana wa kike huwa wanafanya vizuri katika mitihani yao ya *Form IV, Form VI* hata Vyuo Vikuu. Lakini hatuna utaratibu ndani ya serikali yetu ya kuangalia wale watu wenye vipaji hasa wanawake na kuwaendeleza, sasa hili ni tatizo. Mimi ningeshauri Mhe. Waziri angelikuwa na utaratibu huo. Kwa sababu kama

tunataka kumuendeleza mwanamke hatuwezi kumuendeleza kwa kumpa mkopo wa shilingi 40 elfu tukamwambia fanya biashara ya mama ntilie. Kwa kweli pahali pazuri pa kuanzia ni hapa, unaaza na kwenye maskuli, unatafuta vile vipaji (*best brain)* unaziendeleza halafu unazilea ndio baada zinatumika.

Sasa mimi ningeshauri hilo afanye, wenzetu wanafanya sana hili, wanajaribu kuzi-*sport* mapema *best brain* katika nchi. Sasa kwa sababu sisi tunataka tuendeleze wanawake lazima tuliangalie hilo. Kila mwaka tunafanyua mitihani, kuna watoto wanawake wanafanya vizuri, lakini wengine wanyonge wazee wao hawana uwezo na wanabakia tu kwa sababu ya unyonge wa wazee wao hawapati nafasi ya kujiendeleza. Hili ni jukumu la wizara hii kuona kwamba wanawaangalia wale watoto wanawake ambao wamefanya vizuri skuli halafu wakawatafutia namna ya kukuza vipaji vyao.

Lakini pia katika maeneo ya majira kuna matatizo mengi, hata watoto wanawake wanapomaliza skuli wanapofika katika sehemu za kazi kuna matatizo mengi. Sasa ningewashauri na hilo pia kuliangalia namna gani kupunguza ule mkandamizo wa wanawake, ule mfumo dume kidogo kuupunguza na kuangalia namna gani wanawake watapata *exposure*. Kwa sababu wanawake watakuwa wamesoma vizuri, lakini kukosa *exposure* bado anakuwa hana uwezo wa kufanya kazi vizuri. Kwa hivyo, hili ningeshauri kwamba, ni jukumu la Mhe. Waziri angeliweza kufanya gani akachukua katika suala hilo, vyenginevyo tutakuwa nyuma katika suala hili.

Mhe. Spika, jengine nimeona kuna Idara ya Maendeleo ya Jamii. Sasa mimi nikasema hivi hakuwezi kuwa na *duplication* ya majukumu. Kule Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuna Idara ya Ustawi wa Jamii, huku kuna Idara ya Maendeleo ya Jamii. Sasa nilikuwa najiuliza mambo haya vipi, ustawi na maendeleo ukiangalia ni suala moja, sijui nini tofauti ya idara hizi mbili. Kweli ziko katika wizara tofauti lakini bado nahisi zina ukaribu wa lugha, sasa sijui majukumu yao yakoje.

Mhe. Spika, jengine ni Kamisheni ya Kazi, kwanza inafanya kazi nzuri lakini bado ina kazi kubwa sana, tuna tatizo la ajira za wageni. Sasa hili jambo nahisi Mhe. Waziri angelisimamia kwa ukaribu zaidi kuisaidia kamisheni yake kuona kwamba hatuwezi Zanzibar kazi chache tulizonazo kuendelea kuchukuliwa na wageni. Wazanzibari na sisi tuna mashaka yetu, tuna umaskini wetu na mtu kumpatia ajira ndio aina moja ya kumsaidia angalau kutafuta kijio. Sasa hata kama kazi chache zilizopo nazo wageni wanazichukua kwa kweli hili ni jambo ambalo linapaswa tulishughulikie na katika hili tuondoe muhali sana.

Mhe. Spika, mara moja mimi nilikwenda nchi za nje, mimi kwa taaluma ni mhandisi, nikapata kazi. Baada ya muda wenyeji wakaja wakasema kwamba huyu jamaa ni mhandisi kweli lakini na sisi ma-*technician* tupo ambao ni

wenyeji wa nchi tukipewa uzoefu kidogo na sisi tutafikia ngazi ya uhandisi. Kwa hiyo, wakanambia bwana itabidi utusamehe tuna vijana wetu tunataka hii kazi waifanye wao. Bila ya muhali, bila ya lolote, nilikuwa nafanya kazi na kampuni ya nje lakini hawakujali. Sasa meneja wangu alikuwa mkali kidogo lakini hatimaye ilibidi asalimu amri.

Sasa Mhe. Spika, hapa Zanzibar tuna tatizo kubwa sana, kazi tunaona muhali sana hatimaye wenzetu majirani zetu wanaona hapa ni *safe heaven* ya kutafuta ajira. Kwa kweli wanakuja hapa wanafanya kazi hawatumii fedha ile inakwenda kwao inawasaidia wao na watu wao, sisi tunatumbua macho watu wetu wanabakia na unyonge. Sasa hili Mhe. Spika, halipasi kuwa na muhali hata mdogo vyenginevyo tutakuwa na matatizo makubwa.

Mhe. Spika, jengine ukurasa wa 37 Idara ya Wanawake na Watoto na mashirikiano na *UNICEF* na kutengeneza sheria ya mtoto. Mhe. Spika, mwenzangu amesema nafikiri ni Mhe. Mwenyekiti wa Kamati na mimi naomba hapa tuwe makini sana tusiburuzwe na ufadhili mno tukaacha malengo, silka, tabia na dini. Mimi sijaiona hiyo *draft* ya sheria, lakini kuna mtu mmoja alinambia kwamba kuna kipengele ambacho ukimpiga mtoto basi mzazi anaweza kufikishwa Mahakamani akapata kifungo.

Sasa kama ni kweli Mhe. Waziri nafikiri hatujafika huko mimi sijaiona inawezekana si kweli, lakini kama ni kweli Zanzibar hatupaswi kuwa na sheria za aina hiyo. Pamoja na fedha nyingi walizonazo wafadhili tunahitaji lakini tuwaambie aaa kwa hili mtatusamehe kidogo bado na *inshaallah* hatutafika huko. Mhe. Spika, hatupaswi kuwa na utovu wa nidhamu wa watoto kupitia huko tu kwa sababu tunaiga umagharibi. Naomba sana Mhe. Waziri kama imo basi uangalie sana silka, mila na utamaduni na kwa ulivyo najua hilo utalishughulikia sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine ni ujenzi wa Afisi Kuu Pemba. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa hatua yake ya kutaka kujenga ofisi Pemba ya wizara yake ni jambo zuri kwa sababu wengine wengi hawajaanza na wameshindwa. Lakini hapa kuna jambo limenishtua kwamba ujenzi huo unaofanywa *paragraph* ya 86 naomba kunukuu: “Mhe. Spika, ujenzi wa Afisi Kuu ya Wizara Pemba unasimamiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi”.

Mhe. Spika, nimeshtuka kuona kwamba afisi yake Mhe. Waziri anayojenga inasimamiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi. Wizara ya Fedha na Uchumi inajenga afisi yake kule Pemba lakini inaporomoka. Sasa nikahofu kwamba yeye mwenyewe ameshindwa kusimamia ujenzi wa afisi yake, wewe ndio umempa afisi yako kukujengea, hofu yangu utakwenda kukuta kiwanja siku ya pili.

Mhe. Spika, nakumbuka kuna utaratibu wa *tender board* katika mawizara na sheria ya manunuzi ya mwaka 2005 inaipa uwezo Kamati ya *Tender Board* ya Mawizara kusimamia shughuli za aina hii. Sasa nilikuwa najiuliza ni kwa vipi *Tender Board* ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto isimamie ujenzi wa afisi yake Pemba hata ikasimu madaraka hayo kwa Wizara ya Fedha, kila mmoja ana jukumu lake na kila mmoja ana *tender board* yake anaweza kusimamia shughuli yake kwa mujibu wa sheria ile ya *procurement* ya mwaka 2005.

Sasa Mhe. Spika, ni kwa vipi Mhe. Waziri shughuli hii aikabidhi Wizara ya Fedha hali ya kwamba sheria inamruhusu na yeye kufanya shughuli hizi.

Mhe. Spika, nilikuwa na mambo mengi lakini kwa kumalizia naomba nishauri tu kwamba katika kiambatanisho namba 1 ukurasa wa 75 kuna shughuli za wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa mwaka 2009/2010. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa uamuzi wake wa kusomesha wafanyakazi 31, wanawake wakiwa 21 na wanaume 10, ama kweli hii ni Wizara ya Wanawake.

Mhe. Spika, tatizo nililoliona ni kwamba Mhe. Waziri hakutwambia hawa wafanyakazi wamesomea nini. Kwa mfano, shahada ya pili hakutwambia wamesomea nini, au shahada ya kwanza wamesomea nini, au diploma wamesomea nini. Kwa hiyo, ningeshauri mara nyengine hizi kada ambazo wamesomea basi nazo tukajua kwamba labda katika wizara hii kuna utaalam wa kiasi gani.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa muda ulionipa na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuja kwenye Baraza kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, pia nikushukuru wewe binafsi kunipatia nafasi hii pamoja na kwamba nilipendekeza pengine nichangie baadae ili kama kuna watu wengine watachangia masuala ya wizara yetu tuweze kuyaeleza kama walivyotangulia. Lakini hata hivyo, naomba nichangie kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nianze na malengo ya wizara. Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwa na malengo madhubuti ya kuimarisha wizara yake hasa kwa kuwapeleka wafanyakazi wake katika mafunzo mbali mbali katika maeneo ya utendaji pamoja na ya ufundi.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba nalipongeza hilo kwa sababu unapowasomesha wafanyakazi basi wanakuwa na uwezo mzuri wa kufanya kazi zao kama vile ambavyo inahitajika. Kama baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walivyosema, nafikiri Mhe. Aziza Nabahan Suleiman alizungumza hili kwamba tunahitaji watu ambao wana elimu ya kutosha ili kuweza kufanya majukumu yao vizuri katika utekelezaji wa kazi zao za kila siku. Mhe. Spika, kwa hilo naomba nipongeze hatua hiyo ya wizara.

Lakini pili Mhe. Spika, naomba vile vile niipongeze wizara kwa kuwa na uwiano mzuri wa wafanyakazi wake na hasa katika sekta hii ya uongozi. Kama walivyosema wajumbe waliotangulia kwamba wizara hii ni Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, kwa hiyo wafanyakazi wake wengi ni wanawake. Niwapongeze basi na wao kwa hatua ambazo wamezichukua kuona kwamba kinamama nao wamo kwa wingi katika wizara hii na hasa katika nafasi mbali mbali za uongozi.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu wizara kuamua kwa makusudi kuwajengea uwezo wafanyakazi wake katika sekta ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hili nalo vile vile naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwamba wizara ina mkakati madhubuti wa kuona kwamba tunaondokana na umaskini kupitia Mpango Mkuu wa Serikali wa MKUZA.

Mhe. Spika, jengine ni ile dhamira ya wizara kuona kwamba tunaondokana na tatizo la madawa ya kulevya pamoja na kupunguza athari za ukimwi. Mhe. Spika, mambo haya mawili yaani madawa ya kulevya na ukimwi yanakwenda sambamba. Kwa sababu unapokuwa unatumia madawa haya basi unapungukiwa na uwezo wa kufikiri, kwa hivyo una uwezo mkubwa wa kuweza kuambukizwa au kuambukiza wewe ukimwi kwa mtu mwengine. Kwa hivyo, wizara hii kwa kuwa wameliona hili na kulifanyia kazi naomba niipongeze wizara.

Lakini pia Mhe. Spika, ili uweze kutekeleza majukumu yako vizuri basi unahitaji kuwa na fedha za kutosha ambazo zitakufanya wewe uweze kufanya kazi zako vizuri. Waheshimiwa Wajumbe wengi waliochangia wamezungumzia kwamba wizara hii pengine ina fedha kidogo ambazo zimeombwa kwa ajili ya utekelezaji wake wa kazi za kila siku pamoja na kazi za maendeleo. Kwa hivyo, mimi nataka niungane na wale waliosema hivyo kwamba ni vizuri wizara wakae pamoja na watendaji wake kuona kwamba wanaomba fedha ambazo zingeweza kukidhi mahitaji ya kila siku katika maeneo hayo.

Pamoja na kwamba wanaweza wakaomba hizo fedha lakini wakaweza kupata upungufu kama zilivyo wizara nyengine, lakini pengine wangeomba nyingi

zaidi wangeweza kupata zile ambazo pengine angalau nusu ya yale mahitaji yao.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu azma na utekelezaji wa wizara hii kuondoa ajira za watoto. Mhe. Spika, kama tunavyoelewa kwamba watoto wanahitaji malezi bora na tunasema siku zote kwamba watoto ni taifa la kesho. Sasa itakapokuwa watoto wetu wanafika kuwa wanafanya kazi hizi za ajira na wanaacha kusoma, maana yake maendeleo yao ya baadae pamoja na wazee wao yatakuwa duni. Kwa sababu mtu ambaye atakuwa hajasoma katika ulimwengu ujao atakuwa hana nafasi kubwa ya kuweza kukidhi maisha yake lakini pia kuweza kusaidia jamii yake ambalo ni jukumu la lazima kwa binadamu yeyote. Sasa mimi naomba niipongeze wizara kwa hili.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu vitendo vya unyanyasaji. Mhe. Spika, naomba niipongeze wizara kwa kushughulikia suala hili la unyanyasaji wa watoto na hasa kijinsia. Mhe. Spika, vitendo hivi vya kuwanyanyasa watoto kijinsia vinajitokeza sana katika nchi yetu hasa katika miaka hii ya karibuni. Pamoja na kwamba huko nyuma yalikuwa yakitokea lakini yalikuwa kidogo yana nafuu, lakini kipindi hichi cha karibuni yamekuwa yakijitokeza sana.

Sasa naipongeza wizara kwa kulishughulikia hilo, lakini pia naomba ichukue hatua zaidi kuona kwamba kuwepo na utaratibu maalum ambao utashughulikia hizi kesi. Pengine niziombe taasisi husika hasa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kuona kwamba kunakuwa na utaratibu mzuri wa kushughulikia hizi kesi. Mhe. Spika, hivi sasa hizi kesi zinashughulikiwa lakini katika ushughulikiaji wake sasa kidogo hauleti tija kwa sababu muda unakuwa mrefu, pengine kunakuwa na mambo ya labda wazazi ambao ndio sisi tunafikia pahala kusameheana kwa mambo yaliyofanywa ya udhalilishaji wa watoto. Kitu ambacho unapoyasamehe makosa kama haya makubwa maana yake unayafanya haya makosa yanakuwa sugu.

Kwa hivyo, ningeiomba sana wizara ikashughulikia hilo na nafikiri wizara inalitazama hilo. Kwa sababu wakati mwengine wizara nimepata kuona hasa wanakata rufaa jinsi ya hukumu zinazotolewa ambazo wizara wenyewe hairidhiki na maamuzi yale yaliyotolewa. Mhe. Spika, naomba niwapongeze sana wizara lakini pia naomba wachukue juhudi zaidi kuona kwamba wanafanya kazi hiyo kwa manufaa ya taifa letu.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Waziri Kivuli alikuwa anazungumzia masuala kama mawili katika wizara yangu. Moja alikuwa anazungumzia suala zima linalohusiana na kujenga utaratibu mzuri wa kazi, yaani katika ajira za melini tuweke utaratibu wa *sign in* na *sign off*. Mhe. Spika, kama tunavyokumbuka kwamba tayari wizara yangu imeshasoma bajeti yake na hili limo na

tumeshalizungumza. Kwa hivyo, nataka kumkumbusha Mhe. Mwakilishi kwamba hilo limo katika wizara yangu.
Lakini jengine la kuhusu chelezo katika Bandari ya Malindi, nalo pia katika bajeti yetu ya wizara tayari tumeshalifanyia kazi na mwaka huu ujao wa fedha tunategemea kwamba kukiimarisha chelezo hicho na kuweza kufanya kazi zinazohusiana na meli kabla ya kuzipeleka chelezoni kule Mombasa kwa yale mambo ambayo yatakuwa pengine yako nje ya uwezo wetu kiufundi.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Haji Mkema Haji alizungumzia kuhusu barabara yake ya Uzi katika eneo lile ambalo linavuka kwamba barabara pale kidogo hali yake sio nzuri. Kwa hivyo, aliiomba wizara yetu ishughulikie hilo eneo.

Mhe. Spika, nataka kumhakikishia Mhe. Haji Mkema Haji kwamba ushauri wake huo na maombi hayo tunayachukua na tutayafanyia kazi katika wizara yangu kuona kwamba hilo eneo tunalifanyia kazi ili wananchi wa eneo hilo wasipate shida.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na maelezo machache kwa sababu nilikuwa naangalia kuona kwamba kama kutakuwa na maelezo ambayo yanatugusa moja kwa moja kama walivyochangia wajumbe tuweze kuyatolea ufafanuzi. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Chaani tunaunga mkono bajeti hii ya wizara kwa asilimia mia moja. Tunaomba yale mafungu yote ambayo yamepangwa basi wapewe ili waweze kutekeleza kazi zao. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kutoa machache kuhusiana na bajeti hii ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, pili namshukuru *Allah* kwa kutuweka hai na tukawa wazima na tukapata fursa hii ya kuzungumza.

Mhe. Spika, kama ambavyo walitangulia baadhi ya wenzangu kuzungumza kwamba katika serikali ni muhimu kutoa kipaumbele kwa yale mambo ambayo yana uzito. Sasa labda tatizo hili la kwanza tuliachie serikali. Hii wizara huko nyuma ilikuwa haipo, huko nyuma hakukuwa na wizara maalum inayohusiana na mambo ya wanawake na watoto. Lakini pia huko nyuma kulikuwa hakuna vikosi vya SMZ, kwa hivyo yote mawili ni mapya. Sasa sababu maalum ya kuifanya hii wizara ikawa finyu na haina bajeti mimi siioni. Kama ni upya basi na vile vile ni vipya. Kwa hivyo, tuangalie maeneo ambayo yangeweza kutusaidia na sio kuendeleza mazungumzo tu kila siku.

Mhe. Spika, la pili bajeti yetu ya serikali ni ndogo kama ambavyo tunalizungumza kila siku. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi aandae mipango mizuri zaidi

ya kutoa vyanzo vipya vya mapato ili wizara mbali mbali ziweze kujikimu. Mhe. Spika, bajeti ambayo inapangiwa wizara hii na majukumu yake hayalingani, sasa inabidi wote wawili wafanye kazi kwa pamoja.
Mhe. Spika, tunamuomba mheshimiwa huyu niliyemtaja mwanzo na Mhe. Waziri wa Wizara hii wafanye kazi kwa pamoja. Ikiwa atakuja kurithi katika kipindi cha Baraza lijalo au atamwachia mwengine. Lakini wataalam wa dunia wanapenda sana kitu wanachoita *legacy*, yaani kuweka kitu ambacho mwenzio atakuja kurithi atakuona kwamba umefanya jambo kubwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aende akapiganie huko katika ngazi za juu za Wizara ya Fedha, ikiwa ni kamati ya ceiling au kamati nyengine, lakini wizara hii bajeti yake ipandishwe kidogo. Hilo la mwanzo.

Mhe. Spika, la pili nilitaka kuzungumza tena kuhusiana na hii Kamisheni ya Kazi. Kwanza ripoti zinazokuja katika vitabu vya bajeti zinakuwa mpya mpya, sasa unaweza kujiuliza lile kongwe liko wapi. Tulikuwa na suala la mikataba ya kazi hatujaelezwa imefikia wapi. Utaratibu ule wa mikataba ya kazi hasa katika ajira binafsi umefikia wapi. Kazi imemaliza na sasa hivi katika ajira binafsi mikataba ile imeshawekwa na ndio inayofuatwa au vipi.

Lakini jengine ni kufanya kazi pamoja na Tume ya Utumishi Serikalini, ni suala zima la kufuatilia nguvu kazi ya nchi. Tungesema kwamba moja katika kazi ya kamisheni ni kufuatilia kwa karibu na kuchambua nguvu kazi ya nchi *(manpower scrutiny and analysis).*

Kwa nini nikasema hivyo. Kwa sababu sisi tunavyo vyuo vyetu sasa hivi, tuna taasisi mbali mbali za kielimu, kuna vijana wanakwenda nje kusoma katika fani mbali mbali. Sasa kama hakuna ufafanuzi huu inawezekana ikawa tunasomesha wengi lakini katika fani chache na kuna fani muhimu vijana wetu hawaendi.

Mhe. Spika, kwa mfano, wakati nazungumzia katika Tume ya Utumishi niliwaambia kwamba uchambuzi unaonesha fani ya uhandisi *(engineering)* na fani ya *fisheries* haina watu katika Zanzibar, utafiti wa ghafla ghafla. Lakini kama Kamisheni ya Kazi wangelifanya uchambuzi huu ingeliona na ingetoa ushauri wake kwa wizara mbali mbali kupeleka watu wa aina hii kusoma.

Mhe. Spika, mimi nilipokuwa mwalimu tulipata ugeni kidogo wa walimu fulani kutoka Marekani walikuja kulikuwa na *workshop* yetu. Sasa yule profesa alizungumza hivi kwamba katika miaka ya 80 Marekani ilibadilisha *curriculum* yake kabisa kabisa kwa sababu ya Japan tu, waliona kinchi kidogo kile Kijapan kinaiweza Marekani kwa kuleta vitu vya ma-*electronics* kwa nini. Jinchi kubwa kama lile Marekani lenye 51 *states* linapitwa na nchi ndogo tu ya Japan.

Kwa hivyo, waliona kwamba utaratibu ni kubadilisha *curriculum* yote na huyu alikuwa ni mtaalam wa kielimu yaani mtu wa *education*. Wanasema hata vile

vitabu na kila kitu kilibadilishwa kwa sababu ya kujifunza kwamba kwa nini Japan kinchi kidogo kinawapita wao jinchi kubwa kama lile, inabidi wao waagize vitu kutoka Japan.

Sasa fani ya *technology*, *engineering* na *fisheries* ambapo sisi tumezungukwa na bahari fani hizi hazipo. Sasa ni sababu gani zinazopelekea fani hizi kutokupata watu. Kwa hivyo, katika kupanga huu utaratibu wa ajira inawezekana ajira hazipatikani kwa sababu zile fani tunazosomesha sisi sizo tunazozihitaji, wengi wanakwenda katika fani ambayo haihitajiki sana na matokeo yake ajira inakuwa ndogo. Lakini pengine kuna mahitaji ya watu wa aina hii na hii.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nafikiri ni vizuri zaidi kuandaa utaratibu wa kufanya huu utafiti au uchambuzi wa namna gani wanafunzi wetu wanaotoka katika vyuo mbali mbali, wanaotoka nje na ajira ambazo zinakosekana au mahitaji yaliyopo. Hilo la pili.

Mhe. Spika, la tatu kuhusiana na misaada hii ya *SACCOS* na mengineyo. Mhe. Spika, mimi mawazo yangu nilifikiria zaidi kwamba tupo zaidi katika kufanya biashara ikiwa ndogo ndogo au kubwa kubwa, lakini hatujalenga zaidi katika uzalishaji, uzalishaji wetu ni mdogo sana si katika kiwanda wala si katika ardhi. Wale ambao wanazalisha zaidi katika ardhi sio wale wanaopewa ile misaada. Kwa hivyo, bora afadhali tufanye utafiti wa kuona wale ambao wanatoa bidhaa iangaliwe hapa gari gani inayoleta ndizi, inayoleta muhogo. Ikiwa inatoka Matemwe basi tuelekee kule Matemwe, lakini ikiwa gari ya muhogo inatoka Matemwe sisi tukaelekea Nungwi au tukaelekea Fuoni itakuwa hatufanyi haki.

Wataalamu wa kibajeti wanasema bajeti ni ile inayotoa fursa wa kiwiano wa usawa katika maendeleo. Kwa hivyo, wale wanaosaidiwa ndio wasaidiwe.

Mhe. Spika, sasa *phase* yetu ya pili tumeanza vizuri na tumewasaidia wengi katika fani ya biashara ndogo ndogo. Basi *phase* yetu nyengine tuangalie uzalishaji sasa ili watu wetu wawe wazalishaji zaidi, kuliko kuwa wauzaji tu, waweze kununua na kuuza.

Kwa hivyo, mimi naomba niseme kwamba tufanye utafiti katika fani hiyo je, tunaweza tukaongeza. Kwa mfano, kuna mradi hapa unatolewa mpaka zawadi. Wanao pale *Chamber of Commerce* na wengineo, lakini wao wanataka *value added product*. Usinunuwe unga ukauza unga, ununuwe kitu ukiongezee thamani yake hii huulizi kitu chengine, hii inahitaji utaalamu. Tena wanapewa msaada, kwa sababu mimi nimezungumza nao wanasema wanapewa msaada tena wa kifedha kabisa. Lakini ina maana kunataka wataalamu. Ikiwa unanunua yai na ukauza yai basi angalau uuze keki, kwa sababu utakuwa umeshalifanyia matengenezo kidogo, tusibaki hapa hapa. Mhe. Spika, alisema Mhe. Waziri

Kivuli hapa kwa urefu sana, kuhusiana na soko tunaloendelea nalo la Afrika ya Mashariki, sina haja ya kulizungumza mimi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo naomba wizara iliangalie nimeona mambo mengi sana ni *UKIMWI*, lakini *UKIMWI* una vyanzo, haupatikani tu. Mhe Spika, leo asubuhi nilikuwa nikisikiliza habari. Mmoja akasema kwamba huyu, kwa kizungu anashughulikia *symptoms*, hashughulikii *symptoms* tu ya mambo mengi yaliyojificha, sio tatizo hasa. Tunawaomba sana wizara hii ndio maana nikasema iongezewe pesa ili ishiriki kikamilifu katika vita vya madawa ya kulevya, kwa sababu inahusu *young generation*. Vijana wetu wamebadilisha sauti, wamebadilisha mwendo, wanabadilisha mavazi na hakuna hata kitu kimoja ambacho kimebaki katika miili yao ambacho hakijabadilika.

Mhe. Spika: Dakika mbili bado.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante. Lakini la mwisho, nataka nizungumzie kuhusu suala la kupanga kima cha chini cha mshahara. Hivi kweli kupanga kima cha chini cha mshahara tunahitaji wataalamu kutoka nje ili waje watupangie. Mimi ninastaajabu ikiwa hata kima cha chini cha mshahara tunahitaji wataalamu waje watupangie ni tatizo *it is a symptom*, ni tatizo kwamba sisi hatuna uwezo, kwa sababu ni lazima uweke vigezo. Kima cha chini cha mshahara kinapangwa kwa vigezo, unampa kima cha chini cha mshahara mtu huyu ni tunza tu kwa kazi aliyoifanya au unampa pesa zile akajikimu na wanawe.

Mhe. Spika, kwa mfano, Shs. 100,000/= iliyopo sasa hivi, *average* ya Shs. 3,000/= kwa siku. Wizara hiyo hiyo ya kamisheni ikifanya semina, *package* iliomo katika kibati kile ni zaidi ya 3,000 kila kinachoitwa *container*, leo kuna jina jipya limetoka hapa kwa Mhe. Waziri, kifurushi au sijui kifungamanishio. Kwa hivyo, niliuliza nikaambiwa ndio ile *container*, sijui kama ni sawa. Ile *container* ukiingiza vile vitu 3,000 zimeshapita. Leo unampa mfanyakazi ambaye ana mke na watoto wanne au watano.

Kwa hivyo, mimi nafikiria tungekuwa *more serious* kuangalia, je huu mshahara wa chini tunampa kwa njia gani au kwa sababu gani. kwa sababu ya tunza yake ya kuja kazini wakirudi au tunampa kwa sababu ndio jasho lake. Yule mfanyakazi tumfikirie kwamba akimwita fundi muashi basi atamlipa kwa kijio chake, akimuita fundi umeme atamlipa kwa kijio chake na akimuita fundi yeyote basi fundi atafanya hesabu kwa mujibu wa anavyotumia nyumbani. Sasa sisi tuko radhi kumlipa mfanyakazi kwa shilingi laki moja, halafu yeye akiwaita watu wengine kumsaidia kazi nyumbani kwake awalipe zaidi ya kile. Mhe. Spika, nakushukuru sana. Napenda nimalizie kwa kuunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Ali Abdallah Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto asubuhi hii.

Pili nimpongeze Mhe. Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote kwa kuweza kuwasilisha hotuba mzuri, iko wazi na imefahamika na mimi sikuwa na mashaka mengi katika hotuba hii, nia yangu ni kuunga mkono, lakini niseme japo maneno mawili au matatu. Kwa hivyo, nina masuala yangu manne niyawasilishe kwa Mhe. Waziri ili na mimi baadae niunge mkono.

Mhe. Spika, nikianza katika hotuba nije kwenye ukurasa wa tatu Kamisheni ya Kazi. Kamisheni ya Kazi imeelezwa hapa naomba kidogo ninukuu, halafu baadae nizungumze hayo niliyokusudia, inasema kwamba

"Kamisheni ya Kazi ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria katika kazi, katika sekta za umma, sekta binafsi nchini". Namalizia kule mwisho. "kughuhulikia suala zima la ajira pamoja na utoaji elimu kwa waajiri na waajiriwa na jamii kwa jumla".

Mhe. Spika, tunashukuru kwamba hii ni kazi nzuri na wenzetu wanawajibika siku zote katika kutekeleza haya na kuyasimamia. Katika kuwasimamia watu kuna matatizo yake na changamoto zake. Kwenye malengo yao wanayomalizia ya mwaka 2009/2010 wameeleza kuna mambo ambayo wanayafuatilia, hivyo na mimi nilikuwa niulize maswali machache katika suala hili.

Mhe. Spika, katika ukurasa unaofuata wa 24, kuna malengo pale matano ambayo walikusudia katika kipindi kilichopita wayatekeleze na mwaka huu wameweka malengo mengine, mengine yamerudiwa lakini mengine yamefanyiwa kazi.

Mhe. Spika, katika lengo la kwanza linasema kutekeleza sera ya ajira, mipango kukuza ajira, mpango wa kudhibiti ajira ya watoto na kanuni za kazi. Mhe. Spika, tunashukuru kwamba hili wamelifanyia kazi, lakini hatujajua ni kwa kipimo gani. kwa sababu katika hotuba hakuna pahala paliposema kwamba tumefikia asilimia fulani katika utekelezaji. Lakini tunashukuru kwamba wananchi wengi sasa hivi ajira za watoto zimepungua, lakini bado zipo. Yako maeneo maalum, ningemuomba Mhe. Waziri wakazidi kuyasimamia yanaweza yakasaidia kuweza kuondosha ajira hizi.

Kwanza kwenye zile sehemu zote ambazo ni za Kaskazini mwa visiwa vyetu, ajira hizi zinakuwa ni kubwa kwa sababu kule bado wenzetu wako katika hali duni na taaluma pia inachelewa kuwafikia. Ningeomba kwenye sehemu hizi wakazifanyia kazi zaidi. Pia sehemu za mkusanyiko wa watu.

Kwa mfano, Kwerekwe, sehemu za kugeesha magari. Utakuta vijana wanapewa vitu vidogo vidogo wanauza kama maandazi, wengine wananyonyoa kuku na shughuli nyengine. Sasa maeneo haya yote yangedhibitiwa na kutolewa taaluma kwa kutumia mbinu mbali mbali. Kama vipeperushi na ushauri nasaha, nadhani ingesaidia kupunguza hizi kazi za watoto wale ambao waliobakia. Ziko kazi za watoto kuwasaidia wazee sio mbaya.

Kwa mfano kama kenda skuli karudi, jioni kapewa kitu kidogo hivi angalau watafute hata mafuta ya taa, ile sio mbaya. Lakini kuna wengine hata skuli hawaendi. Kwa hivyo, nadhani hawa tungewafanyia kazi zaidi ili tukaweza kujua. Hata kwenye bajeti inayofuata tukijaaliwa ukatupa taarifa kwamba je ajira hii ilikuwa ni kiasi fulani kwa mwaka uliopita na mwaka huu tumefikia asilimia fulani, basi tungejua kwamba tunakwenda mbele ama tunapunguza. Kwa hivi ilivyokaa hatuwezi kufahamu imefikia hatua gani.

Mhe. Spika, suala la pili, katika malengo yao ya kipindi kilichopita, lengo la tatu, naomba ninukuu, wanasema "Kuimarisha kitengo cha usuluhishi wa migogoro katika kazi na mengineyo", lakini yangu mimi ni hapa. Nadhani na hili vile vile halikuwekwa wazi kwamba hiyo migogoro pengine ni mingapi kwa kipindi hiki ilikuwepo na imetatuliwa mingapi. Kwa sababu mimi hivi sasa katika jimbo langu kuna mgogoro wa muda mrefu na tayari barua zimepelekwa kamisheni ya kazi, tuna hoteli za mwanzo mwanzo pale za wazalendo inaitwa Mawimbini Chuini. Pale kuna wananchi sasa hivi huu mwezi wa sita, tajiri hawamjui yuko wapi na watu kuondoka makazini hawawezi. Kwa sababu katika hoteli wenyewe wamekuwa kama wamehama, lakini muna vitu mule vya thamani na mtu akisema atoroke vikiibiwa atakamatwa yeye na huu ni mwezi wa sita lakini tajiri hawamjui, kazi wanafanya na malipo hawajapata. Barua hizo zipo na nakala nimepewa, bahati nzuri sikuisahau, hivyo nikitoka nje nitamkabidhi hiyo nakala na mimi nasaidia hili kama ni mwakilishi wao .

Kwa hivyo, Mhe. Spika, bado matatizo yapo. Mhe. Waziri kama unayo takwimu kidogo basi unaweza kutuambia kwenye majumuisho kuwa katika kipindi cha mwaka huu misuluhisho hiyo ilikuwa ni 18, lakini 9 tumeshaimaliza na iliyobakia tunaifanyia kazi na sisi tuweze kujua kwamba kweli hatua zinachukuliwa, lakini kwa hivi ilivyokaa hatuwezi kujua ni hatua gani imefikiwa.

Mhe. Spika, la kuongezea vile vile katika haya mambo ya usimamizi wa ajira, hivi sasa kumezuka mtindo kwa wenzetu wengi wageni wanakuja kwa njia mbali mbali na akishafika anakodi mkahawa, ana usimamia yeye halafu anauza, huyo ni mgeni kutoka nje ndio kaja kuwekeza. Sasa na haya mambo madogo madogo tungeyatizama tukawanyang'anya na kuwaachia wenyewe wazalendo, lakini leo mtu anatoka nje anakuja hapa anauza mkahawa. Sio

jambo zuri na wala halipendezi wakati mikahawa tuuze wenyewe watu wa kawaida yaani wazalendo. Au mtu kajenga kijumba chake kimoja chenye vyumba sita anakuja kukikodi mgeni na kukiendesha yeye.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nadhani mkae pamoja na watu wa ZIPA na muangalie ni miradi gani ya mzalendo na miradi gani ya mtu kutoka nje. Haya mambo yapo na hivi sasa yanaleta ugomvi mkubwa. Mkienda katika sehemu nyingi za Ukanda wa Kaskazini Mashariki huko, basi mtakuta mambo hayo yapo. Mtu kijumba kapata pesa kidogo kajenga kisha anaendesha rizki, halafu anakuja mgeni anakikodi yeye tena anakikodisha kwa pesa za kigeni, halafu inakuwa wewe hupati kitu. Kwa hivyo, kama wenzetu wanataka kuekeza basi waje wawekeze kwenye mahoteli makubwa.

Mfano hoteli ya nyota tano, nyota nne, au nyota tatu, lakini leo mtu anakuja kwenye nyumba ya vyumba sita anakodi yeye halafu anaendesha biashara. Kwa hivyo, nadhani muwe mnaelewana baina wizara mbili na kipi kinaweza kikasaidia.

Mhe. Spika, nije kwenye *point* yangu moja ambayo kaichukua mwenzangu, lakini kwa vile nilitia nia niizungumze basi ni lazima niiseme. Ni juu ya suala zima la kushauri bodi juu ya utaratibu wa mishahara ya wafanyakazi wa chini. Mhe. Spika, nadhani sio vibaya kukiwa na kitu kama hiki na kikaweza kutusaidia, kwa sababu tayari serikali imefanya tafiti sana katika koo mbali mbali, kuanzia kwenye shehia na kujua matatizo ya wananchi wetu kwa hali waliyo. Sasa takwimu kama zile zikipatikana, wakapewa kwenye bodi basi wanaweza kuona ni kitu gani kifanyike ili waweza kuishi kwa matumaini. Kwa sababu hivi sasa utakuta familia nyingi zilizokuwa maskini, basi mtu analipwa mshahara wa Shs.100,000/= kwa mwezi, lakini Shs.100,000/= ukiigawa kwa siku unapata Shs.3,000/= na kidogo. Binadamu anatakiwa ale milo mitatu, asubuhi, mchana na jioni. Sasa igawe Shs.3,000/= kwa milo mitatu na milo inapitana wa asubuhi wa mchana na wa jioni. Utakuta pengine akifanya hesabu ya mlo hasa basi atakula mlo mmoja wa mchana tu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunashauri na hili lingeangaliwa ili tukatoka angalau kwa hapa tulipo na tukasogea mbele, japo kuwa nchi yetu ni changa, lakini tuwatizame na wale wananchi wetu kwa sababu ndio wanatupa nguvu zao katika serikali, basi tungesogea mpala Shs.150,000/= ili mtu akaweza kupata milo mitatu ya uhakika kidogo, tena mingi iliyobakia atatafuta mwenyewe kwa mbinu zake. Atalima muhogo akauze au atalima migomba. Lakini mshahara wa Shs.100,000/= bado ni mgumu sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kama utaratibu upo kweli wa kuishauri bodi ili kutengeneza mishahara mpya kwa wafanyakazi wa chini itakuwa ni jambo la busara.

Mhe. Spika, nikienda kwenye hoja yangu ya pili nije kwenye ukurasa wa 58, kuhusu Idara ya Mfuko wa Kujitegemea. Kwenye sehemu hii nije kwenye malengo yaliyopita katika nambari 2, naomba ninukuu, “kusimamia utaratibu wa mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi wa JK na AK”.

Mhe. Spika, nadhni mfuko ni mzuri na malengo ni mazuri, lakini tunachokosana na wananchi hivi sasa ni kuwa, kwanza *speed* yake ndogo hata ikaweza kuwafikia hawa wananchi wenyewe hiyo mikopo, lakini na taaluma bado ingezidi kutolewa katika shehia mbali mbali. Wananchi walivyosikia hivyo walitegemea kwamba mtu kama ataandika mradi wake. Mfano mimi nataka kufuga kuku 400 banda nitajenga kiasi fulani, kuku nitachukua kwa muda wa miezi sita au miezi mitano nitaanza kuzalisha kwa mpangilio mzuri, mtu kama yule anaambiwa huwezi kupata mkopo huu, kwa sababu huna biashara au huna mradi. Inatakiwa kama kuku basi uwe na mabanda na kuku uwe nao tayari. Sasa kwa njia hii hatuwezi kuwasaidia, tutakuwa tunawaongezea wale wale walichonacho wazidi kutononoka zaidi, na yule wa chini tutamuacha pale pale.

Kwa hivyo, mimi ningeshauri kwamba kama wako wataalamu na mtu kaandikiwa mradi mzuri na unakubalika kimahesabu na kitaalamu basi mtu kama yule mkopo pia apewe. Lakini mtu hana kitu halafu anaambiwa mkopo unakuja kuwasaidia watu kuwawezesha kiuchumi, kuwapunguzia umaskini lakini mpaka aanze mradi pesa hiyo ataitoa wapi. Sasa nadhani na kidogo tubadilishe utaratibu ili lile lengo lililokusudiwa na viongozi wetu liweze kuwafikia wananchi ili haya matatizo ya umaskini yapunguwe. Kwa hivyo, nashauri Mhe. Waziri wataalamu kama wapo basi wananchi waandikiwe miradi na halafu wakopeshwe fedha ili waweze kufanya biashara hizo.

Mhe. Spika, nikiendelea na hoja yangu ya tatu nije katika ukurasa wa 33 kifungu cha 47(6) kuhusu Idara ya Maendeleo ya Vijana. Idara hii ina malengo manane imejipangia. Mimi nitazungumzia malengo mawili tu katika hayo ya kipindi kilichopita, wanasema

Kifungu cha 47(6)

> “Kuanzisha kituo cha majaribio cha miradi ya kiuchumi ya vijana kwa hapa Unguja”.

Mhe. Spika, ni lengo zuri na linaweza likawasaidia vijana wengi waliokuwa hawana kazi, wakaweza kuelimika na kuweza kujiajiri. Lakini sikuona katika maendeleo ya huko mbele kwamba kituo hiki tayari kimeanza kazi ama kimejengwa au kiko pahala gani. sasa ningemuomba Mhe. Waziri kama utekelezaji wake kwa kipindi kilichopita kimefanikiwa basi angeniambia kituo hiki kiko pahala fulani na tayari tumeshatoa pengine mafunzo kwa vijana kiasi

fulani, ili tuweze kujua kama na mimi ninao katika jimbo langu, niwapeleke ili wakapate taaluma na waweze kujiajiri wenyewe.

Mhe. Spika, jengine katika hilo ni lengo la nambari 8, naomba ninukuu, kinasema

Kifungu cha 47(8)

> "Kuandaa na kutekeleza mpango wa malezi kwa vijana kwa kutoa mafunzo ya ushauri nasaha, stadi za maisha, afya ya uzazi, vita dhidi ya UKIMWI na madawa ya kulevya".

Mhe. Spika, hili sio jambo baya kwa sababu vijana wetu ndio waridhi wa nchi hii na viongozi wa baadae. Lakini taaluma hizi zinatolewa maeneo gani, mashuleni, mitaani au vigengeni. Mhe. Spika, ningependa kujua ni maeneo gani ambayo yanafanyiwa kazi hii ili tukaweza kujua na sisi kama tunayo maeneo hayo tukawaita wataalamu wakatusaidia.

Mhe. Spika, la mwisho katika uchangiaji wangu, nije kwenye viambatanisho. Kiko kiambatanisho kwenye ukurasa wa 90, kiambatanisho nambari 13 kuhusu mfuko wa kujitegemea Zanzibar na utoaji wa mikopo kimikoa. Hapa kwenye kiambatanisho hiki kaonesha mikoa yote ambayo imepata hii mikopo yenyewe, lakini mimi ningemshauri Mhe. Waziri hapa katubana sana angekuwa muazi, angesama kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi, Wilaya ya Magharibi, Wilaya ya Mjini anatuonesha ni vikundi fulani na jimbo fulani unapata kujua. Kwa hapa katuweka jumla jumla, sasa hatujui nani kapata na nani kakosa.

Mhe. Spika, mimi niko Mjini Magharibi, lakini sina kitu mpaka sasa hivi, lakini kanichanganya. Sasa bora angetueleza kwa huyu kapata na huyu kakosa ili tujijuwe, kwa hivi anatuchanganya kwenye kundi wala hatumo. Sasa namshauri Mhe. Waziri katika kuandika mambo kama haya awe muwazi zaidi. Mfano Wilaya ya Magharibi Chukwani, Kiembesamaki, Maungano, Dole basi tunajua alaa wenzangu wameshapata, na sisi labda kuna mbinu tufanye ili tupate. Kwa hivi kaweka vizuri lakini naomba wakati mwengine akiandika kitabu chake basi awe muazi zaidi ili tuweze kujua, mimi kwa kweli sijapata kitu.

La mwisho la kumalizia Mhe. Spika, tuje kwenye sheria ya mtoto, ambapo mimi nilibahatika Bwawani kwa siku mbili na tumetoa na sisi maelezo mengi ya kuweza kuisaidia. Nashauri kwamba bado jamii ishirikishwe zaidi katika suala hili kabla haijafika kwenye vyombo vyetu ambavyo tunaipitisha. Kwa sababu bado malalamiko kwa wananchi bado ni mengi na sisi tuko kwenye jamii, Misikitini yanasemwa. Kwa hivyo, nashauri kwamba bado sheria irudi kwa wadau ili waweze kuichangia, hatimaye ikifika kwenye chombo chetu iwe hakuna malalamiko kwa wananchi wetu. Huo ni ushauri wangu Mhe. Spika.

Kwa kumalizia mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini, nimetoa mchango wangu na sasa hivi natamka kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha leo hii tuko hai na salama. Vile vile nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto, Mhe. Asha Abdalla Juma.

Mhe. Spika, pamoja na kitabu hiki kizuri, Mhe. Waziri, Katibu Mkuu wake, wakurugenzi na maafisa wake nao tunawapa shukrani kubwa sana kwa kupoteza muda wao, ili kuweza kutuletea kitabu hiki chenye maudhui mazuri na mipangilio mizuri.

Mhe. Spika, kawaida yangu huwa nachukua dakika 30. Lakini kutokana na hali ya uzuri wa kitabu hiki basi nitajaribu kuchukua dakika chache sana mheshimiwa, ili na wenzangu niwape nafasi waweze kufaidika. Hasa ilivyokuwa yeye mwenyewe Mhe. Waziri alisoma hotuba yake kwa muda mchache sana, tunampongeza sana.

Mhe. Spika, naingia kwenye ukurasa wa 23 moja kwa moja katika hii kamisheni ya kazi. Mhe. Spika, hatuna haja ya kutaka kurudia, lakini kuna mambo Mhe. Spika, ni lazima tuyatilie mkazo ili Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wazidi na wao kuelewa umuhimu wao katika kutukazia sisi katika idara hii.

Mhe. Spika, mimi nina ukanda huo wa mahoteli kwenye Jibo la Kitope, tunayaona matatizo ya kila leo na kila siku kukicha yanaendelea tu. Sasa Mhe. Spika, kama hatukusema na tukasisitiza kwa kweli itakuwa ni suala ambalo halitokuwa na busara, hatupendi sisi bajeti hii tuirudie, lakini inabidi tunarudia kutokana na hali ilivyo.

Mhe. Spika, juzi mimi nimeitwa katika Kijiji cha Kiwengwa, kuna kamati ya maendeleo. Kamati ya maendeleo hiyo kazi yake ni kuratibu mambo ambayo huwa karibu na mahoteli na kuwapatia ajira wananchi wake katika ile sehemu ya kijiji. Kwa bahati nzuri huko nyuma alikuwepo Mhe. Waziri Kiongozi, tulikwenda naye katika hoteli hiyo na tukakubaliana naye vizuri, kisha akatoa muongozo mzuri na akatushirikisha idara zote husika. Wakiwemo wenyewe utalii, idara ya kazi wapo hapo na wengine.

Mhe. Spika, sasa hivi wakati wa ajira tayari na wale ndugu zetu kila inapofika wakati wa ajira, wale wenye mahoteli ndio wanapokuwa wanaume ni wao, basi hapo mheshimiwa ndio yanapotokea mambo mengi machafu kama rushwa na

rushwa ya mwili hapo ndio inaanza kutawala. Kwa kweli Mhe. Spika, Mhe. Waziri nataka nimuambie hatujaweza kulifikia kwa asilimia kubwa, kwa sababu tunao watu kwenye mahoteli wanafanya vitendo hivyo na wanasemwa kila leo, hatimaye utamkuta mtu yule anaendelea kuwepo kwenye sehemu ile.

Sasa hili suala Mhe. Spika, hata na sisi tunavunjika moyo wawakilishi, kwa sababu hatusemi kitu cha kubahatisha. Mimi siku zote nasema kama nabahatisha basi anifungulie mashtaka mtu, kwa sababu lile suala tunalosema ni la kweli na lipo. Ubaya wake ni mmoja tu, ukimuendea yule mama wewe vipi. Aah! Mimi naogopa kusema. Sasa unaogopa kusema hiyo haki yako utaipata wapi. Nalo suala hili Mhe. Waziri hebu awaelimishe akina mama. Mimi nashangaa sana Mhe. Spika, waziri mwenyewe alivyokuwa *strong*, humjui kama ni mwanamke, humjui kama ni mwanamme. Lakini hao wengine sijui kwa nini wanashindwa kufuata tabia zake yeye, mimi hapa kinanishangaza kweli

Mhe. Spika: Waziri ni mwanamke.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ehee! Sasa ule ujasiri wake Mhe. Spika, ndio unaoondoa tofauti kutokana na alivyokazana.

Sasa suala hili Mhe. Spika, mimi naishukuru sana idara inafanyakazi, sio kama haifanyikazi. Narudia waheshimiwa wenzangu wanavyosema kwamba labda vitendea kazi hawana, hiki kitu nakisema. Vitendea kazi na maafisa wako kidogo, hili nakubaliana nalo. Kwa sababu leo utakuta afisa wawili tu ambao tunawaona machoni kila leo wanazunguka hao hao. Kwa kweli ukanda ule ni mkubwa sana. Sio ule tu wa Kiwengwa. Hata na jirani yangu Pwani Mchangani, Nungwi. Halikadhalika sehemu za Kusini wako wengi, lakini sasa utakuta maafisa wale ni kidogo. Kwa hivyo, tunaomba maafisa kwanza waongezwe, halafu na vitendea kazi pia waongezwe jamani, vile vihonda wanavyopanda ni vibovu, suala hili tuseme ukweli, wanashindwa kufanya kazi kutokana na wakati ulivyo.

Mhe. Spika, sasa hivi ni wakati wa ajira kama tulivyosema, watandae sasa hivi wawepo mule katika maafisi kuangalia. Kwanza mikataba wanapewa ya uongo. Tulisema mikataba iwe kwa lugha yetu ya Kizanzibari, wengi lugha bwana ni Kiswahili. Sasa iangaliwe na ipitiwe ili itengenezwe ya Kiswahili, wasitengenezewe ya Kizungu, kwa sababu Kizungu wanawabana wale, hata wakija kufahamishwa basi wameshateketea.

Halafu utakuta kwenye mikataba ya *supplier* hawa watu wa kazi hebu wakae na wao ili wawasaidie, wanaonewa kusema ukweli na wanashindwa kufanya mikataba hawajui taaluma ile ya kufunga nao mikataba. Wanafunga mikataba hivi kiholela holela kwa kuwa mtu anaona anapata ajira, basi anaona mimi

nikubali hivyo hivyo. Kumbe baadae yakitokea matatizo sheria inakuwa haimlindi yeye. Kwa hivyo, suala hili tunaomba Mhe. Spika, Mhe Waziri aliangalie hili kwa maafisa wake. Sasa hivi tujikite kabisa, la kama si hivyo kwa sababu sasa hivi ajira za wageni zimekuwa nyingi kuliko wazaliwa wenyewe.

Mhe. Spika, utakuta leo mtu anaambiwa ni *export*, wakati *export* yule Mzanzibari ameshasoma na amefundishwa taaluma ile ile. Sasa ile dhana ya kusema tunafungua milango ya kuwekeza, sasa inakuwa sisi tunajiezeka sisi maana hatufaidiki nayo. Kwa hivyo, hebu tuangalie vizuri.

Halafu jengine Mhe. Spika, hebu Mhe. Waziri kubalianeni kati ya *migration* na hawa kamisheni ya kazi. Kwa sababu kuna mambo haya yanakuwa yanatofautiana. Kwa mfano, kamisheni ya kazi inatoa kibali pengine cha miezi mitatu au minne, lakini utakuta mtu yule ameshamaliza kule *migration* wanataka kutoa yao, ili wamuhalalishe yule aweze kukaa. Haya mambo hebu kidogo tunaona yanakwenda tofauti. Kwa sababu kuna tatizo limejitokeza. Kamisheni imekubali yule mtu afanyekazi nchini, lakini *migration* imekataa. Tunaathirika sasa hivi kuna viwanda viko kule vya uwekezaji vinaharibika bure kutokana na kutokuelewana tu. Hebu namuomba kamishna hili suala alifuatilie, kuna tatizo gani, hawasemi.

Mhe. Spika, ukiwauliza nyinyi mnatatizo gani kwa nini hamtoi vibali. Wanajibu tunajua sisi wenyewe. Sasa mnajua nyinyi wenyewe mpaka lini itafika hali hiyo. Kwa hivyo suala hilo naomba Mhe. Waziri kamishna akae na wale watu wa *migration*, ili kuweza kulitatua hilo suala, mtu akimaliza miaka mitatu na aende zake bwana, hakuna kuweka tena hapa.

Mhe. Spika, nije kwenye suala hili la mbio za mwenge. Mhe. Spika, hapa kidogo naomba niulize. Kila siku kukicha wenzetu Bara wakimbizaji mbio wanakuwa wengi, lakini sisi tunakuwa kidogo katika ukurasa huu wa 41, hebu Mhe. Waziri kulikoni ni nini. Kama mara hii tuna Wazanzibari wawili tu, waliobakia wote ni kutoka Bara huko. Sasa hebu tuliangalie ni tatizo gani. Kwa nini tusiweke uwiano mmoja, wale watatu na sisi watatu mchezo ukaisha. Hili suala hebu tulitizame Mhe. Waziri ili liweze kutusaidia.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, naingia katika suala la kusimamia masuala ya uratibu wa mfuko wa uwezeshaji wa wananchi wa kiuchumi JK na AK. Hili Mhe. Waziri nakupa sifa sana hapa. Mmesimamia vizuri, na idadi inaendelea kuwa nzuri, lakini ucheleweshaji sasa bado upo. Litilie mkazo hili Mhe Waziri ili hii sehemu iliyobakia angalau na sisi tunaogombea kwenye majimbo tupate kurudi na wananchi waone jinsi gani ambavyo tunasimamia katika mfuko huu.
Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana kabla hatujamaliza muda wetu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba mimi sitokuwa na hoja nyingi sana kuhusu wizara hii. Kwa hivyo, ninaunga mkono kwa asilimia mia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope. *(Makofi)* Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuchangia machache sana pamoja na kutoa ufafanuzi kwamba waziri wa wizara hii ni mwanamke, licha ya ukakamavu wake lakini ni mwanamke. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze mchango katika ukurasa wa 17 kwenye ibara ya 25. Katika ibara hii Mhe. Waziri anatuelezea juu ya Kituo cha Kutoa Taarifa kwa Waomba Kazi na Wajasiriamali na pia natufahamisha kwamba tayari kituo kimeshajengwa kazi imeshamalizika pamoja na vifaa.

Kwa hivyo, hapa ninayo maswali mengi ambayo nataka kumuuliza Mhe. Waziri. Kwanza kituo hiki kama tunavyoambiwa kwamba kitakuwa kikitoa habari za watu wanaoomba kazi na sisi Wawakilishi mara nyingi tunapiga kelele kuwa hatutaki wataalamu wetu watutoke na kwenda nje. Lakini kituo hiki kina-*entertain* watu wakaombe kazi nje.

Sasa sijui kama tunao wafanyakazi wa ziada katika nchi yetu na kusema wengine waende nje kwa ajili ya kuomba kazi, kwa sababu bajeti zote tunazojadili hapa suala linalojitokeza ni upungufu wa wafanyakazi. Kwa mfano, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mali, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wizara hizi ninakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi na kwa ujumla hakuna wizara hata moja ambayo haina upungufu wa wataalamu.

Mhe. Spika, leo tunaanzisha kituo hiki kwa ajili ya kuwapa fursa vijana kutafuta kazi kwa kupitia kituo hiki. Sasa mimi hofu yangu je, kwa kupitia kituo hiki huoni kwamba tutatoa fursa kwa vijana waihame nchi yao wakati tunahitaji wataalamu. Hilo la kwanza.

Vile vile kituo hiki tunaambiwa kwamba vijana watapata fursa ya kutangaza pamoja na kuuza bidhaa zao kwa kutumia mtandao. Mhe. Spika, tunao ushahidi wa kutosha kwa watu wengi waliotapeliwa kwa biashara za mitandao hapa Zanzibar. Kwa kweli watu wengi wamefukarika pamoja na kuingia maradhi kutokana na biashara hizi za mitandao.

Sasa sijui wizara yake imejipanga vipi na uharamia huu. Kwa mfano, hivi sasa unaweza kufungua mtandao na kuona kazi zinatangazwa na kuambiwa lete dola 1,000/- na kufanyiwa mambo yote, kwa kweli kesi hizo hapa Zanzibar zipo nyingi sana.

Mhe. Spika, ndani ya Baraza hili tukufu wamo watu watoto wako wameshafikwa na kadhia hiyo. Lakini dakika ya mwisho unakuta ule mtandao unafungwa na hata ukitafuta mawasiliano haupo tena, nadhani tunataka kuwapeleka vijana wetu huko.

Kwa hivyo, nafiriki suala hili tulichukue kwa tahadhari kubwa, kwa sababu hivi sasa kuna mitandao mingi ya uongo duniani kuhusu masuala ya kazi na ipo mingine ya kweli. Kwa mfano, tukiangalia Uingereza kuna mitandao inayotafuta kazi hasa Kada ya Afya, yaani ipo ya kweli na kama mtu anao uwezo basi anaweza kuomba.

Mhe. Spika, hofu yangu ni vijana tutakapowaingiza kwenye mambo hayo, nina hofu mbili kwanza wataalamu kututoka ambao tunao wachache, lakini hofu ya pili kwamba vijana wetu tukajakukumbana na mabingwa wa kutapeli watu na vijana wetu kutapeliwa na ikawa hakuna ajira yoyote na ikawa mtihani. Sasa nadhani hilo wizara ilichukue kwa tahadhari kubwa sana.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumze ambalo liko kwenye ukurasa wa 28 lenye kuhusu Kamisheni ya Kazi kushiriki katika majadiliano ya Soko la Pamoja. Mhe. Spika, Wazanzibari kama wenzetu kaka zetu wa damu Watanzania tunalikaribisha kwa woga Soko la Jumuia ya Afrika ya Mashariki, kwa nini nikasema tunalikaribisha kwa woga. Tunalikaribisha kwa woga kwa sababu wenzetu *quality* ya elimu yao iko juu na lazima tukubali Mhe. Spika.

Kwa mfano, tumchukue kijana aliyemaliza *Form IV* Kenya umuweke na umuweke na kijana wetu aliyemaliza *SUZA*, katika suala la kujieleza huyu aliyemaliza *SUZA* ataangushwa chini na kugaragazwa hasa, kwa sababu wenzetu *quality* ya elimu ya ni nzuri.

Sasa mtu anapotangaza kazi jambo la mwanzo atakalofanya ni *interview* kuna masuala ya kujieleza, inawezekana mtu ni mtaalamu mzuri, lakini kijieleza hawezi. Kwa hivyo, mwenye fursa ya kujieleza mara nyingi kwenye *interview* ndiye mwenye kufanikiwa zaidi.

Mhe. Spika, ni vyema kamisheni imeshiriki kwenye majadiliano hayo bila ya shaka kwa kupitia mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano. Lakini nasema sisi Wazanzibari hivi tumeshafanya *research* na kuona faida na hasara katika soko hili kuhusiana na masuala ya ajira, hata katika suala la uwekezaji. Kwa kweli kuna suala la ajira moja na pia kuna suala la uwekezaji wa rasilimali. Hivi kuna Wazanzibari wangapi wenye uwezo wa kwenda Kenya au Uganda kwa ajili ya ku-*invest* na haya ndio masuala ambayo wengi tunajiuliza.

Mhe. Spika, tunajua kwamba wapo Waganda pamoja na Wakenya wengi wenye uwezo wa ku-*invest*. Vile vile wapo Waganda pamoja na Wakenya

wengi wenye elimu na kuweza kuja hapa na kupata kazi. Sasa kwa upande wetu huwa tunajiuliza maswali kama haya. Kwa hivyo, nadhani ni changamoto, lakini Mhe. Waziri anaweza kutujibu kwa vile walivyojiandaa.

Sasa nataka nirudi nyuma kidogo kwenye kitabu chake katika ukurasa wa 6. Mhe. Spika, katika ukurasa huo ambao ni muendelezo wa malengo makuu ya wizara, yaani yameanzia ukurasa wa 4, 5 mpaka wa 6 ibara ya 7 (7) naomba kunukuu.

Kifungu cha 7 (7) kinasema hivi:-

> "Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa, Sera, Sheria na Programu zinazowalenga wanawake na watoto, vijana, waajiri na waajiriwa.

Mhe. Spika, tukiangalia siku hizi *development* katika masuala ya Mikataba ya Kimataifa hasa inayohusu Sheria za Mambo ya Watoto pamoja na Vijana, kwa kweli zina matatizo kidogo. Kwa hivyo, hivi sasa ulimwengu umeingia kwenye u-*liberally*, yaani umetawala sana dunia, kwa sababu kwa wenzetu hizi sheria za kuoa watu wa jinsia moja zinapigiwa kelele sana nina hakika siku moja litakuwa ni Sheria za Kimataifa. Kwa kweli hivi inaonekana ulimwengu mzima ndio wimbo na sisi Tanzania tunaridhia mikataba mingi ya kimataifa.

Mhe. Spika, pamoja na kuridhia Mikataba ya Mikataifa, lakini tusijetukaacha na kuridhia maadili yetu ya nchi, kuridhia mikataba ya kimataifa bila ya kuridhia sila zetu za nchi itatufikisha pabaya. Kwa mfano, katika Ijumaa mbili zilizopita tulisali Sala ya Ijumaa katika Msikiti wa Welesi (maarufu Msikiti Udi). Kwa hivyo, tulisikia Hotuba ya Khatibu anavyoonesha wasi wasi kuhusu Sheria ya Mtoto inayotaka kuletwa na kumbe haiko msikiti mmoja karibu misikiti yote na alizungumza Mjumbe mwenzangu mmoja.

Kwa kweli watu wanavilio na wala hawaridhiki na zile sheria ambazo zinawabana wazee, yaani mtoto hivi sasa atakuwa nalelewa kama vile anavyolelewa London na Washington na itakuwa mzee hana kauli tena juu ya mtoto wake. Mhe. Spika, watu wanasema tukiangalia vitabu vyetu vya dini haviko hivyo, zile sheria zinakuwa za kilimwengu lakini tukiangalia kwa upande wa dini inapingana.

Kwa hivyo, ushauri wangu Mhe. Spika kwa Mhe. Waziri awe na wanasheria wazuri katika wizara yake kwa ajili ya kuangalia sana hii Mikataba ya Kimataifa ambayo tunairidhia, kwanza kabla ya kuiridhia haidhuru sio sisi tunayoiridhia na wanaoridhia ni wenzetu wa Tanzania Bara na kwetu sisi inakuja kama tunafuata shangwe.

Lakini pamoja na kufuata shangwe tunapochoka basi unarudi kwenu. Kwa mfano, shangwe linaweza kutoka Jang'ombe na ukifika mjini na kuona umeshachoka basi ukasema huku sendi tena na kukata shangwe na kurudi nyumbani.

Sasa nadhani na sisi katika kufuata hii Mikataba ya Kimataifa tufanye kama hawa watu wanaofuata shangwe, yaani tufuate na tukifika pahala tukiona tumeshachoka basi tusimame njiani na kurudi nyumbani. Kwa hiyo, tusifuate kwa asilimia mia moja itakuja kutuletea matatizo na kuleta migongano ya kijamii.

Mhe. Spika, hakuna kitu ambacho kinachokiogopa kama hizi *social dynamism* katika nchi za kila siku, kwa sababu hizi baadaye zinajikusanya na kuibuka nchi inafika pahala pabaya sana.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze kwa uchache sana kwa sababu muda ni mfupi ni kuhusu suala la utatu. Kwa kweli utatu upo nakubali, lakini ni kinadharia zaidi, kwa sababu najua kuna Serikali, Chama cha Waajiri na Chama cha Wafanyakazi, mfumo huu hapa Zanzibar haufanyikazi vizuri.

Kwa mfano, Chama cha Wafanyakazi sisi kwa bahati nzuri katika ziara zetu za kamati tunaonana nao, tunapokwenda wanasikitika tu, sasa unapomuona mtu anasikitia anakuwa mnyonge, kwa hiyo huyu anakosa kushirikishwa vizuri katika masuala mbali mbali.

Kwa kweli mara nyingi tunavichukulia Vyama vya Wafanyakazi kama ni wakosoaji au wapinzani au *Pressure Groups*, yaani mara nyingi tunakuwa tunaviangalia kwa jicho la kushoto. Mhe. Spika, nadhani tuachane na tabia hii kwa sababu hawa ni watu muhimu sana.

Lakini hata Chama cha Waajiri tumekwenda wakati tulipopekea maelezo, yaani tuliona hata hawa wawekezaji wakija hapa nchini serikali haioneshi umuhimu kwa waajiri, yaani wawekezaji kujiunga na kile Chama cha Waajiri. Sasa serikali inaona fahari zaidi wale waajiri kuwa na *communication* moja kwa moja na wizara kuliko kupitia kile Chama cha Waajiri.

Mhe. Spika, nafikiri serikali ingebadili mfumo wake na kulazimisha hasa kwa hawa waajiri, ambao wanaokuja kuwekeza wawe wanachama cha Chama cha Waajiri. Sasa serikali badala ya ku-*negotiate* na mwekezaji mmoja mmoja ikawa ina-*negotiate* kupitia kile Chama cha Waajiri, nafikiri ingekuwa ni jambo zuri. Lakini serikali inakuwa na mfumo kama huo wa kutoka kwa mwekezaji moja kwa moja na kwenda kwa waziri wakati Chama cha Waajiri kipo.

Nadhani ni vyema tungekiimarisha kile chama chetu pamoja na kujenga heshima ya waziri kuonana na watu ambao hapaswi hata kuonana nao na wengine ni watu wadogo tu, *just* mtu kwenda na kuonana nao na kumaliza mambo yao. Lakini japo mtu mdogo utamkuta na *briefcase* yake anakwenda kwa waziri, sasa wanatuona hawa watu vipi, kumbe yule hapaswi hata kumuona waziri, *just* angekwenda kwenye Chama cha Waajiri na mambo yake kumalizwa. Sasa nadhani tubadilike kwa hilo.

Suala jengine kwenye ukurasa wa 46 kuhusu Programu ya Ajira kwa Vijana, ambayo ni nzuri. Mhe. Spika, ni bahari njema sana kwamba Mhe. Waziri kuanzisha mpango wa ajira kwa vijana. Swali langu ajira hizi hasa wamezielekeza vipi. Kwa mfano, kwenye sehemu fulani hivi katika kitabu hiki zimeorodheshwa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo sikulipenda sana kuhusu kuundwa Kamati ya Kuchunguza Walimu Wanaoharibu Watoto. Kwa kweli wanaoharibu watoto si walimu peke yao ni jamii nzima inaharibu watoto, kwa sababu hii inaonesha kama walimu ndio mafataki, yaani inaleta picha katika nchi hii walimu ndio mafataki, lakini walimu sio mafataki. Sasa nao hapa kuna kuundwa kwa kamati ya kuchunguza vitendo vya uzalilishaji wanafunzi hasa vile vinavyohusisha walimu.

Kwa hivyo, tukisema hasa walimu na mimi ni Mhe. Haji Faki Shaali ni mwalimu na wala siku moja sikuwahi kumdhalisha mtoto wa mtu, yaani nimesomesha miaka 17. Sasa itakuwa tunawanya hawa walimu ni mafataki, lakini kuna watu ambao si walimu ndio mafataki katika nchi hii.

Nadhani tungeunda kamati kwenye mitaa kwa ajili ya kushughulikia masuala haya ya udhalilishaji, lakini tukisema *particularly* walimu hili si zuri na litawatia roho mbaya sana walimu wenzangu, lakini kuwa moja moja mwenye dosari yupo na wala sio walimu wote.

Sasa kuona inaundwa kamati maalum kwa ajili ya walimu tu, hii si nzuri. Kwa hivyo, hizi kamati tuzigeuze badala ya kuwa walimu ziwe zinashughulikia hao mafataki wa watu wote kwa ujumla.

Suala la mwisho ambalo nataka nimalizie, kwa sababu muda mchache umebakia. Kwa hivyo, ninamuunga mkono Mhe. Said Ali Mbarouk katika wazo ambalo amelieleza kuhusu fedha za maendeleo. Kwa mfano, tunaona Mhe. Waziri ameomba shilingi milioni 60 kwa ajili ya maendeleo, lakini si kweli kama atatumia shilingi milioni 60, bila ya shaka kuna fedha nyengine zinatoka kwa hawa washirika wetu wa maendeleo, lakini hizi mara nyingi mawaziri na sio yeye tu haziombwi.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora mara nyingi huwa ninahoja kuhusiana na suala hili, kutokana na kusoma Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba fedha nyingi kwa sababu haziombwi kwenye Baraza basi zinaingizwa moja kwa moja katika ile miradi husika.

Kwa hivyo hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anashindwa kuzikagua, kwa kweli anashindwa na kupata tabu sana kukagua na mahesabu ya fedha zile zinazoletwa na wafadhili, kwa sababu wafadhili wengine wajanja moja kwa moja wanaingia katika mradi.

Sasa hata wanapokagua Idara ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wanashindwa, hapa kidogo kunakuwa na maswali mengi ya kujiuliza, yaani Mdhibiti anakuwa anatapa tabu na sisi wengine ambao tunaosoma ripoti zake pia tunapata tabu. Mhe. Spika, naunga na Mhe. Said Ali Mbarouk, kwa sababu alisema ah! Hivi Mhe. Waziri baada ya hizi shilingi milioni 60 alizoomba hakuna tena fedha nyengine kwa ajili ya maendeleo. Je, zitakapokuja nyengine tusiidhinishe.

Kwa kweli najua nyengine zipo za wahisani, lakini hizi mawaziri hawaziombei, yaani wanakuwa na sababu zao wanazoeleza kama vile inakuwa bado hazijapatikana, kwa hiyo kuzitia kwenye bajeti baadaye itakuwa matatizo kama hazikuingizwa. Sasa wakati zinazoingizwa kwenye miradi bila ya kukaguliwa na Mdhibiti nalo ni tatizo kimahesabu.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, nianze mchango kwenye wizara hii kwa kuangalia bajeti, kwa sababu bila ya shaka Mhe. Spika bajeti ambayo inaletwa hapa ndio ambayo inayomuwezesha Mhe. Waziri kuteleleza zile kazi kaze ambazo anazileta hapa na kusema hizi ninaahidi kuzitekeleza katika kipindi au mwaka huu wa fedha.

Kwa kweli nataka nioneshe masikitiko ambayo ninayo kwa wizara hii au serikali kwa jumla. Mhe. Spika, mwaka jana wizara hii imepata asilimia 39 katika fedha ambazo waliomba, wizara hii tunasema ni mtambuka na kweli Mhe. Spika.

Kwa mfano, kama alivyokuwa mama ndani ya nyumba inakuwa ni mtambuka, basi na wizara hii ni mtambuka, kwa sababu mama ndiye ambaye mwenye kuangalia watoto na wala haijatokea hata siku moja Mhe. Spika, mtu kwenda

nyumbani na kuulizwa na watoto baba chakula changu kiko wapi na haidhuru baba ndiye mtafutaji, lakini mama ndiye mpangaji wa mipango yote. *(Makofi)*

Vile vile kwa upande wa elimu, afya hatujawahi hata siku baba kubeba mtoto na kumpeleka *clinic* na wenye kufanya kazi hiyo ni akinamama. Kwa hivyo, haya majukumu tunaanza tokea majumbani. *(Makofi)*

Sasa wizara hii Mhe. Spika, inaonekana ndio ya mwisho kibajeti. Kwa kweli hatumfanyii haki Mhe. Waziri na wala sio tu kama hatumfanyii haki Mhe. Waziri, lakini hatuwafanyii haki Wazanzibari, wakiwemo akinamama, vijana pamoja na watoto. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naiomba serikali ione umuhimu wa akinamama, vijana na ajira pamoja na watoto. Kwa hivyo, ili tuone kwamba serikali kweli inathamini mwanamke ni vyema tuone mabadiliko ya bajeti Mhe. Spika yanavyobadilika, wala hayendi hivi ambavyo tunakwenda na tutakaa hapa na kumlaumu Mhe. Waziri. Lakini kusema kweli tunambebesha mzigo ambao sio wake, yaani tunambebesha mzigo ambao tunauhakika hawezi kuufikisha kwa mujibu wa bajeti hivi ilivyo. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, naiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Spika, iangalie wizara hii kwa jicho maalum, yaani iangalie wizara kwa jicho la kumkomboa mama na mtoto wa nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 58 kuna Idara ya Mfuko wa Kujitegemea. Kwa kweli Mhe. Waziri ametueleza mengi, lakini mimi nimevutika zaidi na kipengele cha 5 na 7 katika kushiriki kwenye maonesho mbali mbali ya kupata masoko ya ndani na nje wananchi wetu.

Kwa hivyo, hapa isiwe kuwapatia fursa za kwenda kwenye maonesho, vile vile Mhe. Waziri ajitahidi kwa sababu miongoni mwa mawaziri ambao wanarunga na yeye mara nyingi anaruka tunamuona. Sasa huko anakokwenda pia awatafutie fursa kwa hawa tunaowapa Mifuko ya Kujitegemea, kwani mifuko hii tunataka iwe endelevu, nadhani ni vyema wakajifunze katika nchi nyengine namna ambavyo wenzao wajasiriamali wanavyoitumia mifuko ile. *(Makofi)*

Kwa mfano, sehemu ya Juakali iko kila nchi duniani, yaani katika nchi zote duniani wako hawa wajasiriamali kwa hapa kwetu maarufu Juakali. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atumie hizi fursa ambazo anazipata, kuhakikisha kwamba kule anakokwenda na watu wetu wanakwenda japo kidogo kidogo, kwa ajili ya kujifunza namna gani wenzao wajasiriamali wanavyoiendeleza mifuko hii.

Vile vile alitueleza kwamba anawasaidia kiubunifu. Mhe. Spika, nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri, kwa sababu tatizo kubwa ambalo tunalo ni kukosa ubunifu. Kwa mfano, fedha zinatolewa japo kuwa hazitoshi, lakini kwa kuganga njaa tu zinaganga, tatizo hasa ni ubunifu wa kutumia zile rasilimali ambazo tunazo katika nchi na kuhakikisha kuwa hizi zinatuletea kipato.

Mhe. Spika, tumekosa ubunifu hata wa bidhaa kama vile ndimu kwa hayo mazulia ambayo yanafanywa, sabuni, lakini hata ile *package*. Sasa wakati tunapokwenda kwenye maonesho haivutii, unaweza kuona kipande kikubwa cha sabuni na kutokana na ile rangi yake pamoja na hali yake basi haiwezi kumvuta.

Kwa hivyo, kama kunakuwa na utaratibu mzuri na Mhe. Waziri alisema kwamba wamendaa vifungashio, yaani *package* tukawa tunawasaidia namna ya kuandaa basi mtu yeyote anaweza kuvutika na ile hali yake. Kwa mfano, hiki kitabu ukikiangalia unaweza kuvutika na hii caver ambayo iko nje kabla ya kufungua ndani. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, miongoni mwa mambo ya kuwasaidia nadhani ile bidhaa ambayo wanaipeleka kwenye maonesho na kuwa kwenye hali ya kuvutia, kitu ambacho kitasaidia kuvutia basi ni ile *package* yenyewe. Vile vile sio kuvutia tu pamoja na kuongeza thamani ya ile bidhaa, kwa kweli ni tofauti mtu unapompelekea kipande cha sabuni ya karafuu au liwa kwenye kifucho cha *plastic* cha kawaida na ukimpelekea kwenye *package* nzuri, sasa bei ambayo utauza ni tofauti sana. Kwa mfano, unaweza kuuza mara tatu ya bei kwa lile box ambalo umeitia bidhaa ile.

Suala jengine Mhe. Spika, ni kuhusu ushauri wa kitaalamu wa mafunzo ya utumiaji wa hii mikopo. Kwa kweli bado inaonekana mikopo haijatumiwa kitaalamu kutokana na watu wetu kukosa hii taaluma. Kwa hivyo, naiomba wizara kupitia kwako Mhe. Spika, iwasaidie sana mikopo badala ya kupunguza umasikini inatutia ufukara.

Sasa mtu anaposikia kuna mkopo anakwenda kuchukua vizuri, lakini matokeo yake anafanyia harusi au ananunulia *furniture*, siku mbili tatu fedha zinatakiwa kurudishwa inakuwa magodoro pamoja na vitanda juu ya vichwa, yaani inabidi mtu auze kwa ajili ya kurejesha mikopo ya watu.

Kwa maana hiyo, mikopo hii haitusaidii na wala haiwi endelevu. Kwa hivyo, tuwasaidie wanawake wenzetu kuifanya mikopo hii ambayo wanayochukua basi iwasaidie kimaisha na iwe endelevu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu uwekaji wa hesabu. Kwa mfano, nilitembelea baadhi ya vikundi vya akinamama, lakini inaonekana bado

hawajafahamu utaratibu wa kuweka mahesabu. Kwa hivyo, nimefurahi sana kuona kwenye malengo ya Mhe. Waziri yaliyopita yale yenye kuendelea kuwafahamisha wanawake au wanavikundi kujua namna ya uwekaji mzuri wa kumbukumbu. Kwa kweli hili nalipongeza kwa sababu inaonekana ni tatizo kumbwa ambalo tunalo. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, kwa kweli bado katika idara hii kuna matatizo, watoto wa Kizanzibari wananyanyasika. Kwa mfano, kuna Mhe. Haji Faki Shaali alisema hapa hii kamati ambayo imeundwa imesama hususan walimu.

Nadhani unyanyasaji wa watoto hautokani na walimu peke yake na huu upo mpaka kwenye mitaa, labda inawezekana huko kuna kesi moja au mbili ambazo inakuwa ni rahisi, kwa sababu ipo machoni kwa watu kama vile walimu nafikiri hizi ndizo Mhe. Waziri zinazomfikia.

Kwa hivyo, kuhusiana na kamati hizi naunga mkono ziundwe, lakini utendaji wake uangalie jamii nzima. Kwa kweli huko mitaani ndiko kwenye matatizo zaidi, kwa sababu kesi hizi zipo na zinamalizika kifamilia. Kwa mfano, mtoto amejeruhiwa hatua ya kwanza kwa wazazi au mtoto amebakwa kwanza wanakaa wajomba au mashangazi na kesi mara nyingi zinamalizika kifamilia tu.

Mhe. Spika, mtoto anapobakwa huharibiwa maisha yake, kwa sababu licha ya kimwili na hata kiakili ikiwa ni mwanamke au mwanamme na wala hakui tena katika mazingira ambayo atakua mtoto mwengine ambaye hakufanyiwa vitendo hivi viovu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, suala hili alishughulike kwa umakini sana.

Hata hivyo, si hapo mpaka kwenye vyombo ambavyo tunashirikiana navyo kama vile polisi na hospitali, kwa sababu kesi haiwezi kuwa kesi mpaka na kuthibitishwa kuwa hiki kitendo kimetendeka kama polisi na hospitali havikushiriki kikamilifu. Kwa mfano, polisi wanamanung'uniko yao.

Mhe. Spika, nahimizwa wakati umekwisho sijui utanipa kiasi dakika kama kumi.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, malizia kwa sentensi moja ya mwisho kuhusiana na hotuba hii. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Zahra Ali Hamad: Mhe. Spika, niseme kwamba ninaunga mkono hoja, isipokuwa ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kuhusu suala

la watoto alitilie mkazo sana, kwa sababu hao ndio vijana wa wazee wa taifa la kesho. *(Makofi)* Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Zahra Ali Hamad, tunakushukuru na kweli tumetumia sentensi moja ambayo ilikuwa na kituo kidogo katikati, kwa hiyo hukuzidi yale masharti ambayo tulikuwa tumeyatoa hapa.

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa mashirikiano yenu makubwa. Kwa hivyo, jioni tutaanza kumsikiliza Mhe. Suleiman Hemed Khamis pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine ni vyema tufike mapema kwa ajili ya kuendelea na kazi hii.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Kazi, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto, pia nimpongeze Waziri wa Wizara hii kwa juhudi zake kubwa za kutaka kuleta mafanikio na maendeleo pamoja na Katibu Mkuu anayeshughulikia suala hili, pamoja na wafanyakazi wote niwapongeze kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya.

Mhe. Spika, mimi katika suala la Wizara hii ya Kazi, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto nasema ina majukumu makubwa sana na nimpe pole Mhe. Waziri kwa majukumu ambayo ni mazito katika Wizara yake ambayo yote anataka yafanikishwe vizuri, lakini vile vile niseme katika wizara hii ana jukumu la kwanza la kuwatafutia watu kazi, jukumu la pili ni kuangalia vijana ambao wametanda walio wengi katika nchi hii pia nao wanahitaji kazi.

Lakini vile vile tuangalie kundi jengine la wanawake ambalo linamuangalia yeye kwa mfanikio, lakini vile vile tuangalie hali halisi ya watoto wetu wengi sana ambao wote wako katika wizara yake, kwa hivyo niseme tu kwa ufupi kwamba Mhe. Waziri ana mzigo mzito sana ambao bila ya kufikiria tunaweza kumtia katika matatizo tukasema labda hataki kutuongoza si kwa namna hiyo, lakini kwa sababu ya kuwa naweza kusema kwamba kwa kiwango cha fedha ambacho anakipata na mgao wa makundi niliyokwisha kuyazungumza ya wanawake, watoto pamoja na vijana. Fedha ambayo wanaipata haitoshi kuweza kufanikisha masuala yote. Kwa hivyo kwa ufupi naweza kusema kwamba bajeti anayoipata haistahiki kwa shughuli zote hizi nzito.

Sasa katika mchango wangu mwengine ambao nataka nizungumzie mimi nitaanza kwenye maisha bora ya katika femilia, tukizungumuza hali ya maisha bora hii ni hali nzuri ya kimaisha kifemilia au ya kimaisha ambayo ikiwa tukiwa tunasema hali ni nzuri katika femilia ina maana mambo yake yote katika femilia ni mazuri yaani hana matatizo bila ya shaka itakuwa katika kujipangia maisha yake ya kutwa nzima milo mitatu inaweza kupatikana. Asubuhi, mchana na jioni hayo ndio yatakuwa maisha bora ambayo hiyo ndio ya kupigiwa mfano hapo ndio utasema wamekamilisha hali nzuri ya kimaisha kwamba mahitajio yote ya nyumbani yanaweza kupatikana chakula kwa wakati.

Hili kama ikiwa mafanikio ya maisha ya kifamilia ikiwa ni mazuri basi tunaweza tukasema hivi, kwamba katika familia ile kutakuwa na utulivu wa kimazingira mazuri, ya bashasha, furaha kwa sababu kila kitu kinakwenda vizuri hakuna matatizo. Lakini pale ambapo utulivu wa kimaisha haupatikani hayo ni matatizo na itakapokuwa imeshindikana kuweka hali nzuri ya kimaisha, hayo ndio tunaita kuna mambo ya matokeo mengi ambayo yatatokezea katika familia ile. Hizi tunaweza kusema ni suala zima la *economic problems* au *domestic problem* za kinyumbani. Hizi *economic* na *domestic problems* zote kwa jumla ndizo zinazochangia matatizo katika familia.

Pale tunaposema familia hii ina mambo mazuri na hii haina mambomazuri, ni kutokana na hizo *economic problems*. Hizo ndizo zinazozaa matatizo katika nyumba, kwa sababu wameshindwa kuweza kufanikisha maisha mazuri. Hapo ndipo tunaposema kwamba umasikini katika familia hizi umetanda na ikiwa umasikini umetanda hali ya kimaisha itakuwa ni ngumu, katika familia hizo utulivu utakuwa haupo, hilo ni jukumu kubwa sana.

Ukitizama kwa upande wa pili familia kama hizo kutakuwa kuna baba, mama na watoto. Watoto wanaweza kuwa wadogo na kuna wajane wengine wa kike watakaokuwemo katika nyumba ile.

Sasa tujaalie katika familia ambayo kidogo *economical problems* zimetanda, umasikini umekuwa wa hali ya juu, hiyo tunasema. Watoto hawa ambao wataokuwa katika nyumba ya familia hii, basi tutarajie kwamba katika skuli zao wanazokwenda u-*truancy* utapatikana. Kwa sababu kutakuwa hakuna *regularity* ya masomo yake, leo atakwenda kesho haendi kutokana na hali ya *circumstance* za kinyumbani, hali za kimaisha za kinyumbani anakatisha masomo.

Kwa hivyo, hiyo hali moja ya familia zilizokuwa ngumu moja katika matatizo yatayojitokeza nikwamba, watoto watakuwa na *irregular attendance* ya skuli zao, hawatokwenda kikawaida. Hilo ni moja.

Lakini la pili ambalo litajitokeza katika matatizo ya familia ngumu, ninalolifikiria mimi ni suala zima la *family separation* (kubaguana) baina ya mke na mume. Kwa nini wakabaguana hawa? Ni kutokana na hali ngumu za kimaisha. Sasa umasikini huu uliosababisha hawa watoto wasipate masomo yao ya kawaida, *family separation* ikapatikana mume na mke kila mmoja yuko kwake. Kwa hivyo, kama familia hizi zitabaguana, tunasema yale mapenzi ya wazee yatakosekana wakati baba na mama na watoto wako mbali mbali. Hilo ni suala kubwa ambalo Mhe. Waziri ni lazima akae kitako alifikirie kwa hali ya kuonesha hali ya umasikini tulionao.

Sasa kama ni hivyo. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuhakikisha kwamba *separation of family* haitokezei, *truancy* ya watoto kwenda skuli haitokezei. Huo ni utaratibu ambao atauandaa yeye.

Mhe. Spika, labda suala ambalo litatusaidia pengine kutakuwa na suala la ajira ambao ni *implement* hii itaweza kutusaidia kidogo, lakini sasa wizara katika hali hii ikiwa ajira haipatikani hilo ni tatizo jengine vile vile. Je, kama yeye ni Wizara ya Kazi anatafuta lazima watu wake awapatie kazi je, kazi ikiwa hazipatikani kwa femilia zote hizi au kwa watu wote hao au kwa nusu ya femilia zile, hapa Waziri atakuwa na mpango gani katika kusaidia kwenye ajira.

Labda tuangalie katika suala jengine ambalo linaweza kutusaidia katika huu mfuko wa kujitegemea ambao naamini kama ikiwa mfuko huu utakuwa ni mzuri na unakuja kwa wakati ni mfuko ambao unawasaidia hawa kwa ajili ya maendeleo yao, sasa mfuko huu wa Mhe. Rais Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Mhe. Dk. Amani Abeid Karume wa Zanzibar ambao utaweza kutusaidia sisi ili angalau kuweka watu hawa katika harakati, lakini jambo ambalo mimi silifahamu kama ikiwa mfuko huu utakuwa upo ni vipi unaendelezwa. Visiwa ni viwili umasikini uko huku na huku tunakwendaje katika ugavi huu nasika kuna *one hundred and twenty million* ziko zinatengwa kwa ajili ya mfuko wa kuwasaidia watu kuendesha maisha yao.

How do you go about tunazitoa vipi hivi fedha, majimbo yetu ni mamsini tunakwenda je au tunaendelea wale kwa wale wanapewa kama hatuna ratiba maalum ya kuweza kuhakikisha kwamba mfuko wa Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete na Mfuko wa Dk. Amani Abeid Karume hawendi sambamba kwa ajili ya majimbo tuliyonayo ugavi wake utakuwa sio barabara, lakini nahitaji kuona kwamba hiyo mikopo ambayo itapatikana kutokana na mfuko huu ambayo itaweza kuwapa wananchi nafuu katika kuendeleza biashara zao.

Lakini sasa nina wasi wasi wa kitu kimoja unajua unapofanya kitu bila ya kitu kile unachokifanya kufanya *follow up* ya lile jambo unalolifanya hayo ni matatizo, huwezi kujua kwamba hii mifuko tunayoitoa inasaidia jamii au

haisaidii jamii. Kama ikiwa mifuko hii wanaipata je wanafaidika kiasi gani?. Faida wanapata au hawapati?. Lakini kubwa ambalo nina wasi wasi nalo kutoa pesa sio hoja, kuwasaidia sio hoja inategemea je, wanapopata mifuko hii wanayo elimu ya kuweza kuendeleza ile mifuko yao ni kiasi gani watu hawa ambao wanapewa mifuko, wana elimu ya kutosha ili kuweza kuhakikisha kile wanachokifanya kitaleta faida si hoja pesa zinaweza kutolewa, kila mwenye bahati yake anapata kama ulivyosema mtu badala ya kufanya kwenye *target* je ana malengo huyu au hana malengo fedha kapewa kweli ana malengo ya kuweza kufanya kitu cha kusawazisha familia yake.

Kwa hivyo ikiwa suala hili halikutolewa elimu ya kutosha katika kuendesha biashara zao itakuwa huu mfuko haukuleta faida, kwa hivyo mimi ningelimshauri Mhe. Waziri afanye *follow up* ya suala lao hili, au kwa ufupi ningemshauri Mhe. Waziri Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwamba pafanywe tathmini katika mifuko yote inayotolewa ni kiasi gani watu wamefaidika katika suala hili. Hili nafikiri litaweza kusaidia na kile kilio cha watu ambacho kipo kwa muda mrefu.

Jambo jengine ambalo baada ya mfuko huu kutolewa kuna mambo mengine ambayo Mhe. Waziri anaweza kuandaa huo ni mmoja katika kuokoa matatizo ya kifemilia, au matatizo ya jamii. Lakini kuna la pili muhimu linahitaji maandalizi ingawa maandalizi yake ni makubwa na gharama zake ni kubwa, kwa hivyo niweze kusema kwamba wizara yake ni wizara mama ambayo wizara hii inajumuisha matatizo yote ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, matatizo yate ya Afya na Ustawi wa Jamii hawa Mawizara wana Wizara moja moja wanakwenda na jamii ya wagonjwa wa wanaume, wanawake na watoto elimu ina wanafunzi pamoja na walimu wake.

Lakini wewe Mhe. Waziri una kazi kubwa sana kwa sababu wewe hao wote walioko katika mawizara wote hawa ni watu wako weye ni jamii yako watoto wanawake pamoja na vijana wote unahitaji kuwahudumia, sasa lile la kwanza nimeshalizungumza la fedha lakini hili la pili ambalo ninaweza kusema ni suala zima la stadi za kiufundi. Hili kama litaboreshwa vizuri, kama litaendeshwa vizuri likaweza kutengenezwa kwa hawa vijana maana watoto hatuwezi kuwatia katika stage hii bado wao wanasoma, lakini wanawake na vijana tunaweza kuwatia katika makundi hayo na tukaweza kuwasaidia kuwafungulia stadi mbali mbali.

Mhe. Spika, dunia ya leo katika kufanya kazi wanawake nimeshawakuta wanabeba makarai katika suala zima la ujenzi wa majumba wanarusha karai kama wanaume, wanajitia vilemba wanafanya kazi kwa hivyo mimi siamini kwamba mwanamke hawezi kutumika au kufanya kazi. Mimi kwa ushauri wangu namwambia Mhe. Spika, kwamba Mhe. Waziri ajitayarishe kuweka hizi stadi mbali mbali na katika stadi hizo tuweze kuelewa kwamba ziko stadi za

uchongaji, ufundi matayarisho kitu kama hicho au skuli maalum tuwape ujuzi, kwa sababu ujuzi hauzeeki, elimu haizeeki.

Kwa hivyo hawa vijana wetu tukiwapatia ili kuondosha ile sokomoko ya *miss under stand* kutofahamiana watu kutokana na ajira makundi ya vijana na wanawake kukaa bila ya kazi tuweze kufungua ili tujue hapa kuna kitu fulani cha ufundi inaweza kuwa useremala, katika kazi nyengine za ufundi mdogo mdogo, kazi za gereji. Au kazi nyengine ndogo ndigo zinaweza kusaidia kuwapa hawa muinuko wa maendeleo kwa sababu katika kuangalia maendeleo hatuangalii mahala pamoja tu tukasema tuwape pesa kwa ajili ya kufanya biashara hiyo njia moja. Lakini kuna njia nyingi ambazo za kuweza kuwasaidia yeye mwenyewe Mhe. Waziri namna gani ataweza kujipanga katika kuzisaidia jamii. Mhe. Spika, hizi ni changamoto tutaweza kuzijenga femilia vizuri na tutaweza kujenga familia zetu nzuri.

Mhe. Spika, lakini jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala zima la maadili mimi niweze kusema tu kwamba kwa wakati tuliokuwa nao sasa nasema hasa maadili yameporomoka, nani anayeporomosha maadili haya ni sisi wenyewe sisi ndio wenye dhamana sisi wenyewe wazazi baba mama pamoja na majirani sisi ndio chanzo kikubwa cha kusababisha maadili hayo kuporomoka, kwa sababu na sisi kama ni wazazi tuna dhamana kwa watoto wetu tuhakikishe kwamba maadili hayaporomoki. Sasa kama sisi tunafanya dharau au kutokujali au kutokubali kwamba lolote mtoto wake analofanya ni sawa hii ndio itatupeleka pahala pabaya.

Mhe. Spika: Mheshimiwa muda umemalizika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ishaalla ni lazima tuhakikishe tunatoa katika madili haya kwenye walimu kwenye wazazi, tunawapa vile vile walimu wa vyuo tunapeleka vile vile maelekezo yetu, kwa hivyo maadili mema na mafunzo yataweza kupatikana. Heshima itaweza kurudi na wazee wataweza kunena, lakini mimi niweze kumwambia tu Mhe. Waziri hapa kutakuwa na kitu kama mnapigana hivi kutakuwa na mvuto fulani, huku wazazi wanataka kuweka maadili mazuri, lakini huku kuna *Inver mental process* yani mazingira au *immigration* watu wanaoingia na watu wanaotoka wao ni walimu wazuri sana wa kuwaharibi watu au watoto na mafanikio ya maadili kupotea, hii huingia kwa watu na kutoka kwa watu maadili yetu yanaanza kupotea kwa namna hiyo sijui hapa Mhe. Waziri hii *integration* ya watu na kuona watu wameendelea kwa maendeleo ya kisasa sijui hapa Mhe. Waziri atatusaidia kwa kiasi gani kuweza kuhakikisha mambo haya.
Mwisho Mhe. Spika, niseme tu afya ya wazazi katika wazazi hakuna sekta ambayo au binaadam aliyekuwa ni muhimu kama wanawake lazima tuwajali sana, ndio maana Wizara hii ukapewa wewe kama ni mwanamke kwa sababu wewe ni Mwanamke sasa hapa tukisema kwenye takwimu wanaweke ndio

wengi sana kuliko wanaume, sasa una kazi kubwa. Kuna suala zima la lishe bora kwa wanawake hapa tunakwenda je Mhe. Waziri, kwa sababu tunahitaji kupata takwimu ni watu wangapi tulionao ambao bado uwezo wao wa kuweza kupata lishe, kama wanawake hatukuweza kuwapa lishe huyo mtoto anayezaliwa atakuwa vipi na sisi tunataka yule mtoto tuweze kumpa kazi yeye awe mfanya kazi wetu bora.

Kwa hivyo nasema Mhe. Waziri nakupa pole kwa kazi ngumu uliyonayo na kwa sababu muda wangu ni mfupi nina mengi ya kuzungumza lakini muda hauruhusu. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako mimi nasema naunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri mia juu ya mia kwa hayo nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii na mimi kuweza kutoa mcahngo wangu mfupi mbele ya hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana Maendeleo ya Wanawake na Watoto kwa ajili ya kumsaidia maarifa ya kuboresha zaidi.

Mhe. Spika, kwanza nipongeze wizara hii kwa ujumla kwa jinsi walivyo makini na walivyochapisha kitabu chao, nimejaribu kuangalia vitabu vyote ambavyo tumeletewa hapa lakini kitabu cha wizara hii kina hali ya juu, ukiangalia vitabu vyote ambavyo tumeviangalia vya wizara kumi na moja kitabu cha waziri mwanamke kinaongoza kwa umadhubuti nimpongeze kwa hilo na naomba aendelee na hilo.

Mhe. Spika, lakini jambo la kwanza ambalo nataka kuchangia ni malalamiko ya watoto ambayo wizara imeyapokea kwa kipindi hiki cha mwaka 2009/2010, malalamiko ya watoto kwa Unguja ni malala miko mia mbili na kwa Pemba ni malalamiko mia moja na sitini na mbili sawa sawa na malalamiko mia tatu na sitini mbili. Ukiangalia malalamiko haya kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja Kaskazini (A) sitini na saba na Kaskazini (B) thalathini na tisa, jumla ni malalamiko mia moja na sita sawa sawa na asilimia 53% ya malalamiko ya Unguja.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri anifahamishe kwa nini Mkoa wa Kaskazini Unguja ukawa na asilimia 53% ya malalamiko ya watoto kwa Unguja kuna tatizo gani la msingi, na je wameweza kufanya utafiti wa kujua kwa nini Mkoa wa Kaskazini Unguja ukaongoza kwa malalamiko na kesi za watoto.

Sambamba na hilo Chake Chake wana malalamiko mia moja na sita sawa sawa na malalamiko 65.4% ya malalamiko ya Pemba pia ningetaka nijue kwa nini Chake Cheke ikaongooza kwa Pemba kwa malalamiko. Ukiangalia wilaya ya Chake Chake, Kaskazini (A) na Kaskazini (B) ina malalamiko 58.56% ya malalamiko yote ya Zanzibar kwa maana hiyo Kaskazini Unguja na Chake

Chake inaongozwa kwa asilimia hiyo kwa malalamiko yote ya Unguja na Pemba. Sasa hapa tunataka kujua kwa nini wilaya hizi tatu zikaongoza kwa malalamiko ya watoto.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ningeligusia ni suala zima la mafunzo ya wafanyakazi na nitoe pongezi kwa juhudu ambazo Mhe. Waziri amechukua kama walivyosema wenzangu, ukiangalia kwenye mafunzo haya wanawake ishirini na moja wamepatiwa sawa sawa na 67.7% na wanaume kumi sawa sawa na 32.3%. Ningetaka nimueleze Mhe. Waziri tunapozungumzia jinsia hatuna maana ya wanawake tu tuna maana ya wanawake na wanaume kwa hapa kidogo upendeleo umeufanya mkubwa kwa asilimia 67.7% ya wanawake, ningekuomba basi ile hamsini hamsini ikawa kwa mote isiwe kwa sehemu nyengine tu. Kwa sababu hapa kidogo wanaume umewapa asilimia thalathini na tatu wanaweke sitini na saba kidogo umejipendelea, ningekushauri ukatoa haki sawa kwa elimu kwa wanawake na wanaume ili ile dhana ya hamsini kwa hamsini ikapatikana.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningelizunguzma ni suala zima la mfuko wa kujitegemea na mikopo kwa wanawake na wanaume ukiangalia kwenye takwimu za mikopo tumeambiwa mikopo thamanini na nne imetolewa kwa wanawake sawa na milioni arubaini na nane na laki tisa, ukigawa ni sawa sawa na shilingi laki tano thalathini na nne mia tano na ishirini na nne. Mhe. Spika, mkopo wa Shilingi laki tano na thalathini na nne elfu kwa mwanamke si mkopo wa kusema kwamba tumemsaidia mwanamke kujikwamua na umasikini. Lakini kwa wanaume ni sawa sawa na shilingi laki sita thamanini na tano elfu mia nne na thalathini na nane na senti sita huu ndio mkopo ambao wanaume wa Zanzibar wamepewa, kwa ujumla pesa wambazo wamepewa wanawake na wanaume ni laki tano tisini na moja elfu mia nne thamanini na tisa huu ndio mkopo amba Wazanzibari wamekopeshwa.

Mhe. Spika, mkopo huu ni mdogo sana na wala hauwezi kuwakwamua Wazanzibari kwenye mashaka haya ya umasikini, kwa mimi ushauri wangu ni kwamba ili kuwawezesha Wazanzibari hasa wanawake serikali imefika wakati sasa kuanzisha benki maalum kwa ajili ya wanawake, juliko kuwapatia fedha hizi za shilingi laki tano tano ambazo kwa upande wangu nahisi ni kumuongezea umasikini na kuongezea madeni ambayo hayataweza kulipika. Ushauri wangu serikali ijiandae kuanzisha benki maalum kwa ajili ya wanawake kama ambavyo wenzetu wa nchi mbali mbali wameanzisha mfumo huo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ningeligusia ni mmong'onyoko wa maadili na hapa niseme kwamba kumekuwa na dhana kwa baadhi ya watu kwamba mwanamke kwa kiasi kikubwa anachangia katika mmong'onyoko wa maadili katika jamii, mimi sio mtaalam wa hilo wala sijafanya utafiti lakini kwa sababu

changamoto hii wananchi wanaizungumza ni budi kwamba serikali ifanye utafiti kujua je, ni kweli wanawake wanachangia kwa kiasi kikubwa katika mmong'onyoko wa maadili ya jamii. Hoja zao hawa ambao wanasema hilo wamesema kwamba kumekuwa na elimu kubwa kwa wanaweke walio matajiri na hata vyeo basi wao ndio mwanzo ambao huchangia kuharibu ndoa, sasa hili ni jambo ambalo linazungumzwa na wataalam wa wizara hii ni vyema wafanye utafiti kujua kwamba je, kweli wanawake wenye elimu, utajiri na uongozi ndio ambao wanakuwa wa mwanzo kumong'onyoa ndoa na kama hilo ni kweli basi likatafutiwa dawa ili mmong'onyoko wa maadili katika ndoa ukaweza kusimamiwa.

Lakini jengine ambalo watu wanalalamika ni kwamba kunakuwa na baadhi ya wanawake wanatumia mtoto wa kike kama ni chanzo cha fedha, sasa kama hili ni kweli pia ni vyema wizara hii ikafanya utafiti kujua kama hilo lipo basi wizara wakalifanyia kazi mapema.

Lakini jengine ambalo wananchi wanalalamika ni kwamba suala zima la omba omba wanawake wanachangia kuwatuma watoto wadogo kuongoza kwenye biashara hii ya omba omba, sasa mambo haya matatu nadhani ni nafasi nzuri kwa serikali kuwa ni changamoto ya kufanya utafiti kwa suala hili ili kuweza kuliondoa ndani ya jamii. Kwa sababu kama litashamiri na kuota mizizi basi jamii itakuwa inaendelea kudumaa siku hadi siku.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri katika changamoto hizi ambazo zinaonekana ni vikwazo kwa jamii najua fedha wanazotiliwa hazitoshi na nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha kwamba tumekuwa na kilio miaka yote mitano ambayo tumo kwenye baraza hili, kwamba wizara hii ni wizara ambayo inapata fedha ndogo sana sasa tusingependa mwakani baada ya uchaguzi tukaona wizara hii inaendelea kushika mkia, tutakuwa hatupendi na tutakuwa hatukuelewi Mhe. Waziri pengine mwakani utakuwa waziri wa fedha lakini hizi salamu umpe waziri wa fedha kwamba wizara hii musiendelee kuionea kwa sababu ina jukumu kubwa la kuongoza wanawake, vijana na watoto.

Mhe. Spika, kwa mchango huo naomba Mhe. Waziri azingatie maelekezo yetu naunga mkono hoja hii mia kwa mia ahsante sana.

Mhe. Moh'd ali Salim: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii sasa hizi, mimi naanza kwa kumshukuru allah na kumuomba aniongoze vyema katika kuchangia wizara hii iliyokuwa ni wizara mtambuka.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia kwa sababu naogopa kusahau naomba niunge mkono hoja kabla sijaanza kuchangia *(Makofi).*

Mhe. Spika, kama nilivyotengulia kusema kwamba wizra hii ni wizaa mtambuka ni wizara iliyoziguza wizara mbali mbali katika utekelezaji wake, kwa kuwa katika kamati tulipokuta tukitembelea sehemu mbali mbali tumekuta mambo ambayo yalikuwa yanahitaji uratibu wa kukaa pamoja baadhi ya wizara kama mbili au tau kulitatua tatizo moja lililoko, sasa hili naomba nitoe wito kuwa wizara nyignie zinazohusiana na wizara hii basi ziwe tayari kukaa pamoja na wizara hii ili kutatua mambo yanayohusiana na wizara mbali mbali.

Mhe. Spika, labda nitoe mfano mdogo tu huu ambao tuliukuta katika eneo la Maziwani wananchi wa Maziwani wamejenga kituo cha mayatima cha kusoma, wamejenga *foundation* ya kituo cha Afya sasa walikuwa pale katika kituo cha kujifunzia tayari kuna walimu wanaojitolea kufanya ile kazi, lakini ilikuwa kuna haja sasa kile kituo kwa kuwa ni cha mayatima na kwa kuwa kinahusiana na mambo ya elimu basi kichukuliwe na Wizara ya elimu wale wafanyakazi pale waajiriwe waweze kufanya kazi kama wanavyofanya wafanyakazi wengine.
Lakini hilo lilikuwa gumu kufanyika kwa sababu wizara ya elimu ilikuwa haielewi kuna kitu gani pale wizara ya kazi inaelewa kuna kitu gani pale, sasa mimi natoa wito mambo kama haya kama ingelikuwa kuna vikao vya kawaida wanavyokaa, najua vikao vipo lakini sijui kwa nini likatokea hili ilikuwa mambo kama yale ambayo yanahusi wizara mbali mbali yazungumzwe katika vikao vile ili yakishazungumzwa kila mmoja wa wizara inayohusika achukue sehemu yake katika utekelezaji. Nafikiri mengi yangelikwamuka bila ya matatizo.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niingie katika mada yenyewe hasa nianzie katika siku ya Wanawake Duniani ambayo ilizungumziwa hasa mambo ya Beijing. Wito uliotolewa mimi nauunga mkono sana. lakini nina wasi kuwa hao waliopewa wito inawezekana ama wakawa hawakufahamu au wanaogopa au wito haukuenea kila mmoja akaupata. Wanawake wanaweza kwa hivyo wapewe nafasi. Inasema hapa miaka 15 ya Beiging wanawake wanaweza wapewe nafasi.

Mhe. Spika, wasi wasi wangu katika hili kuwa wanawake bado woga na nitatoa ushahidi wangu. Hivi hebu niambiwe katika wanawake waliokuwemo katika Baraza hili ni wangapi wameambiwa kwenda kugombea katika majimbo, hakuna. Ikiwa hakuna, ingawa hapa wanasema. Naomba ninukuu wito ulitolewa kwa wanawake kujipanga vizuri kugombea nafasi za uwakilishi na ubunge katika majimbo yao ili kuweza kufikia asilimia 50 katika uchaguzi wa mwaka huu wa 2010. Huu ndio wito uliotolewa, wito huu ulikuwa uitikiwe ndani ya Baraza kwanza na baadaye waitikie waliokuwepo nje Baraza.

Mhe. Spika, nina mtu ninayemjua mwanamke ambaye analikuwa na uwezekano mkubwa kabisa wa kuweza kushinda ndani ya jimbo lakini tu kwa

sababu kuna mwanamme kagombea kutoka tawi lile lile lake anasema kamwachia mwanamme kanambia mimi mwenyewe. Ndio maana nikasema hili nilizungumze hapa, bado hawajahamasika naomba Mhe. Waziri awahamasishe zaidi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niingie katika suala zima la Kamati za Utendaji za kudhibiti unyanyasaji wa kijinsia katika shehia kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 13 wa kitabu cha Mhe. Waziri. Naomba ninukuu.

Kifungu cha 18	"...kuziimarisha Kamati za Utendaji za Kudhibiti Unyanyasaji wa kijinsia katika Shehia zao ili kupunguza kesi za aina hii".

Mhe. Spika, kama zipo kamati hizi basi hazifanyi kazi. Kwa sababu sijapata kusikia hata siku moja kuwa kumetokea unyanyasaji wowote wa kijinsia na kuwa kuna Kamati ya Shehia iliyofanya kazi ikasaidia angalau polisi au pahali popote pale. Kwa hivyo Kamati hizi kama zipo zitakuwa bado hazifanyi kazi inavyostahiki zifanye kazi.

Mhe. Spika, hapa nataka nizungumze kitu kingine. Kutokana na hali halisi ilivyo kuthibitisha kesi hizi za unyanyasaji wa wanawake linakuwa ni jambo zito. Ni ni jambo sio kuwa ni zito lakini ni zito kwa sababu linafanywa liwe zito. Ili jambo hili lithibitike basi ni lazima Wizara ya Afya yaani hospitali ithibitishe kuwa tendo limetendeka.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya imepanga siku moja kwa wiki kuchunguza habari hizi na siku yenyewe wenyewe wananambia Alhamis. Sasa hivi kweli tendo litokee Jumatatu lingoje Alhamis kwenda kuchunguzwa si itaonekana kuwa kazi ilifanywa lakini hajulikani nani aliyefanya. Hili kama halijarekebishwa ikawa linapotokea tukio ndio hapo hapo hospitali inapofanya kazi, bado tutaendelea kupiga kelele siku hasi siku wala hakuna litakalokuwa.

Jambo jengine Mhe. Spika, mimi mwenyewe nina uzoefu kwa kupata kesi nyingi kuja kuambiwa polisi siku hizi wanasema kuwa wao wameambiwa jambo la kwanza wameambiwa wasuluhishe wasipeleke mahakamani tu kitu. Kwa hivyo likitokea jambo kama hili kesi ikifika polisi, wao wanawaita wazee kuja kusuluhisha. Hivi kweli watu kuitwa kuja kusuluhishwa polisi ndio litamalizika jambo hili. Haliwezi kumalizika.

Mhe. Spika, hili jambo bado ni baya na kwa sababu ni baya kuna haja ya kuchukua hatua za makusudi za kulirekebisha ili tukaweza kulikomesha kama vile inavyostahiki kukomeshwa.

Mhe. Spika, sasa niingie kidogo katika Kamisheni ya Kazi kuna malengo ya mwaka 2009/2010 lengo la pili linasema kukiimarisha kitengo cha ajira ili kiweze kuweka takwimu za ajira kwa lengo la kupunguza ajira kwa wageni. Hapa mimi kwanza ninaswali je, lengo hili limetekelezwa ? je tayari sasa hivi takwimu zipo? Na takwimu hizo ni takwimu za walioajiriwa tu au na nguvu kazi ambayo ingestahiki kuajiriwa?

Sasa kama haya yapo tayari basi ni rahisi sasa kusema ukiwa na kazi sehemu yeyote basi moja kwa moja agizo lipelekwe katika wizara ili wizara ianze kuwatangazia wale ambao tayari wanao katika takwimu. Lakini kama si hivyo itakuwa bado hatujafanya ile kazi inayostahiki kufanywa nab ado wageni watapata ajira na wenyeji watazikosa. Hizi takwimu kama zipo je, zinatumiwaje? Kama zinatumiwa vizuri basi na mambo yatakuwa mazuri natarajia na mambo ya ajira yatakuwa mazuri zaidi.

Nitoke hapo niingie moja kwa moja kwenye vikundi vya vijana wajasiri amali na hili linaonekana katika jaduweli ukurasa wa 82 na 83. Tunaoneshwa hapa tumeambiwa katika kiambatisho Nam 9A na 9B, vikundi vya vijana wajasiri amali vilivyofanyiwa tathmini (A) Unguja na (B) Pemba. Ninalouliza hapa kama hivi vikundi vimefanyiwa tathmini vimeonekanaje. Nadhani ilikuwa kuwa na sehemu moja pembeni huku ya kuonesha kama hiki kinafanya vizuri hiki kinafanya vibaya, hivi kipo wastani nafikiri ingekuwa tathmini ipo na hapa tungeliona kwa urahisi na tukajua kikundi gani kinahitaji msaada na kikundi gani hakihitaji. Hili nadhani limekosekana katika jaduweli hizi na hali ya kuwa hapa hili jaduweli halikukusudia kuonesha vikundi tu na majina yake lakini limekusudia kuonesha tathmini iliofanywa ya vikundi hivi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niingie katika mfuko wa kujitegemea ukurasa wa 90. Tunaona hapa kuna wanawake na wanaume waliopatiwa mikopo lakini kama utafanya hesabu upande wa wanawake Mjini Magharib wanawake 38 waliopatiwa mikopo wamepata milioni 23 na laki 9 hizi kama utazigawa kwa mtu mmoja mmoja utafute wastani najua hawakupewa sawa sawa lakini kama utafanya wastani kila mwanamke mmoja kapata laki sita ishini na nane elfu mia tisa na arubaini na saba na senti arubaini. Chukua mkoa huo huo kwa wanaume ambao ni 11 tu. Ukifanya hesabu utakuta kila mwanamme mmoja wastani kapata lakini nane, sitini na tatu elfu mia sita na thalathini na sita na senti arubaini. Hapa inaonesha kuwa bado wanaume tunapendelewa zaidi kuliko wanawake.

Ukija Mkoa wa Kaskazini hali ni kama hiyo utakuta pengo ni kubwa zaidi kwa sababu wanawake ukigawa pesa walizopewa kwa watu 11 waliopewa utapata kila mmoja kapata laki mbili na tisini, mia tisa na tisa na senti kumi. Lakini wanaume kumi tano ukigawa hizo pesa kila mmoja atakuwa kapata laki tisa na ishini elfu, pengo kubwa mno.

Mhe. Spika, najua hakika hali halisi hawa hawakupewa kisawa sawa kuna waliopewa nyingi na kuna waliopewa kidogo. Lakini bado nililokusudia kulionesha kuwa bado wanawake hawajaangaliwa kwa jicho linalostahiki wao kuangaliwa. Hali kama hiyo ipo katika ukurasa wa 94 katika taarifa za mikopo ya uwezeshaji kiuchumi kijinsia. Ukiangalia Unguja wanawake wamepewa mikopo wanawake 191 lakini wanaume wamepewa 211. Hii tofauti yao sio kubwa unaweza ukaikubali.

Lakini njoo Pemba sasa, wanawake wamepewa 33 wakati wanaume wamepewa 132. kuna pengo kubwa mno baina ya idadi ya wanawake waliopewa mikopo hii na wanaume waliopewa. Hii inaonesha kuwa wanawake bado hawajaelimishwa vya kutosha wakaweza kuandika miradi mizuri ikakubalika kule benki na wakaweza kupewa pesa kwa wingi za utekelezaji. Pengine inawezekana ni lile wanalolizungumza wenzangu kuwa mpaka uwe na mradi ndio upewe pesa. Kwa hivyo kwa sababu wanawake wengi hawana miradi na kwa sababu wanaume wengi wana miradi kwa hivyo pesa zinakwenda kwa wale wale wanaume wenye miradi na zinakosa kwenda kwa wanawake ambao hawana miradi.

Mhe. Spika, kwa kuwa sitaki nipoteze muda wako naomba niseme kuwa Wizara hii kuna haja ya kuongezewa ile sehemu ya pesa inayopewa ili iweze kutekeleza majumu yake vizuri zaidi. Kwa sababu ni Wizara mtambuka basi iweze kusaidiwa na kila wizara katika mambo ambayo inastahiki kusaidiwa. Lakini pia namuomba Mhe. Waziri wa Wizara hii asiogope, asione haya, asione vibaya kuomba msaada popote panapostahiki kuomba msaada.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa mara ya pili. Ahsante.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii japokuwa sina mambo mengi ya kusema. Mimi nataka nianze na ukurasa wa 35 Idara ya maendeleo ya vijana.

Katika ukurasa huu kuna malengo ambayo wizara ilipanga kuyatekeleza katika kipindii cha bajeti ya mwaka 2009/2010. kuna lengo moja la nane naomba nilisome `hili lengo wanasema ni “kuandaa na kutekeleza mpango wa malezi kwa vijana kwa kutoa mafunzo ya ushauri nasaha, stadi za maisha, afya ya uzazi, vita dhidi ya ukimwi na dawa za kulevya.

Mimi nataka niseme vijana ni nyenzo moja muhimu sana katika kila taifa. Niwapongeze kwanza Wizara kwa kuwa na malengo kama haya. Ni lengo moja zuri kwa sababu vijana tumekuwa tukipiga makelele sana kwamba ni moja katika sekta inayoongoza katika mporomoko wa maadili. Wakishajiingiza katika tabia hizi mbaya basi tunakosa nguvu kazi. Tunawakuta vijana kadhaa katika chochoro za mji wa Unguja ikiwa kazi yao ni kusinzia tu, kwa sababu ya

kujishirikisha katika madawa ya kulevya. Mimi nafurahi sana Wizara kulizingatia hili.

Mhe. Spika, nafikiri niungane na Mhe. Mula, hili lengo liwekwa kutekeleza katika bajeti ya mwaka uliopita. hata mwaka huu nimeliona limeandikwa tena vile vile sijui sehemu gani, nimesahau lakini nimeliona. Lakini hatupati tathmini ya huu utekelezaji wenyewe umekwendaje. Kwa sababu tulitaka tuambiwe baada ya lengo hili kuwepo kazi hiyo imefanywa na kama imefanywa basi imezaa matunda gani. Lakini Mhe. Waziri yupo kimya kaandika tu malengo, sasa naomba sana akija atwambie katika kufanya kazi hii basi kapata mafanikio gani nakapata changamoto gani.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nende kwenye Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Nimesoma sehemu moja katika hichi kitabu nikagundua kuna sheria ya watoto inaandaliwa, nadhani si muda mrefu italetwa hapa Barazani kwa ajili ya kupata baraka za Baraza. Sheria hii mimi sijapata hata rasimu yake kwa hivyo sijui kilichomo ndani ya sheria. Sijui niseme kama ni bahati mbaya au ni bahati nzuri hii sheria imezagaa katika midomo ya watu katika jamii yetu ya Zanzibar. Na kwa kweli haisemwi vizuri. Mimi kwa kuwa sijui kilichopo lakini kwa kuwa nasikia maneno ya watu yamekuwa makubwa na mengine makali miongoni mwa ambalo linapigiwa kelele sana ni kuhusu malezi ya watoto kwa kutumia bakora. Nasikia hiyo sheria imemkataza mzee kumkanya mtoto wake au kumuelekeza mtoto wake au kumfundisha mtoto wake kwa kutumia bakora. Hili wazee wengi wanalilalamikia.

Namuomba sana Mhe. Waziri tena sana. najua miye watoto anawapenda kweli kweli na ndio maana akapewa hii Wizara. Wakati wa kutunga sheria Mhe. Spika, Mhe. Waziri akumbuke kama anawatungia sheria Wazanzibari, Wazanzibari wana dini yao, wana mila zao, wana imani zao wanazoziamini. Si vyema kutunga sheria hizi usizipe kipa umbele. Nakusudia Mhe. Waziri anapotunga sheria asichupe mipaka ya kidini. Ndani ya qur-an bakora imewajibishwa itumike, ukenda kwenye aya ya tatu kama sikosei ya suratun Nnur nikikosea Dr . Salmin anaweza akaniweka sawa pale. Pale Mwenyezi Mungu kaweka adabu ya bakora ni sheria. Kutunga sheria ya kukataza watu wasipige mikwaju ni kuvunja sheria ya Mungu na ni kuchupa mipaka. Hata miongozo ya Mtume wetu Muhammad (*SAW*), kasema mtoto akiwa na umri wa miaka mitatu mfundishe kwa mdogo aswali akifika umri wa miaka kumi kama hajataka basi mpige bakora. Mafunzo yanayotokana na Mtume (*SAW*) hiyo ni sheria ya kiislamu ukitunga sheria kwenda kinyume na hilo unachupa mipaka. Ndio maana wazee katika nchi hii wakapigia kelele sana suala hili.

Mimi najua ni mfumo wa kidunia lakini tujue hao tunaojaribu kuwafuata huko duniani wengi wao hawana itikadi hizi za kiislamu. Tusifuate itikadi zetu, sisi tuwe watu wa dini bwana. Naomba sana dini ipewe sehemu yake na inaweza

ikawa ni sababu ya mchafuko mkubwa hapa. Kwa hivyo naomba kama kuna kifungu hiki, mimi sijaiyona hiyo sheria lakini kama kuna kifungu hiki naomba sana kabla haijafika hapa kitolewe, kabisa kisije kikaleta mtafaruku hapa katika nchi.

Mhe. Spika, nikiacha hapo nende kwenye Idara ya Maendeleo ya Jamii. Naomba hapa nizungumze mambo mawili. Mhe. Waziri kapanga mambo mazuri sana ya kuiyendeleza jamii, lakini moja sikuliona nalo ni hili la maadili. Kwa sababu kuwa na maadili mazuri au tabia njema basi ni moja katika kuiendeleza jamii kwa kiwango kikubwa sana. Hakuna kikundi kinachoweza kuendelea kama kwanza hakina tabia nzuri au maadili mazuri. Kule nilikuwa nazungumza kwa vijana lakini hapa nazungumza watu kwa jumla.

Mhe. Spika, kila mtu ni shahidi katika nchi hii jamii yetu siwezi kusema kwa asilimia ngapi lakini maadili yameporomoka sana tena sana. Kwa mtu aliyekuwa ana heshimu misingi ya maadili yetu basi mara nyengine anaweza akapata tabu kutembea. Kuna baadhi ya mitaa ukipita utajuta kwa nini ukapita na ukishakuwa na mawazo kama yale kwanza hiyo ni kasoro moja kubwa kwa mtazamo wangu mimi sijui na wenzangu wakoje. Lakini kwa mtazamo wangu mimi kama kweli kuna wizara inashuhulikia maendeleo ya jamii halafu tukaikuta jamii kwa asilimia haipungui 30 haiko kwenye maadili, nafikiri hapo ni kufeli, changamoto hiyo.

Nilikuwa naomba sana katika kuendeleza jamii basi na suala, sujui kama wataendelea kutoa ushauri nasaha ambao mimi naupiga vita kweli kweli ushauri nasaha.

Mhe. Spika, hii na nitakapokuwa Rais wa nchi hii ushauri nasaha nitaupa asilimia 10 au 12 tu lakini zaidi nitakuwa nikitilia nguvu sheria. Maana huwezi ukamuona mtu anafanya kosa kwa makusudi halafu wewe ukaendelea kila siku ukampa ushauri nasaha, hasikii kwa ushauri nasaha. Na kama ushauri nasaha unatosha basi Mungu asingeumba moto. Mimi nafikiri Mhe. Waziri angeshawishi wizara hii inayoshuhulikia mambo ya sheria Katiba na utawala bora wakatunga sheria zitakazodhibiti tabia mbovu katika nchi ili tuipate jamii ikiwa safi ili tuweza kuiendeleza. Lakini leo kila mtu yupo huru anafanya anavyotaka, kubwa linalochukuliwa ni ushauri nasaha, maisha tutakwenda hivi hivi.

Mhe. Spika, jambo jengine katika Idara hii katika kupita pita kwenye Kamati tumegundua kwamba kweli kuna vikundi vinapewa miradi ya kujiendeleza, lakini kuna changamoto mbili kubwa. Kwanza mtaji wenyewe wanaopewa unakuwa ni mdogo kiasi kwamba hauwezi kuwaendeleaza halafu wakatengeneza faida. Mtaji ni mdogo sana.

Pili hao unaowapa huo mtaji hawana taaluma. Kwa hivyo unaweza ukukakuta pahali watu wamekaa wanakwambia tumepewa kiasi fulani tunafanya hivi na ukiwauliza mnatengeneza faida kiasi gani, hawana kabisa, wala huoni kama wana mawazo ya kuweza kuuendeleaza. Nafikiri taaluma hata kama inatolewa bado haijatosha. Wizara ifanye juhudi ya kutoa taaluma kwa kila kikundi. Halafu na mtaji utakao wapa uwe unakidhi haja. Kikundi cha watu 20 au 30 unakwenda kuwapa laki tano wazifanye nini, mtu mmoja hasimtoshi. kutengeneza *profit*. Hili ni jambo moja la kuzingatiwa sana.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo kwa kweli niliposoma hiki kitabu nilifurahia sana. Kuna mpango wa kutayarisha vikundi vya wazazi vitakavyosimamia ulinzi na malezi ya watoto katika kila shehia. Hili kwa kweli ni jambo la kutiliwa mkazo sana. Kwa sababu wanatwambia wazee sisi hatufahamu. Siku hizo lakini walivyokuwa wakilelewa wale wazee wetu ili kuwa hawalelewi na baba na mama tu, walikuwa wakilelewa na jamii nzima. Kama mtoto kafanya kosa basi kila mtu anakayemuona yule mtoto kafanya kosa basi ana wajibu wa kumrudi lile kosa. Jambo ambalo utamaduni huo katika zama hizi tulizokuwa nazo sisi umepotea sana.

Kama Mhe. Waziri anaunda vikundi hivi kwa kweli mimi nafurahia sana na kuna haja sasa ya jamii kupewa taaluma hiyo. Kwa sababu inawezekana sana mbele yangu mimi mtoto wangu hatofanya kosa hata siku moja kwa sababu ataogopa nitamtia bakora. Mimi nitaendelea kumtia bakora akifanya kosa, lakini takuwa anafanya makosa huko pembeni pembeni. Sasa kama wazee watakaomuona huko hawatamnyoosha basi kwa kweli mzee peke yake hawezi kumlea mwanawe hata siku moja. Kwa msingi huo ni wajibu wa jamii nzima. Ndio maana nikasema nafurahishwa sana na hivi vikundi. Kwa sababu kila mtoto atakuwa na hofu ya kufanya kosa popote pale alipo. Kwani anajua popote nikifanya kosa hata kama baba hayupo lakini aliyekuwepo atanitia abadu au atarekebisha. Au hamna hamna atakwenda kumwambia baba kwamba mwanao kafanya jambo kadhaa.

Hii ni faraja sana kwa kweli na nampongeza sana Mhe. Waziri katika hili na namuomba sana hili alipekipaumbele cha hali ya juu. Sio kuandika humu tu halafu Mhe. Waziri asiyafuatilie. Mimi napenda sana hili alifuatilie na halafu tuweze kuona tathmini ya mwaka hadi mwaka tumefanikiwa katika kiwango gani.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi nataka niungane na wenzangu kwa kuunga mkono hoja hii mia juu ya miya.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata nafasi ya kuchangia mawili matatu katika Wizara yetu hii ya

Wanawake, Vijana na Watoto. Kwanza mimi nakwenda moja kwa moja katika bajeti.

Mhe. Spika, wizara hii ni wizara iliyochukua gurupu kubwa la wanawake, watoto na vijana. Magurupu haya ni magurupu ambayo yanataka kutizamwa kwa macho ya huruma sana kwa sababu ni magurupu yenye watu wengi hasa gurupu la wanawake na watoto. Mhe. Spika, katika nchi inavyotakiwa vijana wawe ni asilimia 60, wazee wawe asilimia 40. Lakini kama wazee watakuwa wengi kuliko vijana basi nchi hiyo haiwezi kupata maendeleo. Kwa hivyo, kuna kila hali ya kuwatizama vijana, wanawake na watoto. Kwanza naingia kwenye vijana.

Mhe. Spika, vijana wa nchi hii si wengi wenye ajira rasmi, wengi wanajiajiri wenyewe huko mitaani, kuna wafanyabiashara, kuna wakulima, kuna wafugaji, kuna wavuvi. Lakini hawa wanataka kutazamwa kwa sababu hawaendi mbele kwani hawana mitaji ya kutosha ya kufanyia kazi zao. Vijana wengi wanafanyabiashara za jua kali, lakini hawaendi mbele wala hawawi wabunifu wazuri kwa sababu walichonacho mkononi kinachumia tumbo tu, waende wakahangaike mchana kutwa wapate kitu waje wale na watoto kesho watoke wakahangaike tena.

Mhe. Spika, vijana kama hawa hawana akiba ya kujiwekea kwa ajili ya maendeleo ya watoto wao na wao wenyewe. Ni kwamba kwa sababu hawana mitaji wanaanza biashara zao wakiwa katika hali duni kabisa. Kwa hivyo, jambo hili haliwezi kumkwamua katika hali aliyonayo ya umasikini yeye kila siku atakuwa anachumia tumbo tu. Mhe. Spika, kwa hivyo vijana kama hawa wanataka kutizamwa sana na hii wizara haiwezi hata kuwaita pengine ikawafanyia semina kwa fupi fupi, kwani bajeti yake inayopangiwa na serikali ni ndogo.

Mhe. Waziri wa Fedha vipi huko mbona sisi kila siku hii wizara yetu unatupa pesa kidogo kwa sababu bila ya wanawake hili taifa litakuwaje, litakuwa haliwi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunaiomba serikali hii wizara kama wanaitaka kweli ifanye kazi basi waipe fedha za kutosha sio waipe fedha kidogo waambiwe tu kama na wao wamepewa. Mhe. Spika, hivyo haitatupeleka mbele.

Mhe. Spika, suala jengine ni wanawake kushiriki katika maoneshe mbali mbali. Wanawake wa Zanzibar wanashiriki katika maoneshe lakini maoneshe yao mengi wanaoshiriki ni ya saba saba hapo Dar es Salaam. Mhe. Spika, kwa kweli bado hawajenda na bidhaa zilizo makini zikaweza kushindana na masoko ya kimataifa yanayoingia au hata Soko la Afrika ya Mashariki. Mhe. Spika, hii yote ni kwa sababu hawana ujuzi wa kutosha wakuingia katika ushindani wa masoko katika maoneshe. Mhe. Spika, ukenda katika maoneshe ya saba saba

utakuta wanawake kutoka Kenya, Uganda, Burundi na nchi mbali mbali wako pale wanaingia na bidhaa zao.

Mhe. Spika, wanawake wa nchi za wenzetu kila yanapofanyika maoneshe wanawake wa nchi za wenzetu wanakwenda na vitu vyao vizuri ambavyo vinaingia katika masoko. Hata maoneshe yakawa nchi za nje, basi wanawake wa nchi mbali mbali wanasaidiwa kufika katika hayo maoneshe ya kimataifa lakini wanawake wetu sisi hawaendi kwa sababu mwisho wao ni hapo Dar es Salaam hawaingii katika maoneshe makubwa makubwa na kama wanaingia ni wachache.

Mhe. Spika, wanawake wa Zanzibar ni wajuzi sana wa mambo mbali mbali kwa kazi hizi za mikono na ndio nyingi zinakuja katika maoneshe. Lakini kwa sababu hawana nyenzo na pengine wamo majumbani tu hawajatafutwa, hawajashajihishwa utakuta ndio hatuwezi kuingia katika maoneshe haya ya kimataifa. Kwa kweli sisi hatujaweza bado hivyo wizara hii ikishirikiana na wizara nyengine wawezeshwe wanawake hawa ili wapatiwe wataalamu ili wasomeshwe ni namna gani unaweza kuingia katika maoneshe ya kimataifa na bidhaa zako zikapata soko.

Mhe. Spika, jambo jengine ni safari za kujifunza wanawake na vijana wale ambao wana hamu ya kujiendeleza katika shughuli mbali mbali ni kwamba watafutiwe safari za kwenda kujifunza wasibakie tu hapa petu. Mhe. Spika, kwa sababu kusafiri ni kusoma kama hujasafiri basi bado hujasoma, usafiri wende ukatazame mambo ya wanzako wanafanya vipi ili na wewe ukirudi kwenu uweze kufanya jambo kama lile.

Mhe. Spika, kama tutawaacha humu humu ndani ya nchi basi hawa maisha hawatojifunza na hawatopata maendeleo. Mhe. Spika, mambo haya hayaji kama hii wizara haikupewa fedha za kutosha. Kwa hivyo, naiombea sana wizara hii ipewe fedha za kutosha ili iweze kukabiliana na changamoto walizonazo.

Mhe. Spika, katika wizara hii kuna wafanyakazi wazuri tu na kuna wataalamu wazuri lakini wanashindwa kufanya hizi kazi kwa sababu ya fedha wanazozipata ni kidogo. Vile vile katika nchi yetu hii ya Zanzibar kuna rasilimali nyingi, lakini kwa sababu ya uchache wa utaalamu rasilimali hizi zinapotea. Kwa mfano, katika msimu huu *alhamdulilahi* tuna machungwa ya kutosha sana, ingelikuwa kuna wanawake ambao wana ujuzi mzuri na wana fedha basi wangelifanya *juice* za matunda wakatia ndani ya chupa na wakaweza kuuza.

Mhe. Spika, hapa ndani ya Zanzibar nathubu kusema kwamba hakujawa na chuo cha wajasiri amali cha kuwasomesha vijana wakaweza kufanya hizi kazi

na wakatumia rasilimali tulizonazo wakaweza kujipatia fedha. Kwa mfano, Zanzibar ina embe nyingi wakati ule wa msimu wa embe yanapoanza basi wenzetu huwa wanatumia hizi embe changa kwa kufanya achari ya embe na iko madukani inauzwa. Mhe. Spika, wengine wanathubutu kusafirisha pengine kupeleka Dar es Salaam, kupeleka katika mahoteli mbali mbali. Mhe. Spika, ni nzuri kwani inaingia katika masoko na inakubalika.

Mhe. Spika, ni vijana wangapi wa Zanzibar wenye ujuzi kama huo, ni wachache mno na ni wale ambao wameweza kupata fedha wakenda wakasoma katika vyuo vilivyoko vya Dar es Salaam. Mhe. Spika, ingelikuwa watu wana uwezo wa kwenda kujisomea au hapa Zanzibar kuna vyuo vya kuweza kuwasomesha ndio hii wizara niliposema mpaka ishirikiane na wizara nyengine.

Wizara hii ingelitoa watu kwa sababu yeye ana watu lakini wengine wakatoa vyuo kama Wizara ya Kilimo ili kuwasomesha hawa vijana watakaopelekwa na Wizara ya Kazi Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto japo watakuwa na fedha zao. Wakishakusomeshwa wakirudi wataweza kutumia rasilimali tulizonazo ndani ya nchi na wakaweza kuzifanyia kazi wakaweza kuendesha maisha yao.

Lakini madhali hakuna hayo ndio vijana wetu unakuta wanadhagaa tu hawana kazi za kufanya, wanakaa vijiweni hawana walilonalo ndio hatimae wanaingia katika madawa ya kulevya na mambo mengine yaliyokuwa hayana maana, na wanawake wakati mwengine wanaingia katika hali ya kujiuza miili yao. Hili ni jambo baya ndio matokeo yake madawa ya kulevya, kujiuza na ndio ukimwi unazidi kuenea katika visiwa vyetu vya Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi ningeliomba ubunifu wa utumiaji wa rasilimali katika nchi yetu uwepo lakini uwe na vyuo. Mhe. Spika, wizara hii kwa kushirikiana na wizara nyengine wabuni vyuo japo vidogo vidogo vitakavyoweza kusaidia wanawake na vijana ili wakapata kujiendeleza maisha yao wao na watoto wao.

Mhe. Spika, ikiwa wataweza kusomeshwa hawa basi bidhaa zao wataweza kuziongezea thamani. Mhe. Spika, ilipopitishwa Wizara ya Biashara hapa nilijaribu kusema kwamba wakati wa kutimia pesa za Wazanzibari ni huu wakati wa mwezi wa Rajabu, Shaabani na Ramadhani, huu ni wakati Wazanzibari tunatumia pesa nyingi sana kwa sababu sote tunakabiliana na Ramadhani halafu mbele kuna sikukuu. Mhe. Spika, kila mzazi wa hapa Zanzibar mara nyingi watoto wetu wanavaa nguo nzuri mwaka mara mbili, ni sikukuu ya mfunguo mosi na sikukuu ya mfunguo tatu.

Kwa hivyo, hapa kila mzazi anataka ajipinde aone kama mtoto wake anavaa vizuri. Mhe. Spika, Zanzibar pana washonaji wazuri wa nguo za watoto lakini

kwa vile hawana mitaji ndio pale anasubiri kitambaa changu mimi nimpelekee tena hapo anipe thamani ya vitu nitakavyopeleka anitoze fedha. Mhe. Spika, ingelikuwa hawa wana mitaji mizuri basi bidhaa zao zingeongezeka thamani kwa sababu wangelipewa mikopo wakanunua vitambaa hata kama nchi za nje kama ni kikundi cha watu wawili au watatu basi ingewasaidia.

Mhe. Spika, unaweza kumpa mwanamke mkopo au kijana lakini kwa sababu hajui kuutumia mkopo ule akauharibu, matokeo yake lile lengo likawa halikufikiwa. Mhe. Spika, lakini kama watakuwa na ujuzi, uzoefu halafu wapewe hii mikopo na ushauri mzuri ili waweze kushona nguo au mashuka kwa nini tununue nje kila siku wakati Wazanzibari wengi ujuzi huu wanao. Hili ni jambo linalotaka kushajihishwa kupitia wizara yetu hii ya wanawake na watoto lakini hawawezi kujishajihisha kama hawana pesa kwa sababu mambo haya yanahitaji pesa na yanahitaji mafunzo ili kuwatoa hawa wanawake waliomo ndani wakaja nje yote haya yanataka fedha, ili wanawake waweze kutoka kuliko walivyotoka hivi sasa kwa kuzitia thamani bidhaa zao watakazozitengeneza wakaziingiza katika maduka ya hapa Zanzibar na zikaweza kupata thamani ya kununuliwa na wao wakaweza kujiendesha kimaisha.

Mhe. Spika, hapo hapo ndio pale niliposema lazima kuwe na mafunzo ya utumiaji wa hiyo mikopo, unaweza kunipa mimi mkopo lakini sijui hata niutumie vipi matokeo yake nalipa mkopo ule lakini haukunileta tija na madeni yako pale pale. Mhe. Spika, ina maana ule umasikini ulioutarajia mimi nitauondoa ikiwa sikupata mafunzo ya kitaalamu basi ule umasikini hauwezi kuondoka. Mhe. Spika, haya yote yanakuja pamoja na uwekaji wa mahesabu hawa wanahitaji wafunzwe na miradi iweze kuwa endelevu.

Mhe. Spika, wanawake wengi au asilimia kubwa ya Wazanzibari wanategemea maisha yao katika kilimo, na huko katika kilimo wanaolima zaidi ni wanawake. Mhe. Spika, ukibahatika kwenda mashamba hasa siku hizi za mavuno ya mpunga basi ukitoka huku Mjini mpaka ukiingia Kaskazini huko mashamba mengi utakuta ni wanawake ukiwakuta wanaume ni wachache sana. Kilimo chao wanachokilima mpaka sasa hivi bado ni kile kile kilimo cha kizamani hawapati tija. Kwa hivyo, wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ingeliwapatia semina hawa wanawake wakulima na namna gani ya kutunza mazao ili wakaweza kutumia kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, kinachosikitisha ni kwamba hata hiyo semina ikipelekwa basi utakuja kuwakuta wengi waliomo katika hiyo semina ni wanaume wameshajipeleka wao mbele kama mfuko wa shati. Mhe. Spika, na wakati wao sio wanaotenda kazi za kilimo, watenda kazi za kilimo ni wanawake. Lakini wanawake hawa wanataka walime katika kilimo cha kisasa ili wapate masoko ya mazao yao yaliyo mazuri ili waweze kujikwamua wao na watoto wao.

Mhe. Spika, vile vile kuna *TASAF* kwenye mradi huu wengi ni wanawake kule Pemba tulipokwenda katika kamati watu wa *TASAF* walitusikitikia kwamba wakishakuwasomesha hawa vijana hasa wanawake na watoto wengi wanaingia katika kufuga kuku hasa kuku wa kienyeji. Mhe. Spika, ni kwamba hawa wanapata mayai mengi lakini wanasikitika kwamba mayai yanawaozea majumbani hawana masoko.

Mhe. Spika, ningemwambia Mhe. Waziri angelishirikiana na watu wa *TASAF* ili wakawapatia masoko kwa sababu masoko Unguja yapo, lakini namna gani wasafirishe wenyewe haya mayai mpaka yaje hapa Unguja inakuwa kwao ni mtihani kwa sababu hawajui wafanye vipi. Lakini kwa kweli katika *TASAF* Pemba mayai ni mengi yanaoza na wanawake hawana pakuyauzia wamepoteza nguvu zao nyingi.

Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kabla sijasahau naunga mkono hotuba hii mia juu ya mia.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kupata wasaa huu kuweza kuchangia machache na hasa kujaribu kumsaidia Mhe. Waziri kwenye hoja zile zilizogusa mambo ya fedha, na mimi niungane na wenzangu kabla sijasahau naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, waheshimiwa wengi sana walielezea wasi wasi wao au wameitaka serikali kuiongezea bajeti wizara hii. Mimi naungana nao ni kweli kwamba pesa tunazowapa ukilinganisha na wizara nyengine ni kidogo. Lakini hii ina sababu yake na sababu zake hasa ni msifu sana Mhe. Spika, Mhe. Moh'd Ali Salim alipochangia nimesema amemaliza kazi, ile kazi yangu nitakayosema ameimaliza yeye nikamwambia Mhe. Waziri kwamba majibu yote ameshayatoa Mhe. Mulla.

Mhe. Spika, nafikiri na waheshimiwa wengi walizungumza kwamba hii ni wizara MTAMBUKA inagusa wizara zote na kazi yake kubwa ni kuratibu na Mhe. Mulla alikwenda mbali zaidi akasema ingefaa Mhe. Waziri ujitahidi ukutane na wenzako. Nafikiri amezungumza suala la msingi kweli kweli mimi yamenigusa hasa kwa sababu hizi programu zako nyingi unakutana na wenzako.

Mhe. Spika, akatofa mfano kuhusu masuala ya elimu, masuala ya ujasiri amali, masuala ya kilimo. Kuhusu masuala ya elimu ni watoto na vijana, masuala ya wajasiri ni Wizara ya Biashara, tukenda Wizara ya Kilimo wakulima wengi ni wanawake, lakini mwenye ile sekta ni kilimo. Kwa hivyo, sisi kama Wizara ya Fedha yule ndiye mwenye shughuli kwa mfano za umwagiliaji. Mhe. Spika,

shughuli za umwagiliaji hatuwezi kumnyima pesa mtu wa kilimo tukampa Mhe. Waziri wa Wizara ya Kazi yeye huyu anaratibu tu, lakini yule ndiye mwenye shughuli kwa hiyo tukimnyima yule ule msingi Mhe. Subeit hautochimbwa ule.

Kwa hivyo, lazima tumpe yule tukimtaka yule tumpe huyu itakuwa kidogo kwenye mipango wanasema hayendi hivyo ndio maana unaona ki-*pacentage wise* kwa ule uzito wa shughuli tunampunguzia. Lakini kweli kabisa tunakubali yeye ana uzito wake na umuhimu wake wa kuwatetea wanawake, watoto na vijana. Mhe. Spika, rai iliyotolewa ni nzuri sana na mimi naiunga mkono, hizi shughuli kuziratibu vizuri basi Mhe. Waziri lazima ashirikiane na wenzake ili waende pamoja.

Kwa mfano, kwenye hotuba yake aligusia kwenye ukurasa wa 16 paragraph ya 23 programu ya JP5 ya kujenga uwezo wizara. Alisema programu hii inalenga kutekeleza mkakati wa kupunguza umasikini Zanzibar kwa njia ya kuongeza ajira, kujenga uwezo kwa taasisi za serikali na binafsi katika kutekeleza sheria za kazi, kutoa mafunzo kwa wajasiri amali, kuweka mfumo imara wa hifadhi ya jamii kwa wote nchini na kujenga uwezo kwa taasisi husika katika utkelezaji wa Sera ya Ajira na mpango wa kukuza ajira kwa vijana.

Kwa hivyo, miradi yake mingi Mhe. Waziri kama nilivyoeleza ni *cross cutting* na zaidi wao wako kwenye shughuli za uratibu. Nakiri kwamba kweli kwa shughuli zao zinatanuka na sisi kama Wizara ya Fedha hatuna wajibu twende na wakati twende na wao. Kwa hivyo, nakiri kwamba fedha ni kidogo kwa hiyo tutaongeza.

Mhe. Spika, nilichogundua kwamba katika kuripoti nafikiri ni wizara yake tu na hili tatizo Mhe. Haji Omar Kheri alikuwa akilizungumza kwamba tunaripoti mpaka mwezi Machi. Kwa hivyo, kwa mwezi wa Machi utakuta pesa zilizoripotiwa kidogo ni chache, lakini kesho nafikiri mmeshapata vitabu vya Wizara ya Fedha naomba muangalie kuna jadueli kule mwisho juu ya pesa zote zilizoingizwa katika mawizara kuanzia Julai mwaka 2009 mpaka Juni 2010 utaziona zila *percentage*.

Kwa kweli ni nzuri tu sasa sitaki kwenda ndani kwa wizara hii lakini naomba tufungue ukurasa wa 76 kunaonesha malipo mengineyo kwa kipindi cha Julai hadi Juni 2010 hayo ndio malipo mengineyo. Mhe. Spika, kwa kweli wizara hii imepata asilimia 87 hizi ndio *figure* zetu za Wizara ya Fedha mpaka Juni juzi tu hapa ukilinganisha na *recurrent* nayo ni *figure* nzuri tu katika ukurasa wa 82 Wizara ya Kazi Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ni asilimia 87 ni nzuri tu. Lakini ndio nasema wakati waliporipoti wao walipotengeneza jadueli mwezi Machi ilikuwa bado hatujamaliza na unajua siku zote kupanga matumizi ni kupanga, hatuwezi kuwapa tu huwa tunakwenda kwa *quarter* na *MTEF* na

hasa kwa mfano kwenye miradi ya maendeleo tunaangalia *activities* walizofanya na *returns* wanazoonesha.

Mhe. Spika, kama hawakurudisha *return* Wizara ya Fedha huwa hatutowi fedha, hiyo ndio mikakati ya Wizara ya Fedha lazima waoneshe *return* kazi wamefanya vipi hapo ndipo wanamaliziwa zile fedha zilizopo. Kwa hivyo, ndio utakuta pengine mwisho ndio unamalizia return nzuri na pesa zinamalizwa kabisa.

Mhe. Spika, niseme kwamba ile michango wanaotupa waheshimiwa kwamba tuwa-*improve* pesa zao kwa kweli tunajitahidi kwani huwa tunawapa chote kile walichoomba, lakini kama nilivyosema na wao *activities* zao zinatanuka basi na sisi tutazidi kuwanononesha kadri hali inavyokwenda.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala la Mhe. Haji Faki Shaali nakumbuka aliulizia kwamba hii miradi ya maendeleo wizara haziripoti kwenye bajeti yake. Tumegundua ni kweli baadhi ya wizara kwamba hawaziripoti na ingepaswa waziripoti zile pesa za *recurrent* na za maendeleo ngapi. Wizara nyengine tunashukuru wanazitaja, lakini kwenye *audit* hili hatusemi kwamba sio suala la SMZ ni kwamba miradi hii ni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Spika, hawa ni wafadhili wetu tu kwa hiyo lazima wanafuata taratibu zetu.

Kwa hivyo, wakifuata taratibu zetu ndio miradi hii yote iko *subjected* kukaguliwa na Mkaguzi wetu Mkuu wa Serikali. Mhe. Spika, kwa kuongezea hii miradi wana wafadhili wao nitatoa mfano labda *USAID*, *World Bank*, *IFAD*, *ADB*, *NORAD* hawa hawaamini kabisa pengine wanaona labda ukaguzi wetu tutapendeleana tu huwa wanaleta na wakaguzi wao. Mhe. Spika, nashukuru kwa kweli tunakwenda vizuri sana wakaguzi wao wote wana-*prove* ndio maana tunamaliza mradi mwengine tunaomba *phase* nyengine. Nakumbuka kama Wizara ya Elimu wametoa mpaka zawadi kabisa kwa *project manager* wale vipi wanavyotunza miradi ile ya *USAID* na miradi ya *ADB* na mpaka zimebaki pesa wakasema basi tuanze kwa ujenzi.

Mhe. Spika, nakumbuka lile jengo la Wizara ya Elimu Mhe. Haroun Ali Suleiman alitwambia hapa walijenga lile kwa kuanzia kilichobaki kwenye mradi hilo walifurahi sana wakasema nyinyi ni watu wa ajabu kweli maana yake ule uwajibikaji wetu kiasi ulivyokuwa mzuri. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Shaali kwamba kweli *observation* yake kwamba hatuzi-*mention* hili hizi pesa za miradi lakini ni vyema tukazi-*mention*. Mhe. Spika, hata hivyo utaona sisi Wizara ya Fedha kwenye bajeti yetu wizara zote hizi tunazitaja, lakini kwenye ukaguzi ni vyema kweli wanakaguliwa hawa na SMZ lakini pia *external auditors* wao wenye miradi wanakuja.

Mhe. Spika, suala la tatu ambalo Mhe. Said Ali Mbarouk aligusia ni suala la ujenzi wa wizara Pemba. Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali ina mpango kabambe wa kujenga wizara mbali mbali za serikali kule Pemba na tumesema twende hatua kwa hatua. Mhe. Spika, hatuwezi wizara zote ambazo hazina ofisi Pemba tukazijenga kwa pamoja. Niseme usimamizi unafanywa na Wizara ya Fedha usimamizi wenyewe zaidi ni kwenye mapesa.

Mhe. Spika, kwenye kutafuta ramani, kwenye kutafuta kiwanja, michoro hili ni jukumu la wizara yenyewe na wanafanya wenyewe, lakini Wizara ya Fedha tunashughulikia tu zile *activities* na tumeanza na wizara mbili, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji pamoja na Wizara hii ya Kazi Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Nafikiri tumeonesha hata pesa zitakazotumika kwa mwaka huu wa fedha kwa kuanzia angalau watafika mahala pengine mwakani tutaendelea. Kwa hivyo, si kama hili suala ni la Wizara ya Fedha Mhe. Said yupo nje bahati mbaya nakumbuka alitania alisema wenyewe Wizara ya Fedha hawajiwezi jengo lao linaporomoka inachukua ya wengine mambo haya vipi.

Mhe. Spika, sisi hatuchukiwi ya wengine narudia ile kauli yangu kwamba sisi sio wataalamu wa ujenzi, wataalamu wa ujenzi tuwaachie wenyewe kina Mhe. Hamad Masoud na wengine sisi sio wajenzi ile imetokea ajali tu tutakuja kuielezea kidogo. Kwa hivyo, niseme kwamba sisi tunasimamia kwenye masuala ya fedha na ule ujenzi wenyewe kwa ujumla.

Mhe. Spika, nimalizie kama nilivyosema kwamba tatizo hasa kwamba keki yetu ni ndogo, tungependa wapate asilimia 100 na baada ya kuiona ile keki ndio hii ya bajeti ndio tunagawana kwa *ceiling* wewe chukua hiki, wewe chukua hiki kwa zile hoja zenyewe zilivyo na kwa ule uzito wa wizara yenyewe. Lakini ni kwamba hatuna lengo hilo hii wizara ni ya dada yangu tunapenda mkinonoka nyinyi ndio tumenonoka sisi. Kwa hivyo, kuna haja ya vijana wetu kuwatizama wasile unga, wasile bangi, lakini ni kwamba tushirikiane sote kwa pamoja.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza kabisa nikushukuru tena kunipa nafasi hii ya kuja hapa kufanya majumuisho. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya na kuniwezesha kusimama mbele ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu kujibu masuala na hoja mbalimbali za wajumbe walizozitoa katika kuchangia Bajeti ya wizara yangu kwa mwaka 2010/11.

Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia bajeti ya wizara yangu. Ni imani yangu kuwa hata wale ambao

hawakupata nafasi ya kuchangia wote wameunga mkono hoja yangu, hivyo wote nawashukuru kwa dhati kabisa.

Mhe. Spika, natanguliza shukrani zangu za kipekee kwa Waheshimiwa Wajumbe wote walioona, kuthamini na kutambua umuhimu na majukumu mazito ya wizara hii na kwamba bajeti ni ndogo na hivyo kuongezwa kulingana na majukumu yake. Pia nimeridhika kwa kauli ya Mhe. Waziri wa Fedha kusema kwamba hilo atazingatia na fedha na fedha zitaongezwa ili wenzetu watakaoshika wizara hii kwa kipindi kijacho wasipate matatizo kutekeleza yale majukumu ambayo wananchi wanategemea wayafanye katika wizara hii.

Michango, maoni, ushauri na masuala yote yaliyotolewa na wajumbe ni muhimu katika utekelezaji wa kazi zetu, hivyo tunayapokea na tunaahidi kuyafanyiya kazi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kwa heshima na taadhima niwataje wajumbe wote ambao waliopata nafasi ya kuchangia hotuba yangu.

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.
2. Mhe. Aziza Nabahani Suleiman (Waziri Kivuli wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto).
3. Mhe. Haji Mkema Haji
4. Mhe. Said Ali Mbarouk
5. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi
6. Mhe. Rashid Seif Suleiman
7. Mhe. Ali Abdullah Ali
8. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
9. Mhe. Haji Faki Shaali
10. Mhe. Zahra Ali Hamad
11. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
12. Mhe. Hija Hassan Hija
13. Mhe. Mohammed Ali Salim
14. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
15. Mhe. Najma Khalfan Juma
16. Mhe. Ame Mati Wadi kachangia kwa maandishi.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Ali Suleiman Ali Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mchango na ushauri.

Ushauri uliotolewa na Mhe. Ali Suleiman ni sawa na wa Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe, Said Ali Mbarouk na Mhe. Ali Abdalla Ali, juu ya kuwa makini katika sheria ya mtoto na kwamba iangalie mila, silka na maadili ya Mzanzibari.

Ushauri huo tumeupokea na tutaufanyia kazi na kuhakikisha sheria hiyo itafanyiwa kazi kwa mujibu wa maadili ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Suleiman pia alishauri serikali inunuwe chombo cha *DNA.* Naomba kumhakikishia kwamba, wizara yangu itachukua juhudu ya kuishauri serikali pamoja na wizara husika kuweza kuwa na chombo hicho ili kurahisisha utambuzi wa nasaba na ushahidi wa watu wanaodhalilishwa kijinsia.

Kuhusu suala la wananchi wanaoajiriwa huko Arabuni ambalo liliulizwa na Mhe. Ali Suleiman, wengi wao ni kwamba wanachukua kazi hizo kienyeji na hawafuati sheria na taratibu zilizopo. Lakini wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa jamii ili wafuate taratibu na sheria zinazopaswa kuchukuliwa na mwananchi ambae anatapa ajira nje ya nchi, ili iwe rahisi kumfuatilia anapopata matatizo.

Vile vile napenda kumshukuru Mhe. Aziza Nabahan Suleiman, Waziri Kivuli wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa uchanganuzi wa masuala mbali mbali yanayohusu wizara yangu yakiwemo masuala ya ajira katika soko la pamoja la Afrika ya Mashariki, kusaidia sekta binafsi katika kuzalisha ajira zaidi, maslahi ya kazi, matatizo ya ajira katika sekta binafsi, kutilia mkazo elimu ya ufundi na ujasiriamali, masuala ya haki za watoto yakiwemo elimu, malezi, maadili na afya. Yote tunayazingatia kwa kina.

Mhe. Spika, kuhusu masuala ya maji, afya, barabara na athari zake kwa wanawake, wizara yangu itaendelea kushirikiana na taasisi husika kuhakikisha inalipatia ufumbuzi ili kuondoa kero kwa wanawake kuhusiana na nyanja hizo.

Mhe. Aziza Nabahan, Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Zahra na Mhe, Said Ali Mbarouk walionesha wasi wasi mkubwa kuhusu soko la pamoja la Afrika Mashariki, ambalo limeanza rasmi tarehe 1/07/2010 katika sekta ya ajira. Soko hilo linakusudiwa kutoa uhuru kwa waajiriwa kwa wananchi wa Afrika Mashariki katika nchi yoyote, lakini kanuni za itifaki za soko hilo imezitaka nchi wanachama kufungua milango kwa fani wanazozihitaji tu. Tanzania kwa kuanzia imefungua katika sekta ya elimu na afya. Zanzibar imefungua kwa walimu wa sayansi katika skuli za sekondari na Vyuo Vikuu. Aidha, watu watakaoingia nchini watafuata taratibu zote za kisheria zikiwemo vibali vya kazi, ukaazi na Pasi za kusafiria.
Mhe. Spika, Mhe, Aziza pia, Mhe. Ali Abdalla Ali na Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi walizungumzia suala la watoto wanaodhalilishwa na kungizwa katika masuala ya kuombaomba pamoja na suala la kutenganishwa watoto katika Vyuo vya Mafunzo na kuingizwa katika ajira za watoto. Napenda kuwahakikishia wizaza yangu inalifanyia kazi na itazidi kulifanyia kazi suala

hili ikishirikiana na taasisi husika kwa yale masuala ambayo hayahusiani moja kwa moja na wizara yangu. Pia itashajihisha wazazi na walezi ili tushirikiane kuongeza nguvu zetu kukabiliana na tatizo hili.

Mhe. Haji Mkema Haji wa Jimbo la Koani alizungumza kuhusiana na umuhimu wa maziwa ya mama kwa watoto. Wizara yangu inalipokea na tutashirikiana na wizara husika waangalie kama kuna uwezekano huo. Vile vile, wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhakikisha kwamba, tunatoa taaluma zaidi kwa kinamama kuona umuhimu wa kunyonyesha watoto maziwa ya mama ambayo ndio yenye ubora zaidi wa kujenga mtoto kimwili na kiakili.

Mhe. Spika, Mhe. Haji Mkema pia aligusia suala la matatizo ya usafiri Pemba. Wizara yangu inapokea ushauri wake na tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wazidi kuiombea wizara yetu kuongezewa bajeti ili iweze kumudu kununua vyombo na wizara ipate kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Tumesikia kauli za kuthibitishwa kwa Mheshimiwa anayeshughulikia masuala ya fedha kwamba itaongezwa bajeti hii na labda pengine tutaweza kufikia yale matarajio yetu.

Mhe. Haji Mkema alitoa pendekezo la kuanzishwa Mfuko wa Vijana wa milioni hamsini kwa kila Mkoa. Wazo ni zuri na linahitajiwa kufanyiwa kazi. Hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tushirikiane na wizara yetu ili kuona wazo hili linafanikiwa.

Mhe, Spika. suala la Mhe. Said Ali Mbarouk, ni kweli wizara yangu imekadiriwa jumla ya shilingi milioni sitini (60,000,000/=) kwa ajili ya kazi za maendeleo, fedha hizi ni mshango wa serikali pekee. Lakini suala hili pia limepata ufumbuzi wa kina kutoka kwa Mhe. Waziri Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi Dr. Mwinyihaji Makame kwa hivyo naona sina haja ya kulitolea majibu tena.

Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Said Ali Mbarouk kuhusiana na majukumu ya Idara ya Maendeleo ya Jamii na Idara ya Ustawi wa Jamii kwamba yanaingiliana.

Idara ya Maendeleo ya Jamii inashughulikia zaidi kuhamasisha jamii kujiletea maendeleo yake kama kuchangia shughuli za miradi ya maendeleo ya kijamii kama elimu, upatikanaji wa huduma za kijamii na kadhalika na kutoa taaluma kwa kamati za maendeleo ya jamii.

Kwa upande wa Idara ya Ustawi wa Jamii, shughuli zake zinajikita zaidi katika masuala ya ustawi kama vile kutoa huduma kwa wazee wasiojiweza, watoto wanaoishi katika mazingira magumu, watoto yatima na kadhalika.

Mhe. Spika, Mhe. Rashid Seif na Mhe. Makame Mshimba. Naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, mikataba ya kazi ipo tena kwa lugha zote mbili, Kiingereza na Kiswahili na waajiri wamepatiwa ili kuwapa wale wote ambao wanaomba ajira katika taasisi binafsi. Ila naomba kukubaliana na wajumbe kwamba, bado wapo baadhi ya waajiri wasiokuwa waaminifu ambao hawafuati taratibu na sheria za kazi. Wizara yangu itaendelea kufuatilia na kusimamia ili kuhakikisha wafanyakazi wote wanapatiwa mikataba.

Mhe. Rashid Seif alitaka Kamisheni kwa kushirikiana na Idara ya Utumishi Serikalini kufanya utafiti wa nguvu kazi nchini. Ushauri huo tunaupokea na tutashirikiana na wenzetu kuufanyia kazi. Aidha, Mhe. Rashid Seif alitoa ushauri wa mikopo na misaada kuelekea kwenye uzalishaji. Ushauri huo pia tunauchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mkema Haji Mkema kwamba Mfuko wa Uwezeshaji sasa hivi hauko tena kwenye majaribio, bali unafanya kazi zake kwa maeneo yote. Na fedha za awamu ya kwanza zimeshamalizika na sasa hivi Benki ya Watu wa Zanzibar imeingiza fedha zao kwa kuwakopesha wananchi.

Napenda kumjibu pia Mhe. Said Ali Mbarouk kwamba watoto wenye vipaji waendelezwe. Hili ni suala zuri na wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Elimu na Vyuo vya Amali kuhakikisha suala hili linafanyiwa kazi na watoto wote wenye vipaji wanaendelezwa. Nimezungumza na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alipoingia hapo, amenihakikishia kwamba hilo halitakuwa tatizo na suala hilo litapewa kipaumbele.
Mhe. Spika, napenda tena kumjibu Mhe. Haji Faki Shaali pamoja na Mhe. Zahra Ali Hamad kuhusu suala la uundwaji wa Kamati za Kuchunguza Vitendo vya Udhalilishaji wa Wanafunzi.

Suala hili ni miongoni mwa mapendekezo ya wanafunzi wenyewe waliyoyatoa katika midahalo iliyozungumzia juu ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia pamoja na mbinu za kujilinda na vitendo hivyo. Kwani ilionekana wapo baadhi ya walimu wanafanya vitendo vya udhalilishaji. Maoni hayo yalitolewa na watoto wenyewe na ni kwamba, sio lengo letu kusema walimu ndio wanaohusika na udhalilishaji lahasha, ila tu wako wakorofi wachache ambao wamo katika jamii yetu wanaofanya mambo hayo na sio lazima wawe walimu. Lakini watoto wenyewe ndio walitoa kauli hiyo katika maoni yao.

Mhe, Aziza Nabahan, Mhe. Ali Abdalla Ali na Mhe, Rashid Seif walitaka kujua kupanga viwango vya mishahara vinahitaji wataalamu kutoka nje? Naomba niwaeleweshe kwamba, wizara imeamua kufanya utafiti kuhusu kima cha chini ili kujua hali halisi za wafanyakazi na uwezo wa waajiri kulipa. Aidha, utafiti utaelekeza mfumo bora zaidi wa kupanga kima cha chini katika

sekta za umma na binafsi. Utafiti huo unafanywa na wataalamu wa hapa hapa nchini.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Abdalla alitaka kujua migogoro ya kazi ni mingapi imetatuliwa. Sasa namuomba sana angalia ukurasa 77 na 78 kiambatisho 5a na 5b ambavyo vimeonesha taarifa hiyo kwa ufasaha kabisa. Aidha, alitaka taaluma ya mikopo itolewe. Naomba pia nimuarifu kwamba, taaluma hiyo inatolewa na itaendelea kutolewa.

Mhe. Spika, Mhe. Haji Faki Shaali aliuliza kuhusu mpango wa kukuza ajira. Naomba nimuarifu kwamba, mpango wa kukuza ajira unalenga kuhamasisha vijana wa Unguja na Pemba kujiunga katika sekta isiyorasmi ili kujiajiri katika maeneo mbali mbali ya kielimu, biashara, uvuvi na ufugaji. Aidha, wale ambao tayari wameanzisha juhudi za uzalishaji wamepatiwa mafunzo ya kuzalisha kwa tija na namna ya kupatiwa mikopo na misaada mbali mbali.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alitaka kujua kuhusu uwiano wa wakimbiza mwenge baina ya Tanzania Bara na Visiwani. Naomba nimweleweshe kwamba, wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa wanakuwa ni sita, uwiano wa ugawaji ni Tanzania Bara 3 na Zanzibar 2. Nafasi ya Kiongozi ni ya kubadilishana kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, akitoka kiongozi Tanzania Bara hivyo Bara watakuwa watatu na akitoka Zanzibar, basi wakimbizaji watakuwa watatu.

Utaratibu huo unafanywa kwa kubadilishana, mwaka huu ikiwa watatu wametoka upande ule, basi mwaka unaofuata itakuwa watatu wanatoka upande huu. Na kwa sababu wizara hii nimo mimi na ninashughulika na mambo haya, ukandamizi wala uonevu kwa mambo hayo haujatokea.

Mhe. Spika. Mhe. Ali Abdalla Ali alitaka kuelewa kituo cha majaribio cha miradi ya kiuchumi. Naomba nifahamishe kwamba kituo hicho bado kiko katika maandalizi huko Muungoni Unguja. Fedha zilizolengwa kutekeleza ujenzi huo hazikutosheleza, lakini wizara inaendelea na mazungumzo na wafadhali kuongeza fedha hizo ili kituo kiweze kujengwa na kutoa huduma iliyokusudiwa. Michoro na sehemu imeshafyekwa iko tayari tunangoja hizo fedha na kuanza jengo hilo mara moja.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Haji Faki Shaali suala lake kuhusu kutoa taarifa kwa waomba kazi na wajasiriamali. Azma kubwa ya kituo hiki ni kutoa taarifa za nafasi za kazi zilizopo nchini kwa kutoa fursa kwa vijana wetu kuweza kuzifahamu ili waweze kuzihozi na kupunguza uwezekano wa nafasi hizo kuchukuliwa na wageni.

Aidha, kituo hiki kitatumika kuzitangaza bidhaa zinazotengenezwa na wajasiriamali wa Zanzibar. Na kuhusu suala la kukabiliana na uharamia wa biashara za mtandao, wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kuwaelimisha wajasiriamali wetu juu ya mbinu hizo na utaratibu mzuri wa kuendesha biashara na kuweka taratibu zitakazowakinga na uharamia huo.

Mhe. Spika, Mhe. Zahra alitetea sana wizara yangu katika suala zima la kuongezewa bajeti. Namshukuru sana pamoja na Mhe. Najma Khalfan na waheshimiwa wengine wote waliyoona umuhimu wa wizara hii. Naomba niwaunge mkono sana kwa vile wizara yangu ni MTAMBUKA na inagusa wizara nyingi, inahitaji kuwa na bajeti ya kutosha ili kufanikisha kazi zake kwa ufanisi pamoja na kuwashirikisha wajasiriamali katika maonesho ya nje ya nchi pamoja na kujifunza kuwa wenzao wanafanya nini.

Nakubali sana kwamba mimi na Mhe. Zahra Ali mara kwa mara huwa tunapata bahati ya kusafiri nchi za nje, lakini sote kwa umoja wetu hatujaweza kufuatana na wajasiriamali kutokana na ufinyu wa bajeti. Lakini bajeti itapokuwa imeongezeka na watu watakapokuwa wameona umuhimu wa kuwaendeleza wanawake kwa staili hii ya kusafiri na kwenda kujifunza, naamini tutaweza kuwasafirisha wanawake wengi wakajifunze.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Haji Faki Shaali ambaye alionesha wasi wasi sana kuhusu utatu. Naomba kumhakikishia kuwa utatu upo na tunafanya kazi kwa pamoja. Taasisi za Utatu zipo zinafanya kazi vizuri. Kwa mfano, zimeundwa bodi za ushauri wa mambo ya kazi, Bodi ya Ushauri ya Mshahara na Mahkama ya Kazi, Jumuiya za Uajiri na za Wafanyakazi zinashirikishwa. Nakubali kwamba ipo haja ya kushirikisha Jumuiya ya Waajiri katika mambo yote ya uwezeshaji na uajiri. Naiona haja hiyo na ninakuhakikishia kwamba nitashauriana na wenzangu tuone namna gani tunaoanisha mambo hayo ili sote tuwe katika uwazi na kufahamu nini kinachoendelea.

Pia napenda kumjibu Mhe. Said Ali Mbarouk ambaye alihoji juu ya maelezo ya ufafanuzi wa fani za masomo zilizotolewa na wizara hii kwa mwaka 2009/2010. Nataka nikiri kwamba, hapo ulikuwa ni pungufu kwa kweli ilikuw ani muhimu kuonesha hao watu wamesoma nini.

Wizara katika mwaka 2009/2010 iliwapatia mafunzo wafanyakazi 31 katika fani mbali mbali na mchanganuo wake ni kama hivi ifuatavyo:-

Shahada ya pili wafanyakazi 6
Shahada ya Maendeleo ya Sera - 2
Shahada ya Biashara na Utawala - 3
Shahada ya Sanaa (Kiswahili) - 1

Shahada ya kwanza wafanyakazi 5
Shahada ya Sayansi ya Jamii – 1
Shahada ya Uhusiano Kazini – 1
Shahada ya Maendeleo – 1
Shahada ya Utawala wa Fedha -2

Diploma wafanyakazi 11
Diploma ya Uchumi- 1
Diploma ya Utawala na Raslimali – 4
Diploma ya Ustawi wa Maendeleo ya Jamii -1
Diploma ya Habari – 1
Diploma ya Utawala wa Fedha – 2
Diploma ya Sheria -2

Cheti wafanyakazi 6
Cheti cha Raslimali watu – 4
Cheti Uwekaji Kumbukumbu -2

Kozi fupi wafanyakazi 3
Kozi ya Ukutubi – 1
Kozi ya Uwezeshaji na Ujasiriamali Wanawake – 1
Kozi ya Maendeleo ya Wawezeshaji Wadogo Wadogo na wa Kati -1

Sasa Mhe. Spika, nitaendelea kujibu masuala mengine ambayo yalijitokeza hapa. Kwa hivyo, utanivumilia kidogo.

Mhe. Said Ali Mbarouk pia alizungumzia sana suala la Mfumo dume uliopo unaowanyima wanawake ajira. Mhe. Spika, sheria za ajira zimekataza ubaguzi wa aina yoyote, wanawake na wanaume ni sawa katika ajira, lakini kweli ajira bado ni ndogo kwa wanawake hasa katika sekta binafsi. Wizara yangu inaendelea kutoa elimu kwa waajiri wa vyama vya wafanyakazi pamoja na wanawake wenyewe ili kushajihisha ajira kwa wanawake.

Mhe. Mohammed Ali Salim yeye alilaumu sana na nafikiri pia alikuwa ananilaumu mimi. Nimepokea hizo lawama zake kwamba sisi wanawake ni waoga, lakini sisi siwaoga tunajipanga vyema tu, lakini tutajikita huko kwenye majimbo na mtapata habari zetu.

Mhe. Spika, Mhe. Mohammed pia alisema wanawake wanaonekana kupata mikopo zaidi ukilinganisha na wanaume. Ni kweli kama ilivyooneshwa hapa, lakini wizara itashajihisha wanawake wengi kuomba mikopo zaidi na kuwasaidia kuwapa elimu juu ya kukuza miradi ili iwe mikubwa, jambo ambalo litasaidia kuwakwamua kiumasikini. Vile vile tutaongeza juhudi ya kuwasaidia kuandaa miradi ambayo watapoipeleka Benki isipate kipingamizi.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla alilalamika juu ya malezi na maadili na kwamba alisikitishwa sana na alikuwa anaogopa tusije tukabadilika tukaacha kutumia desturi zetu za kuwagomba watoto hata kuwapiga ikibidi. Kwa hivyo, mimi na wenzangu nafikiri tunakubaliana na hayo kwamba tutaendeleza na ulezi wetu kama tulivyolelewa sisi mpaka tukawa hivi. Kwa sababu na sisi pia tumepigwa ngumi lakini hazikutuuwa na tupo mpaka leo hapa. Kwa hivyo, sisi hilo tumeliona na tutaendela kupokea ushauri na kuona kwamba hii sheria haitotukwaza.

Mhe. Mohammed Ali Salim aliulizia kuwa lengo la kukiimarisha kitengo cha ajira limetekelezwa. Napenda kulieleza Baraza lako tukufu mchakato wa kukiimarisha kitengo unaendelea, deski la kukusanya takwimu za kazi limeanzishwa na takwimu zimeanza kukusanywa. Lakini kwa sababu bado deski ni changa, takwimu na uchambuzi hazijakamilika, lakini takwimu za kazi zitasaidia kujua uhalisia wa wataalamu wa ndani na hivyo kudhibiti ajira kwa wageni.

Mhe. Hija Hassan aliulizia juu ya wizara kuhusu malalamiko yanayotolewa, kwamba kwa nini sehemu nyengine ni mengi na sehemu nyengine ni kidogo. Ni kwamba watu kwa sehemu za mijini wamepata muamko wa kuripoti matokeo kama hayo haraka sana, lakini sehemu nyengine bado hawajapata hali hiyo, lakini tunaamini matatizo yapo na kwamba yataendelea kuripotiwa ili hatua zichukuliwe.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis aliulizia Mfuko wa Uwezeshaji unaoendelea kutolewa unatolewaje na kwa ulingano upi. Alikuwa analalamika kwamba labda sehemu nyengine huu Mfuko wa Uwezeshaji hauwafikii. Ni kwamba mgawanyo ulikuwa kila mkoa upate shilingi mia mbili na Mkoa wa Mjini umepata shilingi milioni mia mbili na milioni mia nne. Kwa hivyo, kila mkoa ulipata sehemu yake ni namna gani watu wanavyochangamka wao wenyewe kujaza fomu na kuandika miradi na kuomba hizo fedha.

Kwa hivyo, yeye naye akiwa kama Mwakilishi achangamkie kufuatilia huko kwenye mkoa wake ili kuona wananchi wake wanafaidika na faida hizi ambazo ziko na zinategemea kuongezwa. Lakini pia elimu ya matumizi ya fedha imetolewa na bado inaendelea kutolewa.

Mhe. Spika, Mhe. Mohammed Ali Salim aliuliza kuhusu kile kituo kinachofanya mafunzo kwa ajili ya watoto yatima. Ushauri alioutoa tumekaa kati ya maafisa wa wizara yangu na maafisa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali limeshafanyiwa kazi na tayari wale walimu wataajiriwa na wameshaitwa Wizara ya Elimu Pemba kwa hatua ya utekelezaji kwa hivyo, tatizo la kituo hicho limeshamalizika.

Tathmini ya vikundi. Inaonekana vikundi vya Pemba vinafanya vizuri zaidi na kutumia vitendea kazi walivyonavyo sawasawa. Kwa hivyo, wizara itaendelea kuwapatia mafunzo na mahitaji ya zana za kazi na kuwajengea uwezo zaidi wa kiutendaji. Haya yatafanywa kwa vikundi vyote.

Mhe. Mohammed Ali alizungumzia kuhusu Kamati ya Udhibiti wa Kesi za Unyanyasaji wa Kijinsia kwa upande wa Pemba. Kamati hizi tayari zimeshaundwa kwa Mkoa wa Kaskazini na Mkoa wa Kusini Pemba. Mchakato wa uundaji wa kamati hizi sehemu nyengine unaendelea.

Mhe. Hija Hassan Hija alizungumzia kuhusu takwimu za kesi za udhalilishaji. Hili limeshajibiwa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niseme nimejitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu na kadiri ya udogo wa wizara yangu. Kwa sababu wizara yangu inaonekana ndogo mpaka humu Barazani, ndio ninapewa siku moja tu ili nimalize kila kitu. Kwa hivyo, kwa muda huo niliopewa nimejitahidi kutoa majibu hayo. Ahsante Mhe. Spika, kwa kunifanyia ukatili kama huo.

Mhe. Spika: Sasa sijui tutoke tu bila ya kujibu kam ahoja imekubaliwa au laa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, wizara yako ilikuwa haina matatizo na ndio maana wachangiaji wakawa wako kidogo na hakuna aliyekataa. Sasa niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja hii ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Maymuna13
Mhe. Spika: (Anaendelea) ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Fungu 28 - Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake naWatoto

Kifungu 08 -	Kamisheni ya Kazi	54,288,000
	Jumla ya Fungu	**54,288,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 28 - Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto

Kifungu 03 -	Ofisi Kuu Pemba	180,640,000
Kifungu 04 -	Idara ya Mipango na Sera	525,142,000
Kifungu 05 -	Idara ya Wanawake na Watoto	87,500,000
Kifungu 06 -	Idara ya Maendeleo ya Jamii	53,900,000
Kifungu 07 -	Idara ya Maendeleo ya Vijana	73,330,000
Kifungu 08 -	Kamisheni ya Kazi	165,488,000
	Jumla ya Fungu	**1,086,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 28 - Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto

Kifungu 04 -	Idara ya Mipango na Sera	2,418,730,000
Kifungu 05 -	Idara ya Wanawake na Watoto	110,000,000
Kifungu 07 -	Idara ya Maendeleo ya Vijana	1,017,360,000
Kifungu 08 -	Kamisheni ya Kazi	183,990,000
	Jumla ya Fungu	**3,730,080,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaoafiki makadirio hayo wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kufanya kazi ya wizara hii iwe nyepesi. Nimeombwa nitoe taarifa kwamba kesho mnamo saa nane mchana katika jengo la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pale Mazizini kutakuwa na shughuli muhimu ya utiaji sahihi kwa ajili ya skuli za sekondari tatu. Hizo ni za Mwenda, sijui kama ni Mwendawima au wapi sina hakika, Matemwe na Chaani.

Vile vile wiki ijayo kutakuwa na kazi kama hiyo kwa upande wa Pemba kwa skuli zote za wilaya za Pemba. Nimeombwa niwaarifuni hivyo lakini inaombwa Kamati ile ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii wao wangefika hasa pale wizarani ili wakaone kazi ile muhimu. Lakini bila ya kusahau kwamba kesho saa kumi na moja tutakuwepo hapa, wasije wakamaliza kazi hiyo wakasambaa. Kwa hiyo, wakimaliza kazi hiyo tunarudi hapa saa kumi na moja jioni.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo, sasa naomba niahirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 14 Julai, 2010 saa tatu barabara za asubuhi ambapo Wizara ya Fedha watasoma bajeti yao.

(Saa 1:10 Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 14/7/2010
saa 3:00 asubuhi)